ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32 Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50. Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne – Tarehe 20 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 127

Afisi za Kibalozi Zanzibar

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Kwa vile Zanzibar ni nchi ina haki kuwa na afisi za Balozi mbali mbali kwa njia ya kudumisha Umoja wa nchi hizo.

(a) Je, ni nchi ngapi zimefungua Afisi zake hapa Zanzibar.

(b) Kwa zile nchi ambazo hazijafungua Balozi zake hapa Zanzibar. Je, serikali inachukua juhudi gani kuzishawishi nchi hizo kufungua afisi zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 127 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, hadi tarehe ya leo jumla ya nchi tano ndizo zenye Ofisi za Balozi ndogo hapa Zanzibar ambazo ni:-
1. China
2. India
3. Misri
4. Msumbiji
5. Oman.

Kadhalika nchi kama vile Uingereza, Sweden, Norway na Denmark zinazo Balozi wa heshima hapa Zanzibar.

(c) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapendelea kuona nchi mbali mbali zilizo na ofisi za balozi hapa Tanzania zinafungua ofisi za balozi ndogo hapa Zanzibar. Lakini utaratibu wa kufungua ofisi za kibalozi ni uamuzi wa nchi husika kulingana na maslahi ya nchi hizo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwasiliana na ofisi mbali mbali za kibalozi zilizopo Dar es Salaam ili zifungue ofisi zao hapa Zanzibar pindi wakiona ipo haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, mafupi yanayolenga moja kwa moja kujibu swali lenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa sababu masuala ya mahusiano ya kimataifa yanahusu pande mbili mbali ya nchi nyengine kufungua ofisi zao hapa Zanzibar, lakini pamoja na haja ya Zanzibar kusimamia maslahi yake nje ya nchi. Na pamoja na kwamba suala la mambo ya nje ni suala la Muungano, lakini kwa sababu mara nyingi kumekuwa na malalamiko kwamba ofisi za Balozi za Tanzania zimekuwa hazihudumii ipasavyo Zanzibar na wakati fulani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuamua kufungua baadhi ya ofisi katika baadhi ya maeneo kwa mfano, Dubai, Indonesia na kwengineko.

Je, serikali kwa hivi sasa haioni pamoja na hali yake ngumu ya uchumi kuna haja hata katika yale maeneo machache yenye maslahi moja kwa moja na Zanzibar kufungua ofisi ndogo za Ubalozi hata kama ni ofisi za biashara ili kusimamia maslahi ya Zanzibar katika maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ukweli nchi yetu inayo matatizo makubwa ya kiuchumi na kadiri inavyotokea njia, mbinu ama nafasi ya kusaidia kukua kiuchumi ni jambo la busara sana kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Ushauri wa Mhe. Ismail Jussa tunaupokea tutaufanyia kazi kwa maslahi ya Zanzibar na maendeleo ya nchi yetu.

Nam. 16

Upungufu wa Watumishi Wataalamu katika Hamlashauri za Wilaya ya Chake Chake

Mhe. Mohamed Haji Khalid – Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi katika Halmashauri za Wilaya hususan Pemba kuwa zina upungufu mkubwa wa watumishi hasa wataalamu ili kuzisaidia Halmashari hizi kufanya kazi zao kwa ufanisi.

(a) Je, Mhe. Waziri unaelewa kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake na nyenginezo zinakusanya mapato madogo kwa sababu ya uhaba wa wakusanyaji kodi.

(b) Je, unafahamu kwamba Halmashauri yako ya Wilaya ya Chake Chake na nyengine hazina Wanasheria na kupelekea taasisi hizo kukosa mapato yake. Kutokana na udhaifu katika masuala ya kisheria.

(c) Je, unachukua hatua zipi ili kurekebisha tatizo hili la upungufu wa wataalamu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, naelewa na nakubaliana na Mhe. Mwakilishi juu ya kuwepo upungufu wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake na nyenginezo kadhaa.

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika sikubaliani kwamba hiyo ni sababu kubwa ya kukosa mapato katika Halmashauri na Mabaraza ya Miji, kwani hali hiyo inajionesha katika ripoti zao wenyewe ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ambayo katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Machi, 2012 walikadiria kukusanya shilingi 26,480,000/- lakini waliweza kukusanya shilingi 34,813,201/- hii ikiwa ni sawa sawa na asilimia 131.47.

Mhe. Naibu Spika, hali hii ya ongezeko la mapato inaonekana takriban kwa kila Halmashauri na Mabaraza ya Miji kwa kipindi hiki. Hii inadhihirisha kwamba mafanikio waliyoyapata yanatokana zaidi na mabadiliko makubwa katika utendaji wao na hasa katika kuweka malengo halisi na kufanya kazi kitaalamu.

(b) Mhe. Naibu Spika, naelewa vile vile kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake na baadhi ya nyengine hazina wanasheria. Hata hivyo, Halmashauri kukosa mapato si sababu ya ukosefu wa hao wanasheria kama alivyoeleza na nilivyoonesha hizo takwimu hapo awali. Vile vile Mhe. Naibu Spika, wizara pamoja na serikali kwa ujumla hutoa kila msaada wa kisheria kwa wakati huu penye upungufu huo wa wanasheria ili waweze kukabiliana na changamoto ya kisheria inapohitajika.

Pia wizara iko mbioni katika kupata au kuwaajiri wanasheria kutumia katika Halmashauri hiyo ya Wilaya ya Chake Chake.

(c) Mhe. Naibu Spika, katika kurekebisha tatizo la upungufu wa wataalamu, ofisi yangu imechukua hatua ya kuwasilisha maombi rasmi katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kutupatia wataalamu na wafanyakazi wengine ili tuweze kuondosha tatizo la upungufu wa nguvu kazi katika Halmashauri ya Chake Chake na nyenginezo.

Aidha, juhudi zimeanza kwa kushirikiana na wizara hiyo niliyoitaja kuwapata wanasheria na maafisa mbali mbali kwa njia muwafaka ikiwa ni pamoja na kufanya uhamisho kutoka Idara moja hadi nyengine. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa maafisa hawa wanasheria na maafisa wengine watendaji katika Halmashauri za Unguja wameajiriwa zamani ni jambo gani lililozuia mpaka leo ikawa huko Pemba hawajaajiriwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikujulishe tu kwamba Mhe. Mohamed Haji ni mjumbe wa Kamati inayosimamia wizara yetu, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na suala hili tumewafahamisha mara nyingi sana kwamba kulikuwa na tatizo la kitaalamu la utendaji kuwa yalipokuja maombi ndio wakati ule tunaipitisha ile Sheria ya Utumishi wa Umma na kuunda zile kamati zote au tume. Kwa hivyo, maombi yao kidogo yalikwama kwa wakati ule. Sasa kumalizika yale ndio mishahara ilipopandishwa na ikawa tunafanya utaratibu wa kupandisha mishahara na tukaona tulivyokwama kwa idadi ya mishahara. Sasa ombi lipo, linafanyiwa kazi na namuahidi Mheshimiwa kwamba naamini ndani ya miezi mitatu ijayo litakamilika.

Nam. 60

Watumishi Kuwajibika Zanzibar

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein, katika ziara zake kisiwani Pemba na Unguja amekuwa akisisitiza sana suala la uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kuharakisha maendeleo ya Zanzibar, lakini bado uwajibikaji ni tatizo kwa watumishi hao.

(a) Je, sababu gani zinapelekea watendaji wakuu kushindwa kusimamia majukumu yao ya kuruhusu tatizo la uvivu na utoro kuendelea kujitokeza katika maeneo ya kazi ikiwemo wimbi la ruhusa za harusini, maulidini, mazikoni jambo ambalo hupunguza ufanisi wa kazi.

(b) Je, Wizara ina mkakati gani wakuhakikisha wafanyakazi wake wanakuwa na mpango kazi wa wiki hadi mwezi ili kujitathmini katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 60 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein katika ziara zake Visiwani Unguja na Pemba amekuwa akisisitiza sana suala la uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kuharakisha maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la uvivu, utoro, ruhusa za harusi, maulidi na mazikoni ni mambo ambayo kweli hupunguza ufanisi wa kazi na kupoteza muda wa kazi ikiwa watumishi hawatosimamiwa ipasavyo. Miongoni mwa sababu zinazopelekea watendaji wakuu kushindwa kusimamia majukumu yao ni muhali. Kwa kuwa tabia hii ya muhali imejengeka kwa miaka mingi si rahisi kuondoka kwa mara moja. Hata hivyo, kila mmoja wetu kwa pale alipo lazima atekeleze wajibu wake ipasavyo na kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Serikali imechukua hatua ya kuweka Sera ya Utumishi wa Umma inayoelekeza na kuweka taratibu za uwajibikaji, utendaji na usimamizi katika Utumishi wa Umma, pia Sheria ya Utumishi wa Umma imetoa nguvu za utekelezaji wa sera kwa kuweka adhabu za kumchukulia mtumishi wa umma ambaye ni mvivu, mtoro au asiyewajibika. Nawaomba watendaji wakuu wa wizara na taasisi za umma kujiamini na kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuondoa muhali.

(b) Kwa sasa kila wizara ina mpango kazi wa robo mwaka ambao kila idara baadae hutayarisha mpango wa mwezi na bila shaka kila mtumishi hupangiwa majukumu ya kufanya kwa kila siku. Suala zima la tathmini ya utendaji limewekewa fomu maalum ya upimaji xw3 utendaji wa wafanyakazi ambayo mfanyakazi hupata nafasi ya kujitathmini na kutathminiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na kutueleza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kueleza utoaji wa adhabu Mhe. Waziri atatueleza ni hatua gani zimechukuliwa kwa sheria hiyo katika kupambana na utoro, uvivu na kutowajibika kwa wafanyakazi.

Pili, ni lini tutaacha kuwa na sera ya sheria ambazo hazitekelezwi ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa hatua ambazo zimechukuliwa kama nilivyoahidi kwenye bajeti yangu ya mwaka jana, ni kutayarisha fomu ya kuwapima watendaji na uwajibikaji. Hatua hiyo napenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba jambo hilo liko tayari na baada ya kupitishwa bajeti ya mwaka huu tutakayoijadili hapa fomu hiyo itaanza kutumika. Tayari muongozo umetayarishwa na fomu hiyo ipo tayari.

Lakini suala zima la uwajibikaji lina maeneo mapana sana, labda niseme tu kwamba hivi sasa tuko kwenye *reform* ya utumishi na *reform* ya utumishi haiwezi ikatekelezeka siku moja lakini itachukua muda hatua kwa hatua katika kuitekeleza kwake. Kwa hivyo, la kwanza katika kujua hilo tumetengeneza hiyo fomu ya uwajibikaji lakini kuna fomu ya *Client Service Chatter* nayo ni sehemu ya *performance management system* ya uwajibikaji katika serikali, lakini pia kuna *performance contract*.

Kwa kutumia nafasi hii nataka Mhe. Naibu Spika, niwaelezee wale ambao Wajumbe wa Baraza lao tukufu kwa kuwaelimisha tu kwamba, kwenda kutekeleza uwajibikaji kwa Mhe. Rais sio kwenda kumdanganya Rais, ni *performance contract* ambayo ni mkataba kati ya waziri au waziri na Mhe. Rais, *performance contract* sio suala la mawaziri tu, lakini Katibu Mkuu ana wajibu wa kwenda kuji-*commit* au kwenda kuelezea ana wajibu kwa Waziri, Mkurugenzi ana wajibu kwa Katibu Mkuu na mtumishi wa kawaida ana wajibu kwa Mkurugenzi. Lakini hata sisi hapa Baraza la Wawakilishi tunatakiwa tuwe na *performance contract* kati yetu sisi na wananchi.

Kwa hivyo, suala la *reform* kwenye utumishi wa umma ni jambo pana sana. Kwa hivyo, hatua tulizozichukua ni pamoja na kuandaa huo utaratibu wa kuweza kufikia kuondosha huo muhali.

Suala lake la pili Mhe. Jaku Hashim naomba alirejee tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Waziri, ni kwamba lini tutaacha kuwa na sera ya sheria ambazo hazitekelezwi ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza serikali haitungi sheria ambazo hazitekelezeki, sheria zilizotungwa na serikali aghalabu huwa zinatekelezeka na pale inapoonekana kuna matatizo ya utekelezaji wa sheria ndipo pale serikali inapoleta miswada ndani ya Baraza hili kwa madhumuni ya kuzirekebisha. Kwa hivyo, sheria yoyote ambayo haitekelezeki serikali itahakikisha inaifanyia mapitio na kuileta ndani ya Baraza la Wawakilishi ili iweze kutekelezeka. Mpaka sasa sheria ambayo inasimamia watumishi wa umma inatekelezeka na ndio maana tuko katika hatua ya kufanya marekebisho na tutaendelea kufanya marekebisho pale inapohitajika kufanya marekebisho.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali imekiri kuwa utendaji wa serikali umeathiriwa na muhali na kwa kuwa Mhe. Waziri amelieleza Baraza hili tukufu kuwa tabia hii imejengeka kwa muda mrefu sana imekuwa ni vigumu kuyaondosha kwa sasa hivi.

Je, serikali kukiri kuwa utendaji wake umeathiriwa na muhali inaonesha imeshindwa kusimamia watumishi wake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza sikubaliani naye kwamba serikali imeshindwa kuwasimamia watumishi wake kama alivyosema. Ninachotaka kumhakikishia kwamba nilikiri kusema ni vigumu kuyaondoa mara moja masuala yaliyojengeka ndani ya nchi yetu katika kipindi cha muda mrefu na ndio maana serikali imekuja na *reform*

ya kuweza kuyarekebisha hayo. Pamoja na hatua tunazozichukua ndio maana tunatayarisha mikataba kwa ajili ya kukabiliana na hizo changamoto ambazo tunakiri kwamba zipo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa haki na wajibu huenda sambamba siku zote, na kwa kuwa kuna wafanyakazi wengi wa serikali ambao haki zao za msingi wanacheleweshwa sana kupata, na kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa. Kwa kuwa kuna walimu ambao hadi leo hii hawajarekebishiwa mafao yao baada ya kumaliza masomo. Kwa mfano wale waliomaliza *CAP* katika mafunzo ya ualimu, kuna madaktari ambao *night allowance call* zinachelewa. Je, ni lini serikali yetu hii tukufu itaondosha kasoro hizi kwa wafanyakazi hawa kusudi utumishi wao uweze kuwa makini kwa serikali yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba haki na wajibu ni watoto pacha na kwa kulielewa hilo serikali ndio maana ikachukua hatua ya kuweza kufanya marekebisho ya mishahara katika bajeti iliyopita ya mwaka 2011/2012. ni imani yangu kwamba wafanyakazi asilimia 99.9 wamefanyiwa marekebisho ya mishahara yao kama wanavyostahili kwa mujibu wa *qualification* zao.

Kwa upande wa walimu na madaktari kwa wale ambao hawajarekebishiwa inawezekana pengine wenyewe hawajabainisha kwamba wana kasoro katika mishahara yao, lakini pale tu ambapo wanajitokeza kubainisha kuwa mishahara yao haikuzingatia marekebisho yanayostahiki basi wizara yangu iko tayari saa yoyote kuweza kuchukua hatua hizo. Lakini naamini kwamba mpaka sasa hakuna mtu ambaye hajarekebishiwa mshahara wake kwa mujibu wa taaluma yake.

Nam. 43

Jina la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Kufuatia Mapinduzi ya Januari 12, 1964 Zanzibar ilitangazwa kuwa Jamhuri na jina lake rasmi likawa ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Jina hilo kwa muda mrefu limekuwa halitumiki tena na wala halionekani katika nyaraka zote rasmi za serikali.

(a) Ni lini jina hilo lilifutwa, chombo kipi kililifuta na kwa tangazo gani la serikali.

(b) Iwapo jina hilo halikufutwa rasmi, lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itarudisha matumizi ya jina hilo na hivyo kuendelea kuyaweka Mapinduzi ya Zanzibar katika misingi yake iliyokusudiwa kama yalivyotangazwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume katika hotuba yake kwa Taifa kupitia Sauti ya Unguja tarehe 13 Januari, 1964.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe swali lake Nam. 43 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kufuatia Mapinduzi ya Tarehe 12 Januari, 1964 Zanzibar ilitangazwa kuwa jamhuri na jina lake rasmi likiwa ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Jina hili la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar lilikuwa likitumika katika sheria ya Katiba ya Zanzibar Nam. 5 ya mwaka 1964 na hata katika sheria mbali mbali zilizokuwa zikitumika kwa wakati ule kama vile inavyotamka Sheria Nam. 1 ya mwaka 1964 ya *Legislative Powers Decree* kifungu cha 2. 2.

Baada ya kufanyika Muungano wa Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar April 26, ya 1964 na kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitunga Katiba mpya ya 1979 na kufuta Sheria ya Katiba ya 1964 ambapo Katiba hiyo kifungu cha kwanza kilielezea kama ifuatavyo:-

Kifungu cha kwanza cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979

"Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Vile vile kifungu cha pili kimesema kwamba,

> "Zanzibar ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pampoja na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar."

Katiba ya mwaka 1979 ilifutwa na kutungwa Katiba mpya ya mwaka 1984 ambayo mpaka hivi sasa inatumika katiba hiyo. Katika Katiba hiyo pia ilitambua kuwepo kwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kama ambavyo ilitambua Katiba ya mwaka 1979.

Katiba ya 1984 kifungu cha kwanza kinaelezea kwamba,

> "Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyozungukwa na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhhuri ya Watu wa Zanzibar."

Jina la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar lilifutika kutokana na Sheria na Katiba zilizokuwa zikitumika kuacha kulitumia jina hilo badala yake kubuni maneno mengine ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kama ilivyoelezewa katika kifungu cha pili moja cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata nakla ya mkataba wa Muungano katika kitabu cha Jumbe ukurasa wa 156 – 157 unaeleza jina la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Sheria Nam. 22 ya mwaka 1964 iliyotiwa saini na Mwalimu Nyerere, Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar inatoa sura ya kuliondoa jina la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kwa kusema sasa ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kifungu cha kwanza.

Jina hili lilibadilishwa tena kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuandikwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa 1977 kama ulivyo utangulizi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ukurasa wa 17 kifungu Nam. 1 na kifungu cha 2.2.

Kisheria iwapo kitu kimetumiwa kwa siku nyingi bila ya malalamiko yoyote, basi matumizi hayo yanahalalisha kitu hicho kutumika. Kwa maana hiyo jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo linalotambulika kisheria kwa wakati huu. Kwa sababu jina hili halikufutwa kisheria ni rahisi kulirudisha tena pale Wazanzibari watapoamua kulirejesha tena.

Kwa hivyo, jukumu la kuliondoa jina liliopo hivi sasa na kulirejesha hilo la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ni la wananchi na kwa kupitia wawakilishi wao kazi hiyo inaweza kufanyika kiurahisi. Zaidi ningeliomba sana kwamba, katika mchakato huu wa maoni ya Katiba suala hilo na mengineyo muhimu kama hilo basi muyaseme ili yaweze kuratibiwa vizuri kama hilo na hayo ndio matakwa ya Wazanzibari.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, kwanza niruhusu nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu fasaha na kina kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Spika, katika utafiti wangu niliofanya katika nyumba ya nyaraka nimegundua kwamba katika gazeti rasmi la Serikali ya Zanzibar (Zanzibar official gazette), jina hili kama alivyosema Mhe. Waziri liliendelea kutumika hata baada ya muungano kama ndio jina la Zanzibar. Lakini ninashukuru kwa maelezo yake kuwa suala hilo lipo mikononi mwa Wazanzibari wenyewe kuliamua.

Swali langu lipo hapa Mhe. Naibu Spika, ni kwamba iwapo wananchi wa Zanzibar iwe moja kwa moja kupitia mchakato wa maoni ya Katiba au kupitia Wawakilishi katika Baraza hili tukiamua kurejesha jina hilo ili kuheshimu msingi wa mapinduzi ya mwaka 1964, jee Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo tayari kuyaheshimu maamuzi hayo na kuyasimamia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kama nilivyosema kwamba jina halikufutwa kisheria, ni kutokana na matumizi ambayo jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio limechukua nafasi. Kwa hivyo katika ofisi ya gazeti zote hizo jina la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar bado lipo. Lakini kutokana na kuanzishwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 jina hilo lilifutika.

Sasa ikiwa wananchi wa Zanzibar wataamua kurejesha jina hili au jina jengine lolote wanalotaka, hayo ni matakwa ya wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo sisi tutaheshimu matakwa ya watu wa
Zanzibar.

Na. 88

Kituo cha Mkono kwa Mkono

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuanzisha kituo cha kushughulikia kesi za unyanyasaji wanawake ikiwemo ubakaji.

a) Jee, ni kesi ngapi hadi saa zimepelekwa katika kituo cha mkono kwa mkono
b) Kuanzishwa kwa kituo hicho kumesaidia vipi haki ya kisheria kufanyika ikiwemo watuhumiwa kukamatwa na kufikishwa Mahakamani.
c) Jee, ni kesi ngapi zimehukumiwa, na kati ya hizo watuhumiwa wangapi wamepatikana na hatia na kesi ngapi zinaendelea Mahakamani.
d) Kwa kuwa matatizo ya ubakaji yanazidi kuendelea kujitokeza Zanzibar. Jee, serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mahakama Maalum ili kesi hizo ziweze kusikilizwa haraka, hatua ambayo itasaidia kupunguza tatizo la ushahidi kuharibika kabla ya kesi kuanza kusikilizwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nichukue nafasi hii rasmi kumpongeza Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Na. 88 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kituo cha mkono kwa mkono (One Stop Centre) kuanzia Januari, 2012 hadi Mei 2012 kimepokea kesi 13 zikiwemo kesi za ubakaji 35, kesi za kukashifiwa 21 na kesi za kupewa uja uzito 27.

(b) Kuanzishwa kwa kituo kumesaidia upatikanaji wa ushahidi ambao unahitaji na kuweza kupeleka Mahakamani. Pia aliyepata matatizo ya udhalilishaji anapata huduma kwa haraka.

(c) Kwa ufuatiliaji uliofanywa na wizara ni kesi ni 6 tuambazo tayari zimehukumiwa. Kati ya hizo ni kesi 3 watuhumiwa hawakupatikana na hatia, mmoja amehukumiwa kifungo cha nje cha mwaka mmoja na faini ya shilingi laki moja, mmoja kesi yake imefutwa na mmoja amepata hukumu ya kifungo cha miaka miwili katika Chuo cha Mafunzo. Idadi ya kesi ambazo zimeripotiwa wizarani na ambazo bado zinaendelea Mahakamani ni kumi.

Mhe. Naibu Spika, serikali imelipokea wazo la uanzishwaji wa Mahakama maalum kwa ajili ya kesi za unyanyasaji na ubakaji.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wakati unajibu swali hili la msingi ulisema kifungo cha nje na faini ya shilingi laki moja, huoni hii ni adhabu nyepesi na inaweza ikachochea vitendo hivi vikaendelea vya unyanyasaji na ubakaji wa watoto

Pili, tumezoea kupokea majibu kutoka kwa Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri ya mkato, lakini utendaji hatuuoni uhalisia wa majibu hayo. Ni lini utachukua hatua thabiti za kuanzisha Mahakama kwa ajili ya kesi kama hizo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ninataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kesi ikishapatikana anayehukumu sio mimi, ni Mahakamani ndio wanaotoa hukumu. Sasa kama ni hivyo kama kuna uzembe kama hatufanyi kazi lakini yote yanamwendea huyu Hakimu, na yeye hivi ndivyo alivyoona ya kwamba ampe huyu kifungo cha nje. Lakini mimi ninavyotaka ampe kifungo cha miaka thalathini ndani.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, sijapata jibu swali langu jengine, nimeuliza kumekuwa na majibu ya mkato kwa Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri lakini uhalisia hatuuoni utendaji wake. Ni lini hiyo Mahakama itaanza kazi yake.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, sijasikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Uliza kwa utaratibu ili Mhe. Waziri apate asikie.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ninasema tumezoea kupokea majawabu kutoka kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri lakini uhalisia wa utendaji hatuuoni, lini utendaji huo utaanza kazi kwa kuanzisha Mahakama za Watoto na tumepitisha sheria hapa sisi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Jabu Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Utendaji unaonekana lakini inategemea na mtu vile anavyouona unavyotendeka. Inawezekana anafurahia au hafurahii.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika majibu yako umekiri kwamba unyanyasaji upo, na kesi umejaribu kuzitaja kwa mpangilio, lakini kinachoonekana ni kuwa kesi nyingi zinakosa ushahidi na watu kuachiliwa huru ni nyingi zaidi kuliko waliotiwa hatiani.

Vile vile katika takwimu zako inaonekana kwamba kesi nyingi bado zipo Mahakamani, na hii inasemekana kwamba inatokana na kukosekana kwa mashine ya DNA Zanzibar. Kipimo hicho kukosekana kwake imefikia pahala watu wengi hata kushindwa kufuatilia kesi zao, na hususan akiwemo mtoto mlemavu wa Kisakasaka.

Jee, wizara yako itahakikisha vipi katika kulisimamia suala hili ili liweze kutekelezeka kwa haraka na kuondosha usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kurundikana kwa kesi Mahakamani kweli kupo, sikatai lakini kesi kwa sababu tuna kituo cha *One Stop Centre* zinapelekwa Mahakamani. Sasa uchelewaji wa hukumu si kosa langu, naona ni kosa la Mahakama.

Na hichi chombo cha DNA ni sehemu moja tu ya kutoa ushahidi lakini kwa kweli ushahidi upo wazi kabisa, *One Stop Centre* inatoa ushahidi lakini bado kesi zinarundikana. Lakini hata hivyo tupo katika hatua ya kuungana na wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ili kurekebisha zile sheria za zamani ambazo zimepitwa na wakati na hazitoi sura nzuri au hazitoi mambo mazuri katika hukumu hii ya haraka haraka.

Kwa hivyo ninadhani tukimaliza kazi hiyo kesi zitakuwa zinahukumiwa kwa haraka zaidi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ninapenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kuliongezea jibu ambalo Mhe. Waziri wa Wanawake amelizungumza.

Ni kwamba sababu ya kucheleweshwa kesi ni nyingi, na moja ambayo kesi zinachelewa ni kutokana na watu wenyewe yaani jamii. Jana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na kikao na viongozi wa Polisi, DPP na Mahakama kuhusiana na masuala kama haya.

Lakini jamii hawapendi kutoa ushahidi hata kidogo. Jana tuliizungumza kesi moja wakati DPP au Mwendesha Mashtaka yupo Mahakamani, mzazi wa mtoto aliyebakwa akenda kumpelekea kikaratasi kwamba anaomba kesi yake ifutwe kwa sababu mambo haya wameshayamaliza wenyewe.

Sasa tukienda kama hivyo jamii inatuvunja moyo. Na ninawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wazungumze na jamii na watu wao kwamba haya ni masuala ya kitaifa, kwamba lazima na watu nao watupe msaada.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, katika hili hili suala la jamii ni kwamba mtoto anapobakwa wazazi wanaficha mpaka siku nne au tano ameshaonekana ndipo hapo kesi inachukuliwa. Ushahidi kama huo inakuwa ni vigumu. Ushahidi mwengine mtoto anabakwa anapata uja uzito anakaa mpaka miezi minane ndio anaonekana kwamba ni mja mzito.
Sasa suala lile mpaka yule mtoto ajifungue, akishajifungua ndio ichukuliwe kupelekwa DNA, na hii mashine ina matatizo, kwa sababu kule Tanzania Bara ni DNA moja kwa Tanzania nzima. Kwa hivyo si kwamba unapopeleka *sample* yetu sisi hapo hapo itachukuliwa hatua.

Kuna kesi zinafika hata elfu moja za Tanzania Bara yote. Kwa hivyo na sisi huwekwa katika foleni. Unaweza ukapeleka leo, ikachukua miezi mitatu bado kesi haijaletwa. Kwa hivyo tuna matatizo ya aina chungu nzima, na haya yote yanasababisha kuchelewa au kuahirika kwa kesi hizi.

Mhe. Naibu Spika, tunajitahidi lakini matatizo mengi ni haya pamoja na jamii yenyewe hawana mashirikiano hata kidogo. Tunaomba jamii itupe mashirikiano kwa kesi kama hizi ili tuweze kuwadhibiti hawa wahalifu wa aina kama hii. Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 9

Ujenzi Wa Barabara Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji (Jimbo la Kwahani) – Aliuliza :-

Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika ujenzi wa barabara ikiwemo barabara ya Amani – Dunga.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuna watu hawajalipwa fidia ya mazao tangu walipokatiwa mimea yao 2006 kupisha ujenzi wa barabara hiyo.

(b) Kama kweli huoni kwamba tathmini waliyofanyiwa ni ya muda mrefu na hivyo hadi leo kutolipwa fedha zao kumewarudisha nyuma kimaendeleo wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu **:-**

Mhe Naibu Spika**,** naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 9 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli kuna watu hawajalipwa mazao tangu mwaka 2006.

b) Ni kweli tathmini waliyofanyiwa ni ya muda mrefu, na jumla ya shilingi 28,174,107.5 wanadai kutolipwa fidia hiyo mapema kutokana na uhaba wa fedha, aidha katika mwaka huu kipaumbele chetu kitaelekezwa katika ulipaji wa mazao kwa kutambua kipaumbele cha kwanza kilikuwa kulipa fidia za nyumba.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ya kusema kwamba zimetengwa fedha za kulipa za fidia kwa nyumba, lakini kuna idadi ya watu wengi ambao wamekatiwa mimea na watu hao ni wanyonge kimaisha.

Madeni wanayodai baadhi yao Mhe. Naibu Spika, hata shilingi elfu kumi hazifiki anaidai serikali kwa muda wa miaka kumi, na wengineo tayari wameshafariki dunia.

Jee, Mhe. Naibu Waziri haoni haja ya kutafuta njia mbadala ili kuondosha tatizo la watu hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Maelezo aliyotoa Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba, kwanza tunadaiwa na muda umekuwa mrefu na kweli kuna baadhi ya watu fedha wanazotudai si nyingi. Lakini ninachokizungumza ni kwamba lile deni kwa jumla suala linalohusiana na fidia hasa ya miti ni deni kubwa.

Katika barabara hiyo ya Dunga tunadaiwa karibu shilingi milioni kumi na nane. Lakini barabara hiyo kutoka Kinyasini, kuna Tunguu tunadaiwa zaidi ya shilingi milioni hamsini na moja, na maeneo mengine tunadaiwa madeni kama haya.

Sasa unapolichukua hilo deni la mtu mmoja na kusema anadai chini ya shilingi elfu kumi, hili ni deni la serikali na limo katika ujumla wake. Sasa mimi ninaamini kwamba tukipata fedha kwa jumla hili deni tutalipunguza kidogo kidogo kwa maeneo, na sio kwa huyo mtu ambaye anadai shilingi elfu kumi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama hivi.

Kwa kuwa shilingi ya Tanzania inaendelea kupungua thamani siku hadi siku, na kwa kuwa toka deni hili liwepo ni muda mrefu, haoni kwamba kuna haja ya kufanya tathmini nyengine mpya kwa mujibu wa shilingi ya Tanzania ilivyo hivi sasa.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, haoni wizara yake kujipanga kabla ya kuanzisha mradi na kuangalia uwezo wao ili wasiendelee kuitia hasara serikali katika misingi hii kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba thamani ya sarafu yetu imeshuka na suala la fidia hili limechukua muda mrefu. Na kweli kuna uwezekano wa kufanya tathmini upya lakini tatizo hapa ni upatikanaji wa hizo fedha.

Sasa mimi ninadhani tungetumia muda huu kutafuta hizo fedha tukalipa hilo deni kuliko kuongeza mzigo wa pili ambao utatushinda, kama huu wa kwanza umechukua muda mrefu hatujaweza kuumaliza, sioni kama itakuwa utaratibu mzuri wa kujiongezea mzigo wa pili.

Lakini jibu la pili, Mhe. Naibu Spika, kinachotokea kwamba serikali inaanzisha mradi kwa mategemeo kwamba upatikanaji wa fedha utakuwa mzuri, inatokea mazingira kwa miradi ya maendeleo na jukumu la serikali mara nyingi ni kuongeza sehemu ndogo na mkono ule wa ushirika wa maendeleo.

Sasa ikiwa kila mradi tutenge fedha kabisa za fidia, basi inawezekana hata ule mkono unaotoka kwa washirika wa maendeleo nao tukaukosa. Kipaumbele cha serikali inachukua miradi hii kwa kutambua kwamba kutakuwa na changamoto ya kulipa fidia, lakini panapokuwa na fidia ya nyumba na mazao, tunatoa kipaumbele kwamba hatutovunja nyumba ya mtu yeyote kabla ya kumlipa fidia.

Tunaamini hizo fidia za mazao mtu anaweza akasubiri kwa kuona umuhimu wa ule mradi wenyewe. Sasa imani yangu kwamba wananchi nao wanafahamu umuhimu wa miradi, na wao umuhimu wao wa kuisaidia serikali katika kuinusuru miradi ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.
Kwa kuwa kuna malalamiko mengi kuhusu fidia zinazolipwa katika wizara yake kwenye ujenzi mbali mbali wa njia na viwanja vya ndege.

Jee, fedha hizo zinapolipwa hulipwa kwa vocha au kwa cash moja kwa moja.

Lakini swali la pili kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri yapo madeni ambayo wanadai katika barabara tofauti zilizojengwa. Jee, ombi hili hamkuwahi kulifikisha katika Wizara ya Fedha, kwa sababu juzi tumeambiwa zinarejeshwa shilingi bilioni tano katika bajeti iliyopita.

Sasa si bora hizo fedha mukaziomba zikalipwa kabisa kuliko kupelekwa katika bajeti inayokwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ninakubali kwamba kuna malalamiko yanayotokana na ulipaji wa fidia. Lakini malalamiko haya yote ukiyaangalia yanatokana na kima kikubwa kinacholipwa kwa wananchi wetu.

Utaratibu tunaolipa tunalipa kwa cash pia kwa utaratibu wa kulipa kwa kupitia njia ya hundi. Kwa maana ya kwamba cheque zile za benki.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, ninadhani serikali itakuwa imesikia kilio chetu kutokana na upungufu wa fedha hasa hizo za fidia, na ni kweli kwamba fidia tunazihitaji na tuna maeneo mengi, na tabaan deni ambalo tunalodaiwa kwa fidia linapita hizo shilingi bilioni tano.

Sasa serikali ni mdau na wao watakuwa wamesikia, wakiona umuhimu huo basi ninaamini kwamba wahusika watakuwa wamesikia tutalipa kipaumbele kwa kuzingatia umuhimu wa mambo mengine katika serikalini.

Na 39

Kutokomeza maradhi ya Kichocho Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Alijibu:-

Kwa kuwa kichocho ni moja ya maradhi mabaya sana yanayozalishwa na maji (water born disease). Na kwa kuwa serikali yetu tangu zamani, ilitumia fedha nyingi kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu.

Jee, serikali yetu imefikia hatua gani katika kutokomeza ugonjwa huu ukitilia maanani kwa upande wa malaria tumefanya vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, jitihada kubwa zilizofanyika hapo kabla na tumefanikiwa makubwa, na tumepunguza tatizo hilo la kichocho kutoka asilimia 60 kufikia 15 kwa Pemba na asilimia 50 kufikia asilimia 8 kwa Unguja kutoka mwaka 2000 hadi 2012.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii inaendelea kupanga na kutekeleza mikakati mbali mbali ya kutokomeza ugonjwa wa kichocho. Sasa wizara yangu ikishirikiana na Shirika la Kimarekani la Schistosomiasis Consotium for Operation Research and Evaluation (SCORE), tunaendelea na utekelezaji wa mradi wa miaka mitano kwa kutokomeza kichocho unoitwa Zanzibar Elimination of Schistosomiasis Transmission (ZEST) uliozinduliwa tarehe 28/2/2012.

Mhe. Naibu Spika, mkakati huu kuna mambo manne. Kwanza ulishaji wa dawa za kichocho kwa wananchi wote wa Zanzibar. Pili kutia dawa kwenye mito, mabwawa na sehemu zote zenye kutuama maji kwa ajili ya kuangamiza konokono wanaosababisha maradhi ya kichocho.

Tatu elimu ya afya ya kubadilisha tabia ya jamii ya kujiepusha kutumia maji ya mito na yanayotuama kwa shughuli za kibinadamu.

Nne, kufuatilia mwenendo wa maradhi ya kichocho ambapo maradhi yamejitokeza na kuhakikisha wanayatibu mara moja.

Pia kwa upande wa Mamlaka ya Maji, wao wana jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama na ya kutosha wakati wote, ili wananchi waepuke kwenda kutumia maji ya mto na yaliyotuama.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza ninaipongeza serikali kwa jitihada zake inazofanya na Mungu akajaalia wakaweza kupunguza athari za kichocho kutoka asilimia 60 mpaka 15. Kwa hivyo ninapongeza sana jitihada za serikali yetu hii, na wataalamu wa wizara hii kuweza kutufikisha hapo.
Kwa kuwa ugonjwa wa kichocho ni kama maji ya bahari yanajaa na kukupwa, na kwa kuwa nadharia za kitaalamu zinaonesha kwamba bila ya konono hakuna kichocho. Na kwa kuwa wenzetu wa China katika miaka

ya 40 walimudu kuondosha kichocho kwa asilimia mia moja pale mwenyekiti Mao alipoamua konono wote waliwe katika mto Yangze, na Wachina walikula konokono na kichocho kikaondoka kabisa.

Kwa kuwa Zanzibar mila na desturi zetu hazituruhusu kula konokono, jee Mhe. Naibu Waziri anatueleza nini Wazanzibari tutumie njia gani kusudi tuweze kuondosha konono aweze kuondoka kabisa na kuondokana na ugonjwa huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nilichozungumza hapa kwamba katika mkakati wa kuondosha kichocho kuna mambo manne yatatendeka. Moja katika mambo hayo ni kutia dawa kwenye mito pale ambapo tunajua makonokono ya kichocho wapo, katika mabwawa na sehemu zote zenye kutuama maji kwa ajili ya kuangamiza konokono wanaosababisha maambukizi ya kichocho. Kwa hivyo, hakuna haja ya binadamu nyinyi kuwala wala kufanya mengineo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ya Afya tayari imefanya tafiti mbali mbali juu ya kichocho, pamoja na kuchukua aina za wanafunzi mashuleni.

Je, ni mafanikio gani yaliyopatikana hadi sasa na ugonjwa huo bado upo unaendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mafanikio yapo, kama tumeweza kupunguza kutoka asilimia kubwa hizo na tumefikia hapo. Mimi nina imani kwamba mafanikio yapo na mikakati iliyo madhubuti sasa hivi imetengenezwa na uhakika wa dawa za kulisha wagonjwa wa kichocho tunao. Kwa sababu ni hivi karibuni tu amekuja CO wa madawa ya Kampuni ya Merick kutoka Ujerumani na akatuhakikishia kwamba atatoa dawa kwa Zanzibar na kwa Afrika nzima. Hao Wachina ambao tunaowazungumzia hapa pia tumewasiliana nao tulipokwenda Geneva, nao pia wametuahidi watalifanya hilo.

Wamesema kwamba kichocho cha Zanzibar kufutwa kinawezekana, kwa sababu kichocho cha China kilikuwa na wadudu wengi ambao wanahusika, kulikuwa na *host* wengi. Lakini sisi *host* wetu ni mmoja tu binadamu, kwa hivyo kichocho cha kwetu ni rahisi kufutika.
Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba pengine hata kabla hatujatoka madarasani sisi tuliopo kichocho kitakuwa historia kwa Zanzibar.

Nam. 182

Ajira za Vijana Nje ya Zanzibar

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Katika siku za karibuni, hapa Zanzibar kumejitokeza mawakala wazalendo kama vile *Job Center*, *Zamu Travelling Agency* na kadhalika ambao wamewaandikisha vijana wengi tu kwa madhumuni ya kwenda kufanya kazi nchi za Arabuni. Vijana hao ambao wamegharimika sana kwa usajili huo, kwa bahati mbaya hadi sasa hawajenda popote kwa kisingizio kwamba mawakala wamekoseshwa usajili na wizara.

a) Ni sababu zipi za msingi zilizosababisha mawakala hao kukoseshwa usajili katika nchi yao wakati sheria ya ajira nam. 11 ya 2005 haikatazi ajira nje ya nchi.
b) Kwa kuwa wenzetu wa Tanzania Bara na jirani zetu wa Kenya wamelivalia njuga suala hili na kuwanufaisha vijana wao kwa kuwapeleka kufanya kazi katika nchi hizo. Mhe. Waziri haoni kwamba kulifanyia uzembe suala hili ni kuzorotesha maendeleo ya vijana nchini.
c) Mhe. Waziri anawapa ahadi gani vijana wa Kizanzibari ambao wamechoshwa na hali ya ukosefu wa ajira hapa nyumbani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 182 kama ifuatavyo. Lakini kwanza naomba kutoa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, ajira kwa vijana ni tatizo na changamoto inayoikumba na kuitikisa dunia hivi sasa. Hali hii ipo kwa sababu vijana ndio wengi katika jamii na ndio nguvu kazi, takwimu nyingi za dunia hasa za nchi changa na zinazoendelea zinaonesha kuwa kundi la vijana ni kubwa ambapo fursa za ajira ni chache, hali inayopelekea vijana wengi kuachwa wakiwa hawapati fursa za ajira hasa ajira zenye heshima. Matokeo yake nchi huingia katika mifarakano ya kijamii na utegemezi wa kifamilia na uvunjwaji wa taratibu za kisheria. Sote

tunasikia matatizo makubwa yanayotokea sehemu mbali mbali duniani hivi sasa na hatua za serikali zinazochukuliwa za kurekebisha hali ya uchumi na mengineyo ili kukinga kuvunjika kwa amani na kuwatuliza vijana hao.
Mhe. Naibu Spika, aidha, kutokana na mfumo wa utandawazi na mabadiliko mbali mbali na mwenendo wa kidunia, serikali pekee haiwezi kutatua tatizo hili. Lakini kwa kushirikiana na taasisi binafsi na wananchi na vijana wenyewe. Serikali iweke, sera, mifumo, taratibu na mikakati ya pamoja ya kuunganisha jamii na kusimamia sera na sheria. Jambo jema zaidi katika ulimwengu huu ni kwamba binadamu yuko huru kufanyakazi katika nchi yoyote au chombo chochote ilimradi tu awe amefuata sheria, kanuni na miongozi ya nchi pekee na nchi anayokwenda kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa misingi hiyo vijana wetu wamo katika kufuatilia fursa za ajira na wanayogharimika. Pia zipo taasisi wakala ambao zimeelezwa nazo zimelenga kutafuta fursa za ajira kwa lengo la kuwasaidia vijana, wizara yangu imeifahamu hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 182 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, sababu za msingi na ya awali iliyokwamisha kutopatiwa usajili wa kampuni ya uwakala wa ajira ilikuwa ni kutokamilika kwa taratibu za kanuni kutokana na maelekezo ya sheria nambari 11 ya mwaka 2005. Sheria hii ilikuwa inaipa mamlaka serikali tu kusimamia ajira za nje. Kutokana na hali na mahitaji ya ajira kwa vijana wetu wizara iliamua kutunga kanuni ambazo sasa zitatoa fursa kwa kampuni kama hizo kushughulikia ajira za nje. Mhe. Naibu Spika, kanuni imeanza kazi mwezi Mei mwaka huu wa 2012 na tayari kampuni ya *Zamu Travelling Agency* imeshapewa hati ya uwakala wa ajira baada ya kufuata taratibu za sheria na kanuni. Hadi sasa ni kampuni tatu za uwakala zimechukua fomu za maombi, lakini kampuni ya Zamu pekee ndio iliyorejesha na kufanyiwa ukaguzi na kupewa hati hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana mdhamini wa kampuni hii kwa jinsi alivyolifuatilia suala hili hili na hatimaye likakamilika.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu haijalifanyia uzembe suala la ajira kwa vijana na hasa kwa ajira za nje. Wizara inaangalia suala hili kwa umakini wa hali ya juu ili kuhakikisha kwamba wanaopata fursa za ajira ndani na nje ya nchi, basi wanapata ajira zenye heshima ambazo zimelindwa na sheria. Aidha, kila atakayepata fursa mkataba wake wa kazi uwe wazi na ufahamike, nani mwajiri kwa kazi gani ama sharti gani ya kazi. Aidha, fidia iwe wazi ikiwa mtu ataumia au kufariki akiwa kazini, au kwa sababu za kikazi. Kwa hivyo, wizara inashirikiana sana na taasisi mbali mbali za ndani na nje kama Idara ya Uhamiaji, Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Kazi na Ajira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baadhi ya ofisi za kibalozi zetu za nchi za nje, nazo pia tumekuwa tukishirikiana nazo hasa zile za nchi za Kiarabu.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi, wizara imeshafanya mkutano na kampuni tano (5) zilizoitikia wito wetu wa kuzungumzia taratibu za kisheria za uwakala na uwajibu wa uwakala katika shughuli hii. Wizara vile vile imeweka katika mpango wake wa kazi wa mwaka 2012/2013 mafunzo ya wakala ili kuwajulisha zaidi namna ya mikataba mbali mbali ya kimataifa inavyoweza kutekeleza suala hili na sheria na kanuni zetu.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tumejitahidi sana na tutaendelea na inahakikisha kwamba inawapenda sana na kuwathamini sana vijana wake. Kama nilivyotangulia kusema kwamba tatizo hili ni kubwa na linahitaji ujasiri na umakini wa kulitatua. Kwa mwaka huu wa fedha, serikali kupitia wizara yangu imetenga shilingi 1,100,000,000/- kwa kutekeleza mpango wa ajira kwa vijana. Aidha, katika mpango mwengine wa kiwizara na serikali, vijana watapatiwa mafunzo mbali mbali ya ujuzi wa kujiajiri, kuanzisha vyama vya ushirika na kupatiwa mikopo yamasharti nafuu, ili kuweza kujiajiri.

Aidha, wizara yangu itaendelea kuwaunganisha vijana wetu na waajiri wa ndani na nje kwenye fursa za ajira. Pia wizara itaendelea kufanya mazungumzo na nchi marafiki kutupatia fursa za ajira ziliopo nchini kwao. Zaidi tunaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kukabiliana na tatizo hili ambalo ni agenda kuu ya Shirika la Kazi Duniani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kina na ya fasaha kabisa. Naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza. Moja katika majibu yake amesema kwamba baada ya kukamilisha kanuni tayari kampuni ya *Zamu Traveling Agency* imefanikiwa kupata usajili. Naomba anisaidie ni nini kimekwamisha usajili wa hii kampuni ya *Job Center* ambayo nimeitaja katika swali langu katika hayo matatizo.

La pili Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Waziri katika majibu yake, kwamba ingependeza zaidi shughuli hizi zingeweza kufanywa na serikali. Nakumbuka mwaka jana alituahidi katika Baraza hili kwamba serikali ilikuwa inafuatilia fursa hizi za ajira katika nchi za Qatar na Oman, kwenye swali ambalo nililiuliza mimi. Alituahidi kwamba ndani ya mwaka wa fedha ambao unamalizika leo suala hili lingekuwa limepatiwa ufumbuzi na kwamba wawakilishi tukae mkao wa kula, kwamba tungepata fursa hizi kupitia kwa vijana kutoka katika majimbo yetu. Lakini mwaka umemalizika fursa hizi hatukutangaziwa katika Baraza hili kama ambavyo likuwa ametuahidi.

Sasa katika kipindi hiki Mhe. Waziri anatuambia nini sisi wawakilishi ambao tumewajengea matumaini vijana wetu kwamba fursa hizi zipo katika nchi za Qatar na Oman na kwamba wizara yake ingesimamia na hatimaye kuzipitisha kwa wawakilishi wao, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nirekebishe, sikusema mkao wa kula, hapana. Nilisema mkao wa kuondokana na umaskini, hii ndio kauli ambayo niliitoa Barazani.

Mhe. Naibu Spika, *Job Center* walichelewa kupata usajili kwa sababu hawajakamilisha taratibu na leo asubuhi wakati nakuja huku, nilimuona ameingia pale na chombo chake nadhani amekuja kukamilisha. Natarajia wiki hii *Inshaallah* ikifika Ijumaa na yeye atakuwa amekamilisha taratibu. Nashangaa sana kwa sababu wao ndio walioanza, huyu mama wa Zamu alikuwa wa mwisho kuja, lakini yeye kakamilisha taratibu zile. Kwa hivyo, taratibu zimekamilika.

Ahadi yangu niliyoiweka hapa Mhe. Naibu Spika, naomba vile vyombo vya habari kama vipo wachukuwe hili gazeti walivute, kama wataweza kuliona na likaweza kuonekana kwenye TV. Hii ni ziara ambayo niliifanya hivi karibuni Oman, katika kutekeleza ile ahadi ambayo nimeiweka hapa Barazani na huyu ambaye nimekaa naye nazungumza naye ni Waziri wa *Main power* wa Oman, na tumefika mahali pazuri sana, kwamba sasa wamepeleka kwenye *cabinet* yao na SMZ tayari imeshapitisha na tayari tumepeleka huko na *Inshaallah* tukijaaliwa mambo yatakamilika hivi karibuni. Haya mambo yanakwenda kwa taratibu na wenzetu kila kitu kama tulivyo sisi ni lazima serikali ipitishe.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya hivyo, katika kuwasaidia vijana wetu hawa kwa kuwapatia mafunzo, kabla ya mwezi wa Septemba tunatarajia kuwapeleka vijana 20 Oman ambao wamepewa nafasi hizo za kwenda kusoma kwa ajili ya kujifunza namna ya kuweza kutengeneza ajira kwa wenzao. Sisi wenyewe hapa Zanzibar tumewatayarisha vijana 33 na tutawasambaza mikoani mheshimiwa, nao tayari tumeshawapatia mafunzo wamelipiwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO). Vijana hao watasambazwa katika kila wilaya kwenda kuandaa ajira, kufundisha ajira za ndani na hata za nje na Shirika la Kazi Duniani litawalipa posho maalum vijana hawa kwa muda karibu miezi sita na kuendelea. Kwa hivyo, ahadi yangu imetekelezwa na tunaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Qatar. Kwa bahati mkataba huu umesainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilipata nafasi safari hii nilipokuwa kwenye mkutano wa Geneva na nilikutana na waziri wa Qatar nikamwambia, pamoja na kwamba mkataba huu umesainiwa katika mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar ingependa isaini mkataba wake kwa mwamvuli wa Zanzibar na tumekubaliana kwamba hilo tutalifanyia kazi na tumo mbioni kulikamilisha, wala tusiwe na mashaka, mbio hizi zitafika mwisho wake tusiwe na wasi wasi, kwa sababu tumekuwa na tatizo mheshimiwa la mawasiliano kati yetu sisi na Qatar, hatuna ubalozi kule inabidi tutumie ubalozi wetu wa Abudhabi. Oman kwa sababu tuna ubalozi wetu kazi imekuwa ni rahisi, bado nawaahidi vijana.

Mhe. Naibu Spika, gazeti la tarehe 04/06/2012 kama tumesoma litaonesha wazi kwamba kufanya kazi nje ya nchi ni ruhusa, sasa hakuna kinachozuwia. Serikali hii ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Dk. Shein haiwezi kuwazuwia hata mara moja vijana kwenda kufanya kazi hapa ndani na huko nje *Inshaallah*.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake alivyojibu, amejibu sahihi na tumeyafahamu. Lakini napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba hivi karibuni kumejitokeza makundi

mengine ndani ya Zanzibar kuwatapeli watu wetu na kuwaambia kwamba wanaajiri wanataka kuwapa na kwa kuwa vijana wetu hawana ajira basi wakiambiwa hivyo wanashawishika.

Mhe. Naibu Spika, siku za nyuma ilijitokeza kampuni kama vile PENCO wakawaibia wananchi zaidi ya milioni 30 au milioni 300 za watu. Hivi sasa kuna makampuni mengine yanatapeli yanapita yakiwaambia watu kwamba kuna ajira na wanawaambia watu watoe shilingi 30,000/- au 70,000/- ili mtu apatiwe ajira.

Je, wizara yako inalifahamu suala hili na kama inalifahamu je, imejipanga vipi kupambana na watu hao matapeli wanaowaibia wananchi wetu fedha zao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, nia za mawakala hawa hazikuwa mbaya, tatizo lililojitokeza kutokuelewa utaratibu wa kuwatafuta vijana hawa na kukusanya fedha zile na ndio maana yake Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ikachukua hatua ya kuwazuwia mawakala wale wasifanye kazi zile wakati ule mpaka tuwape maelekezo sahihi, wafuate taratibu za nchi na hatimaye waendelee na shughuli zao, kwa sababu serikali haina nia ya kuwazuwia. Kwa sababu wakifanya hivyo wanaisaidia serikali kwa upande mwengine kuwapatia ajira vijana wetu na sisi tutaendelea kushirikiana nao.

Kwa hivyo, zile taratibu zilikiukwa kweli na kuna baadhi ya mambo tuliwazuwia. Kwa mfano, walikuwa wanachukua hata pesa za *passport* za wale vijana, yaani wanachukua dhamana ya kuwapatia *passport*, jambo hili ni zito. *Passport* ni jambo lako mwenyewe binafsi hawezi mtu mwengine kuchukua dhamana, kama anachukua dhamana ni kukudhamini tu endapo litatokea jambo jengine. Lakini haiwezi kampuni ikachukua dhamana ya huduma hii muhimu kwa vijana wetu au kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, taratibu zilikiukwa nakubali na ndio maana yake serikali ikazuwia. Sasa tumeshakubaliana kanuni nimeshazitunga na zimeshasambazwa kwa wahusika wote mawakala wanazo, namna gani ya kuweza kuwatafuta vijana hawa wakaomba ajira na hatimaye kuwapatia fursa hizo za ajira. Sisi tutafurahi sana kwamba vijana wetu wengi sasa watajitokeza kwenda kwenye kampuni hizi ili waweze kupata haki zao za kikatiba, kwa sababu ajira ni haki ya kila mtu kupata endapo atafuata taratibu za kisheria.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Toka mchakato huu uanze wa kuwatafuta vijana kwa ajili ya usajili wa kwenda kufanyakazi nje ya nchi.

(a) Je, ni vijana wangapi waliojitokeza.
(b) Ni vigezo gani ambavyo vinahitajika ili kijana awe anafaa kuingia katika kundi hili. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, suala la vijana wangapi wamekwenda kufanya kazi nje, namshauri Mhe. Mjumbe tumsaidie kwenda kuwauliza hao waliopewa majukumu sasa ya kuwapeleka vijana nje, kwa sababu hilo ni jukumu lao sio la serikali. Sisi kazi yetu ni kutoa vibali tu, kwamba unaweza kufanya kazi hiyo, sasa mawakala hao ndio wanafanyakazi hizo.

Lakini kama Mhe. Abdalla Juma atahitaji tumsaidie kumpatia takwimu kwa sababu yeye hawajui watu hao wako wapi, basi serikali itafanya hivyo.

Swali lake la pili ni kuhusu vigezo. Mhe. Naibu Spika, vigezo inategemea na mahitaji ya nchi Mhe. Naibu Spika, wako vijana ambao wanakwenda kufanyakazi pengine kwenye mashamba ya mitende, kwenye ma-*supermarket,* wengine kwenye mabenki na wengine wanafanyakazi za majumbani inategemeana, kila mahali na mahitaji, kiwango na sifa ambayo ile nchi au ile kampuni imeweka, ahsante.

Nam. 193

Ujenzi wa Mahoteli Kushamiri Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu nambari 193, nataka kufanya marekebisho kidogo tu kwenye kifungu (c). Naomba nikinukuu.

Kwa kuwa majengo yanayogeuzwa mahoteli yapo katika makaazi ya watu. Je, Serikali imekuwa ikichukua hatua gani kwa wamiliki wake, baada ya kushindwa kujengwa kwa muda mrefu sehemu hizo na kuzungushwa mabati bila ya kuonekana ujenzi wa aina yoyote kwa miaka.

Baada ya marekebisho hayo, sasa nijibiwe swali langu.

Mji Mkongwe wa Zanzibar hivi sasa unakabiliwa na wimbi kubwa kwa nyumba za makaazi kugeuzwa hoteli na kusababisha athari ya mila na utamaduni kuanza kutetereka.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Hoteli za Kitalii zinaanzishwa katika maeneo yaliyotajwa ili kuepusha migogoro na jamii na kulinda mila na utamaduni wa Zanzibar.

(b) Serikali imeahidi kupiga marufuku majengo ya Mji Mkongwe kugeuza Hoteli, kwa nini majengo hayo yanaendelea kugeuzwa hoteli za kitalii.

(c) Kwa kuwa majengo yanayogeuzwa hoteli yapo katika makaazi ya watu. Je, Serikali imekuwa ikichukua hatua gani kwa wamiliki wake kuhakikisha wageni wanaofikia katika hoteli hizo wanazingatia uvaaji wa nguo zinazolinda mila na utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 193 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kufuata maelekezo ya "*Master Plan*" ya Mji Mkongwe na ya UNESCO itahakikisha ongezeko la hoteli haliendelei katika maeneo ya makaazi ili kuepusha migogoro kwa jamii kwa lengo la kulinda mila na desturi za Mzanzibari.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuepusha athari za baadae za kugeuzwa Mji Mkongwe kuwa ni Mji wa Kibiashara badala ya kuwa ni mji wa kihistoria ambayo ndio inayotambulikana kiulimwengu. Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe imesimamisha na kupiga marufuku zoezi la ongezeko la mahoteli katika maeneo ya Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile urithi huu wa kimataifa unakuwa sio majengo tu ili ukamilike ni pamoja na mambo ya silka, desturi, utamaduni ambao Mamlaka ya Mji Mkongwe imeshirikiana na taasisi husika kwa kuwaelimisha jamii, kuhusiana na suala la mavazi na silka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, bado swali la (c) hajalijibu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, swali la (c) tayari nimeshalijibu, labda nilirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa amekiri kuwa atazuwia ujenzi kutokuendelea katika Mji Mkongwe na bado kuna nyumba na kuna dalili zinaonekana kuwa kuna hoteli na serikali imeanza utaratibu wa kuuza majumba yale hivyo kuna uhakika wa kujengwa mahoteli. Je, kauli hiyo anaihakikishia vipi Baraza kuwa hakutokuwa na ujenzi wa aina yoyote wa hoteli.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba serikali imeamua kuzuwia ujenzi wa mahoteli katika maeneo ya Mji Mkongwe, kwa hivyo hili suala bado linaendelea na huo ndio msimamo wa serikali kwa sasa hivi.
Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, swali limegusa jimbo ninaloliwakilisha hapa. Nilikuwa namuomba Mhe. Naibu Waziri anisaidie hili agizo lililotolewa la kusitisha ujenzi au ugeuzwaji wa majumba ya Mji Mkongwe kuwa mahoteli katika eneo hili, lilitoka lini kwa sababu hadi kipindi hiki ninachozungumza bado kuna majumba kadhaa ambayo yanaendelea kugeuzwa kuwa mahoteli katika Mji Mkongwe, nilikuwa naomba kujua kanuni hii imetoka lini na utekelezaji wake umeanza lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na tarehe iliyotolewa, ili upate uthibitisho wa uhakika basi nitakujibu kwa maandishi, lakini bado nazungumza kwamba msimamo wa serikali ni pale pale kwamba tumezuwia ujenzi wa mahoteli ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

Nam. 35

Umalizaji wa Madarasa ya Skuli ya Ng'ambwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Elimu sera yake ni kumalizia majengo (madarasa) yaliyojengwa kwa juhudi za wananchi pale wanapofikia hatua ya Linta na gabble. Na kwa kuwa aliekuwa Waziri wa Elimu wa Awamu iliyopita alipotembelea skuli ya ng'ambwa iliyoko Jimbo la Wawi katika mwaka 2008 aliahidi kuwa banda la madarasa manne ambalo lilishakamilika katika hatua zote za ujenzi watofali litaezekwa na Serikali kabla mwaka 2009.

Je, ni lini SMZ itatekeleza ahadi hiyo ambapo sasa ni mwaka wa nne tangu ilipotolewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 35 kama hivi ifuatavyo:-
Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa wizara yangu imekuwa ikiwahimiza wananchi katika maeneo mbali mbali kuanzisha miradi ya ujenzi wa madarasa mapya, ili kuwawezesha watoto wote kuweza kupata nafasi ya kuandikishwa katika skuli. Sera ya wizara ni kuwa wananchi kuanzisha ujenzi na kufikisha hadi hatua ya uezekaji na baada ya hapo wizara humalizia kazi zilizobakia.

Mhe. Naibu Spika, napenda kukiri kuwa Skuli ya Nga'mbwa ilioko katika Jimbo la Wawi, Wilaya ya Chake Chake ilianzisha ujenzi wa madarasa mapya manne na yameshafikia hatua ya kuezekwa. Pia, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliekuwa katika madaraka hayo Mwaka 2008 aliahidi kulikamilisha jengo hilo ambalo halijakamilishwa hadi hivi sasa. Kuchelewa kukamilishwa jengo hilo na majengo mengine ya skuli katika sehemu mbali mbali imetokana na uchache wa fedha.
Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inaahidi kulikamilisha jengo hilo katika mwaka wa fedha 2012/13 na mara tu bajeti hiyo itakaporuhusiwa kutumika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara ilikuwa na nia safi ya kuendeleza maskuli kwa kuwataka wananchi washiriki katika ujenzi, ili wao wamalizie kuezeka, lakini wamekwazwa na fedha za kuezeka. Je, wizara haioni kuwa umeshafikia wakati sasa wa kuzuwia ujenzi wa aina hii ili ikenda na uwezo wake.
Je, ni mwaka gani haya ambayo tayari yameshajengwa yatamaliza kuezekwa, ili wale walimu na wananchi kwa jumla wajuwe kwa uhakika hasa kwamba madarasa haya ikifika mwaka fulani yataezekwa badala ya kungoja kila mwaka ukasema bajeti hii haikuruhusu na bajeti hii haikuruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilizungumza mwanzo kwamba sera yetu ya elimu ya mwaka 2006 inazungumzia na inahamasisha wananchi kujenga. Sasa Mhe. Rashid Seif anaposema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumeshindwa, mimi sifikirii kama anatufanyia haki wizara yetu, hatujashindwa. Kwa sababu tunaezeka, tatizo ambalo hata wewe umelizungumza ni fedha, tutakwenda hatua baada ya hatua. Sio lazima majengo yote yanayojengwa leo tukikabidhiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tuyamalize leo kuezeka. Lakini ilimradi tunaezeka na wanafunzi wetu wanasoma. Kwa sababu tuna mahitaji makubwa Mhe. Naibu Spika, ya watoto wetu kupata nafasi ya kusoma, ili tufikie lengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupata elimu nzuri.

Mhe. Naibu Spika, mazingira ya elimu, wanafunzi kusoma kwa nafasi katika madarasa ambayo wanasoma ni moja wapo. Lakini Mhe. Naibu Spika, kueleza ni lini tutamaliza, siwezi kueleza hilo, kwa sababu kila siku wananchi wanajenga na sisi tunamaliza.

Kwa mfano, kwa mwaka huu Mhe. Naibu Spika tumeandaa mradi maalum katika Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa sababu kuna skuli katika Mkoa wa Mjini Magharibi na hususan Wilaya ya Magharibi, yaani kila mwaka wana mahitaji ya wanafunzi kupata madarasa na kila mwaka skuli hizo tunawamalizia. Kwa kweli mpaka hivi sasa ndani ya madarasa ni kama daladala, yaani kuna dereva na kondakta, kwa sababu lazima darasa liwe na walimu wawili, darasa moja lina wanafunzi 100 mpaka 120. *(Makofi)*

Sasa tukisema kwamba tuzuie au tuzungumzie wizara lini tutamaliza itakuwa si kweli, isipokuwa lugha tutakayoitoa hapa itakuwa ni ya kujidanganya au kulidanganya Baraza ama wananchi kwa jumla, na mimi nisingependa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tufikie katika hatua hiyo. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, leo kwa mujibu wa ratiba ya kikao chetu kwamba tunategemea tumalize mjadala huu jioni na hivi sasa tunao wachangiaji 16, yaani 10 *back benchers* na 6 mawaziri.

Sasa ninashauri kwamba wale wote ambao wanaotaka kuchangia wasitoke, na wakati nitakapoita jina hayupo sirudii, na michango tujaribu kuifuata yale yaliyokwisha kuchangiwa basi tusirejee, ili tuweze huu muda tulionao tuweze kuutumie kwa wachangiaji wote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataalla* aliyeniwezesha kunipa pumzi zake, na kuweza kupumua katika Baraza hili na hizi sio nguvu wala uwezo wangu isipokuwa hii ni neema yake *Allah Subhanahu Wataalla*.
Mhe. Naibu Spika, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambaye ni waziri mwenye *experience* kutoka Tanzania Bara hadi kufika Zanzibar. *(Makofi)*

Mchango wangu nitazungumzia sekta tatu ambazo ni muhimu kwa kila binadamu, yaani hana njia kuzunguka lazima akutane nazo. Sekta zenyewe ni afya, elimu na maji.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wengi wamechangia kuhusu suala la muungano na nawashukuru kwa hilo tena niwapongeze kwa dhati kabisa.

Vile vile napenda nimpongeze Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji kwa kazi aliyoifanya kuhusu *ICU* ingawa bado haijamalizika mpaka hivi sasa, lakini amepiga hatua. *(Makofi)*

Kwa kweli ni waziri ambaye anayeweza kupigiwa mfano, kwa sababu alitamka hapa Barazani kwamba atajiuzulu kabla ya miezi kama haijafanyiwa marekebisho *ICU*, yaani alizungumza vile kwa uchungu na wala sijapata kumsikia waziri mwengine yeyote kusema kwamba atajiuzulu kuacha madaraka ya uwaziri, na yeye alifanya vile kwa uchungu na jitihada zake kwa kweli tumeziona. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni waziri ambaye ni makini kabisa kwa muda mfupi tu kwa kipindi cha miaka miwili amefanya mambo makubwa katika hospitali ile. Kwa mfano, hospitali ile ilikuwa haina maji na amefanya jitihada za kupatikana kwa maji, suala la *ICU* pamoja na huduma ya mama wajawazito kujifungua na hayo ni mambo matatu mazito, hivyo Mhe. Waziri wa Afya hongera sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naungana na Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uteuzi wake wa mwanzo wizara hii ameiteua iwe Wizara ya Afya, na hata katika Bango Kitita ni wizara yake ya mwanzo kuiita Ikulu kutokana na umuhimu wa wizara hii, yaani kwa kuwajali wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Waziri bajeti uliyoipeleka humu Wizara ya Afya ni ndogo na wala haiwezi kukidhi, vyenginvo vyovyote tutawatupia lawama tu Wizara ya Afya.

Kwa mfano, hivi juzi tu Mhe. Waziri nadhani huna habari kulitokea mgomo kama ndugu zetu wa Tanzania Bara madaktari waligoma, sijui Waheshimiwa Wajumbe mnayo taarifa hiyo, wakidai posho zao za muda mrefu, kama vile zikiwemo posho za *call risk allowances* pamoja na posho za nyumba. Mhe. Naibu Spika, hivi kweli hospitali ile itafikia kuwa Hospitali ya Rufaa ikiwa madaktari wetu wale hatujawawezesha watafanya kazi kwa mtindo gani.

Vile vile nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa suala alililoliona hili la kuchukua jukumu kwamba dawa tutaagiza wenyewe, Mhe. Naibu Spika mwaka jana Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipiga kelele juu ya suala hili, kwa kutegemea mfadhili tu ataleta dawa, je yametokea maradhi ya Kipindupindu kwa kumtegemea mfadhili atatutibu nani? Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuliona hili.

Kutokana na hali hiyo, mimi naomba Mhe. Naibu Spika hawa jamaa tuwafikirie kwa kiasi fulani, kwa sababu kazi ni kubwa, matumizi yao ni makubwa tena wanatumika.

Vile vile kuna Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuhusu Maradhi ya Figo, na sijui kama hichi kitengo kitaanza kazi mwaka unaokuja au vipi na hili ni suala muhimu Mhe. Waziri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho nadhani na hilo atueleze tumefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Spika, kuna hospitali kama vile ya Makunduchi ambayo nafikiri mfadhili wake ni mzungu kwa asilimia 95. Sasa leo wananchi wa Makunduchi wanapata matatizo makubwa kwenye hospitali ile kutokana na umeme. Kwa kweli serikali sijui inachangia kiasi gani, kwa sababu leo sehemu ya kuhifadhia damu hakuna, umeme ni dhaifu kabisa, yaani ni hospitali inayojiendesha wenyewe kwa asilimia 95 mpaka 99 na wala haina msaada wa serikali.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Sekta ya Elimu. Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukifukuzia tu kujenga vyuo vikuu wakati msingi wa huku bila ya kwenda vyuo vikuu ni mtihani, kwa sababu huwezi kwenda chuo kikuu kama hujapata darasa huku, yaani wanafunzi wamekuwa wakisoma katika mavumbi, kukalia magogo ya minazi na kuandika chini, kwa kweli hapa bado hatujafikia.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine sijui kuna mikataba gani tunayosaini sisi serikali tunayosaini wakati mwengine kwa mfano kuna Skuli ya Mtule, mpaka leo mwaka wa tatu au wa nne hakuna kinachoendelea kule Paje, na imekaa kitako tu ni gharama kwa walinzi pamoja na nyengine.

Vile vile kuna Skuli au Chuo cha Ufundi Kengeja tulipiga kelele sana wanafunzi wanalala msikitini na bweni halitoshi, kweli mwanafunzi yule tutampeleka chuo kikuu kwenda kusoma katika mazingira gani.

Nikiondoka hapo sasa nizungumzie Kuhusu Sekta ya Maji na haya yote Mhe. Waziri yamo kwenye kitabu chake. Mhe. Naibu Spika, maji ni uhai wa mtu kwa mfano hapa tulipo maji yametuzunguka, lakini vitendea kazi hatuna Mhe. Waziri. Hivi leo kweli Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati haina gari hata moja ya maji haina karibu miaka 10 na hiyo si aibu.

Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume amejenga nyumba za Michenzani miaka kadhaa hata rangi hazijapigwa. Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufufua lile bwawa linawasaidia watu angalau kunawa uso. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, leo Mwakilishi anafika kuthubutu kwenda kukodi gari ya *crane*, yaani Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hivi gari ya *crane* kiasi gani na kweli tunawatumikia wananchi sisi na wala haiwezi kulaumika wizara. Kwa kweli maji yamekuwa na tatizo na leo kuna wananchi wanalipishwa maji wakati huduma yenyewe wala haipatikani, kukodi gari *crane* nje ni shilingi 180,000/= mpaka 200,000/=. Kwa mfano, kama mimi kwenye Jimbo la Muyuni ninavyo visima havipungui sita, yaani kwenda kufungua tu *pump*.

Mhe. Waziri nadhani kuna suala na wala sikulitegemea labda umelisahau au umepitikiwa kuhusu bandari. Mhe. Naibu Spika, suala la bandari ni jambo muhimu na katika pato letu baada ya kutegemea zao la karafuu, basi mimi naweza kusema pato kubwa tunalolipata ni kwenye bandari, lakini bado hatujawa tayari na hii ni aibu. *(Makofi)*

Hivi leo kuna meli ngapi ziko Chumbe ambazo zinasubiri kufunga gati pale, wakati bandari tokea miaka mingi mpaka hivi sasa bado hakuna kinachoendelea wala kilichojengwa na tunakosa mapato hivi. Kwa mfano, ndugu zetu wa Bara juzi tayari wameshafungua Bandari ya Bagamoyo, yaani watu wanaendelea na sisi tunarudi nyuma, tunakosa mapato mangapi.

Mhe. Naibu Spika, imefunga meli moja tu bandari imeshajaa, tusubiri sasa zitasubiri mpaka muda gani, kwa hivyo *usidharau dafu kwa embe ya msimu*. Kwa kweli karafuu msimu hadi msimu ndipo zizae, na wakati mwengine zinaweza kuzaa vizuri na wakati mwengine zikapungua kidogo, lakini bandari siku zote tunatumia na mapato yote yanatoka kwenye bandari.

Kwa mfano, leo vitendea kazi bandarini hakuna hivi kweli tunafanya kazi kweli sisi? Kontena ngapi zinazotolewa kwa siku? Mhe. Naibu Spika, vitendea kazi tokea Waheshimiwa Wawakilishi waliopita walipopiga kelele vikapatikana, na leo tunauliza vitendea kazi ni mbuzi na mwanawe, tumeona kwenye magazeti *crane* inabeba tani 75 kwenye Gazeti la Zanzibar Leo nakumbuka kitu kama hicho kimeandikwa.

Kwa kweli hali halisi hakuna *crane* yenye uwezo wa kubeba kitu kama hicho. Mhe. Naibu Spika, hakuna mtu mnyonge katika nchi hii kuliko mchukuzi, yaani mchukuzi kama hana afya basi hawezi kula, leo wachukuzi wetu wanapata shida na serikali inakosa mapato mengi sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, *crane* ile kwa muda wa saa moja ni shilingi 75,000/= inakodishwa pale. Mhe. Naibu Spika, hapa naomba ku-*declare interest* kidogo. *Crane* tokea mwaka 1974 au 1975 msaada kutoka Japan mpaka leo, na pale kuna mbavu tu hakuna *crane* tena na tumeambiwa zimeletwa juzi, lakini hatuzioni utendaji wake wa kazi na moja imewekwa Bwawani tu na nyengine ni ndogo ambayo tani 20 au 25 haiwezi kubeba ni mpya tena ni fedha za mkopo kutoka *PBZ*.

Mhe. Naibu Spika, shilingi 75,000/= kwa *crane* si fedha kidogo na tunakosa mapato Mhe. Waziri, kwa sababu kila tunapokukusanyia fedha sisi ndipo utakapoweza kutulipa uzuri humu ndani. Kwa hivyo *crane* shilingi 75,000/= imekuwa kama nyoka wa mdimu, yaani serikali haina uwezo ukaenda kuzichuma yeye anakurukia na wala hana kazi nazo. *(Makofi)*

Kwa mfano, kuna *crane* ambayo inataka kufanya kazi mule ndani kwa ajili ya kusaidia wananchi, pamoja na serikali hii na matokeo yake imezuiwa. Kwa hivyo, serikali inakosa fedha na wananchi wanazidi kuumia na wala serikali hii isingekuwepo bila ya kuwepo wananchi Mhe. Naibu Spika, kwa kweli shilingi 75,000/= kwa siku au masaa 6 tu, hivi kwa wiki, mwezi na hata kwa mwaka ni kiasi gani? Kwa kweli kuna mambo mengine imekuwa mzigo.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na Shirika la Meli na hivi leo liko wapi, limeanza kazi wakati huo hakuna mtu yeyote kwenye biashara hii na lilikuwa peke yake na wala hakuna kilichobakia, kuna Meli ya *GAPCO* imekopeshwa sijui kiasi gani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika kwamba meli ile ya mafuta amekopeshwa nani? Kwa muda gani? Kipato gani kinachopatikana? *(Makofi)*

Sasa leo wananchi wa Pemba anakwenda kuwaekea ada ya shilingi 1,000/= kulipia bandari kwa maisha ya Pemba shilingi 1,000/= Mhe. Waziri ni nyingi, ndio tunataka tupate mapato. *(Makofi)*

Lakini shilingi 1,000/= kwa wananchi wa Pemba *mashaallah* Mwenyezi Mungu amewajaalia Pemba kwa uzazi wanaongoza, yaani mtu mmoja anaweza kuwa na watoto 4 au 6 na Mwenyezi Mungu awazidishie. Lakini mtoto viatu vya kuvaa hana motto, na akikanyaga msumari basi *tetanus* na Hospitali yenyewe na Mnazimmoja ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, shilingi 1,000/= kwa wananchi wa Pemba ada hii ni kubwa, na kuna haja ya kulifikiria suala hili hasa kutokana na hali ya Pemba ilivyo ya kiuchumi. *(Makofi)*
Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu *ZRB*. Mhe. Naibu Spika, ninawapongeza *ZRB* kwa kazi zao wanazozifanya, lakini wafikirie marungu wanayotumia kwa wananchi wakati mwengine ni makubwa, kwa sababu kuku anataga yai moja na wala huwezi kumtagisha mayai mawili, na matokeo yake unaweza kuja kukosa kuku pamoja na mayai yenyewe.

Kwa kweli wafanyabiashara wameshaanza kuhama na kuelekea Tanzania Bara kwenye maendeleo. Mhe. Naibu Spika, nawaomba ndugu zangu wa *ZRB* kama wapo nawaambia *aste aste* kidole na macho, kwa sababu tunawahitaji wafanyabiashara kwa ajili ya kupata kodi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, nianze kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii ambayo ni safi kabisa pamoja na mipango yake aliyotupangia. Vile vile niwashukuru watendaji wake, hasa wa wizara hii kwenye Tume ya Mipango kwa mipango mizuri waliyotuwekea kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mipango mizuri imepangwa, kwa sababu watendaji hawa wanaonekana ni wazuri sana katika mipango hii tena wenye uelewa mzuri, kwa kweli wanastahili pongezi katika kupanga. Lakini nadhani niende kwenye utekelezaji nafikiri ndiko kwenye matatizo, na kwenye kupanga huku sidhani kama kuna tatizo kubwa sana, isipokuwa tatizo linakuja kwenye utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, nianze na ule mpango wa mwaka jana wa serikali, namna serikali ilivyokuwa na azma njema kabisa ya kuwasaidia wananchi, ili wajiwezeshe katika Sekta ya Kilimo. Kwa mfano, mwaka jana ukiangalia serikali ilipunguza bei za pembejeo za kilimo kama vile mbegu, mbolea, dawa za kulimia na zile za kupalilia mashamba, yaani tunaziita dawa za gugu pamoja na zile bei za trekta zilipunguzwa kwa asilimia kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kama vile mbolea shilingi 200/= tu, dawa ya magugu ikawa ni shilingi 6,000/=. Lakini ukiangalia utekelezaji wa mpango ule haukwenda kama ulivyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, karibu asilimia 95 ya watu wa Jimboni kwangu ni wakulima tena wa mpunga, lakini utakuta zoezi hili utakuta hawakunufaika nalo. Kwa mfano, dawa ile ambayo inayouzwa shilingi 6,000/= sijui kama kuna asilimia mbili ya wakulima wangu waliipata kwa bei ile, na matokeo yake inauzwa kwa shilingi 20,000/=.

Sasa ile azma ya serikali ya kupunguza bei ile huwa hatuipati kutokana na kutokuwa na mipango mizuri ya ule utekelezaji wa ile mipango iliyopangwa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ule mpango uliopangwa, utauona ni mzuri kabisa na suala linakuja kwenye utekelezaji.

Kutokana na hali hii, ndipo pale niliposema kwamba mipango au wapangaji kwa kweli wanastahili pongezi, kwa sababu wanapanga kwa kuangalia mbele kabisa na kuona kile ambacho wanachokipanga namna ambavyo vitaweza kuwanufaisha wale wananchi, lakini suala zima linakuja kwenye utekelezaji na hapo ndipo panapokuwa na mashaka.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia suala la utekelezaji ambalo mimi naliona ni kikwazo kabisa. Sasa sijui serikali inatuambia nini kwenye hili, kwa sababu tunapanga lakini utekelezaji unaonekana unakuwa mzito, au tunaweza kusema kwamba serikali haisimamii vizuri kwenye utekelezaji.

Kwa maana hiyo, tutaendelea kila siku kuongeza vyanzo vya kutafuta mapato na tutayatafuta, yaani watatuonesha wale wapangaji kwamba hapa na pale tunaweza kukusanya. Lakini kama itakuwa tunaendelea kukusanya na huko utumiaji ukawa wa ovyo, basi kazi yetu itakuwa ni bure, isipokuwa tutaendelea kuwatwisha mzigo mkubwa wananchi wa kodi, na matokeo yake wananchi hawa hawafaidiki na zile kodi ambazo wanazilipia.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua kwamba Baraza lako liliunda Kamati Teule hapa kwa ajili ya kwenda kufanya uchunguzi, na ilipewa hadidu rejea ikafanyia kazi na ikaja kutoa ripoti yake kwa Baraza hapa. Kwa hivyo, Baraza liliichukua ripoti ile na kutoa mapendekezo yake na kuitaka serikali iyafanyie kazi. Sasa mpaka tunakuja hapa kwenye bajeti hii sijui kama serikali imeshayafanyia kazi mapendekezo yale au laa.

Lakini leo tunakuja kuombwa fedha nyengine hizi za matumizi, wakati kwenye Ripoti ile ya Kamati Teule tumeona namna ya ubadhirifu wa fedha, mali za serikali zilivyofanywa. Lakini leo wanakuja na tukabidhi tena fedha pengine kwa baadhi ya watendaji, ambao wameonekana kutomudu zile kazi zao au kuvuruga ule mpangilio mzima wa serikali na wala hakuna hatua iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeona ni vyema kwanza serikali ikatueleza juu ya yale ambayo tuliyazungumza kwenye ripoti ile, ili wananchi wakaweza kujua kama kuna mambo yaliharibika, na hivi sasa tayari yameshawekwa sawa. Lakini kama hivi itakuwa tunakwenda kama mchezo wa bao, na hapa itakuwa tumepigwa *kitakomu*, yaani ukiingia tu pale hamna kitu.

Kwa hivyo itakuwa kazi yetu tunatoa na tunapeleka misumari kwa wananchi na kuwatoboa, ili waweze kuendelea kulipa kodi na wala kodi ile haiwanufaishi. Kwa kweli Mhe. Waziri hapa ameomba tena kuongezewa hapa, yaani anataka kutoa kodi nyengine hapa na kuna kodi nyingi ameziomba humu na anaomba turidhie, ili aweze kukusanya vizuri kwa ajili ya kutoa huduma.

Mhe. Naibu Spika, malengo ni mazuri na mipango sikatai kwani ni mizuri, isipokuwa utekelezaji hivi tutaamini vipi hichi ambacho anachokiomba Mhe. Waziri kitakusanywa na kitatekelezwa katika yale ambayo uliyoyaombea. Sasa mimi hapa napata shaka kidogo na ndio maana nakuwa mgumu kidogo kukubaliana moja kwa moja kusema naunga mkono kwa asilimia mia moja, bajeti nasema si mbaya, lakini utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje atueleze kwanza kwa yale ambayo sisi tuliyaona, na tulitoa mapendekezo kwa serikali, basi tuambiwe kwanza yamefanyiwa kazi vipi? Kwa sababu serikali ni ya wananchi, na wao ndio walioona haya. Mhe. Naibu Spika, nadhani ukiangalia Katiba ya Zanzibar kwenye kifungu cha 9 kinaeleza wazi naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 9 (2) (a) kinaeleza hivi:-

> "Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe".

Sasa kama wananchi wameona, maana wananchi ndio hili Baraza hapa wameona kuna moja, mbili, tatu, hivi kuna ugumu gani serikali kufanyia kazi yale mawazo waliyotoa wananchi, kwa sababu hii serikali ni yao. Mhe. Naibu Spika, kama serikali ni yao, na wameona kuna mambo hayendi sawa, wajibu wao ni kusema na ndio maana tulitumia vikao vya Baraza kwa kusema kwamba kuna moja, mbili, tatu, lakini serikali imekaa kimya na kusema tunafanyia kazi.

Kwa hivyo, leo unatuletea na kuomba tena kututoboa, maana kodi ni mwananchi, yaani ukiisema kodi unamgusa mwananchi moja kwa moja, kwa sababu yeye ndiye mwenye kutozwa kodi. Mhe. Naibu Spika, ukiwa unataka kumtoza kodi mpya mbali ya zile nyengine, na hizi za nyuma tumetoa hapa na wananchi wamechangia ndio maana mukazipata zile fedha, kwani ameonesha kuna fedha ambazo zinatokana na mapato, ambayo zinatokana na kodi kwa wananchi.

Kwa hivyo, kama hukutueleza umetueleza namna ambavyo sisi tumeona matumizi yale hayakwenda sahihi na majibu yake hutupi na unaomba nyengine, sisi tukufanye nini Mhe. Waziri? Hivi tukuridhie tu bure na wala haiwezekani. Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kuona kwamba unaendelea kututoboa tena mifuko yetu kwa ajili ya kwenda kuwakabidhi tena watu ambao tayari tumeshawaona kwamba wana matatizo.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwanza ni vyema kwa serikali ikatupa majibu juu ya ile Ripoti ya Kamati Teule. Kwa kweli pale zimetumika fedha nyingi za wananchi, yaani tumekaa kamati ile, imepita na kuzungumza na kuhangaika na hatimae kutoa ripoti ile.

Sasa kama itakuwa kazi yake kamati zinaundwa na kutoa ripoti utekelezaji ule hauridi tena huku, sifikiri kama kutakuwa na uhalali au uzito wa kuweza kutoa fedha nyengine kabla ya kujua zile ambazo zilizoharibiwa kumechukuliwa hatua gani kwa wale ambao waliyoyafanya yale.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu utekelezaji wa hatua za kuimarisha mapato kwenye ukurasa wa 19. Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya Mhe. Waziri ametuonesha hapa namna ambavyo anasema anataka kuimarisha, ili kuweza kupata makusanyo mengi zaidi.

Nadhani nikubaliane na mpango wa Mhe. Waziri, lakini naona bado kama uko legelege katika mpango wa kukusanya mapato au kuimarisha vile vyanzo ambavyo tunavyo, basi ni vyema kwanza avikamate sawa sawa, ili viweze kutoa yale mapato yanayostahiki. Mhe. Naibu Spika, serikali naiona bado haijawa tayari katika kukusanya kodi, kwa kweli mianya ya kodi ipo mingi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika kwenye mkakati wake huu, ni vyema serikali ijikite hasa katika kukusanya kodi na wala sio kuangalia kutoa aina mpya ya kodi, isipokuwa mimi nataka iangalie hapa zaidi na kuliko kwenda kutoa kule kwenye zile za aina ya kodi mpya ambazo umeziweka, tena nyengine naona hakuna haja ya kuwepo.

Lakini hapa kwenye huu mkakati wake anaouonesha hebu tujikite hasa kama tulivyofanya kwenye zoezi la karafuu. Mhe. Naibu Spika, tulifanya zoezi la karafuu hapa na *Alhamdulillah* mara hii mambo yamekuwa mazuri kidogo. *(Makofi)*

Sasa nadhani serikali ioneshe nia thabiti hasa katika kukusanya kodi, yaani tuwawezeshe wale wakusanyaji kwanza, maana yake wakusanyaji tunao wenye elimu pamoja na utaalamu kabisa kuhusiana na mambo haya. Lakini inaonekana bado kuna udhaifu katika utekelezaji wa watendaji wale na mimi namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja hapa hebu tueleze hasa ule mkakati uliouweka mbali na huo ambao unauonesha maana naona ni mdogo sana. Ujuzi wanao hawa, wengi pale ukiwatizama ni wataalamu katika hili.

Mimi nasema bado serikali yenyewe ndiyo ambayo inaachia katika suala hili. Hebu ioneshe ule mkakati hasa madhubuti inaouwandaa katika kuhakikisha kwamba hizi kodi tunazikusanya. Kuna kodi hapa tunaambiwa bado hatujazikusanya vile inavyotakiwa katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Waziri Sekta ya Utalii bado inaonekana haijatuletea ile tijara tunayoitaka ndio maana mimi nikawa nasema hebu tuweke mkakati kama ule tuliouweka kwenye zoezi la karafuu. Tuweke hasa nguvu zetu katika kukusanya kodi kwenye Sekta ya Utalii, halafu tutizame hatutopata manufaa. Lakini tukienda katika njia kama hizi tutaendelea kupiga kelele kila siku, Sekta ile ya Utalii wanakuja tu hawa wenzetu hawa kutoka nje wanakusanya fedha zetu hapa wanaondoka nazo. Sisi kwenye kukusanya kodi tumekuwa kidogo tunaacha.

Mhe. Waziri kuna maeneo mengi bado ukusanyaji wake haujawa madhubuti. Kwenye Sekta ya utalii kuna ukodishwaji pale wa ardhi vile vile ambao wanaokuja kuwekeza katika sekta ile wanakodi ardhi. Utasikia kwanza ana *tax holiday* ikimaliza anasema sijamaliza ujenzi, anafanyiwa *renewal* akimaliza, anasema tena sijamaliza anafanyiwa tena *renewal*. Hatuwezi kukusanya katika njia hiyo. Misamaha imekuwa mingi mno na misamaha ile angalau ingekuwa wanapewa wawekezaji wazalendo zaidi kuliko wale wageni. Madamu katoka huko anakuja kuwekeza kwetu anao uwezo huyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa tuacheni hii habari ya misamaha misamaha mingi ya namna hii. Tunasamehe mno, tupunguze kwenye kusamehe huko. Kama mtu ukishakumpa msamaha mwaka mmoja au miaka miwili, hajatakeleza yale hakuna haja ya kumfanyia renewal ya msamaha tena huyo, alipe kodi, anaweza alipe, hawezi atuachie. Zamani tulikuwa tunasema tanauita uwekezaji kwanza maana yake hii miundombinu yetu si mizuri, barabara sio nzuri, maji hayajafika uzuri, umeme hakuna. Lakini sasa hivi *Alhamdulillah* kila pahala barabara zipo, maji yanafika, umeme umefika, sasa hizi *tax holiday* za nini tena.

Mhe. Waziri mimi nafikiri tuangalie eneo hili, tuliangalie vizuri sana kwa upana kabisa tutaweza kukusanya vizuri. Halafu kuna ukwepaji mwengine wa kodi pale katika sekta ya utalii. Hii habari ya watu kulipia huko kwa huko wakaja tu huku wameshamaliziwa kila kitu, ina maana hapa ndio hakiingii kitu. Mimi nafikiria hebu tuwe makini sana katika eneo hili. Mhe. Waziri kama tutakazana vizuri hapa basi tutafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuna kodi hapa inaonekana haikukusanywa ile ya wafanyakazi wa Jamuhuri ya Muungano *PAYEE* ambao wanafanyia kazi Zanzibar na mwenyewe Mhe. Waziri katika kitabu chake kakiri kabisa kodi ile hakuikusanya. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja tupe ufafanuzi hasa kwa nini kodi ile umeshindwa kuikusanya. Umeeleza kidogo hapa lakini maelezo yao hayajajitosheleza, miye sijaridhika na maelezo haya. Nataka maelezo ya kina kabisa ili niweze kujua, unaweza kuikusanya au tutakuja kukuta na bajeti ijayo ya mwakani unatuletea hadithi hii kwamba umeshindwa kuikusanya manaake marekebisho ya sheria hayajakaa sawa. Sijui sheria zipi katika kukusanya kodi.

Sheria tunazitunga hapa utekelezaji wake wake ndio matatizo. Mhe. Waziri ndio pale niliposema utekelezaji mimi naona bado serikali haijawa *serious* katika utekelezaji. Tunatunga sheria, tunafanya mambo mengi sana, lakini kwenye kutekeleza usimamizi ule wa utekelezaji ndio mbovu. Hilo tukubaliane uje, utwambie sasa mnajipanga vipi ili tukuridhie katika haya. Lakini hili halijatosha kunakuja bajeti hapa za Wizara nazo tunataka tuziangalie zituambie utekelezaji wa huko tunapotoka. Leo wanapokuja kutaka tena.

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee mbele kidogo hapa kwenye ukurasa wa 37, Mhe. Waziri hapa amezungumzia kwenye mambo ya maeneo ya kipaumbele ya huduma za afya. Mimi niipongeze serikali kwenye hili, niipongeze kwa kuweka kipaumbele kwenye huduma ya afya. Kwa kweli hili lilikuwa ni tatizo kubwa sana linalowakumba wananchi wetu kwenye suala la uzazi. Suala hili kwa kweli lilikuwa ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kule katika jimbo langu ninayo hospitali ya Kivunge, nalijua hili tatizo. Mama zetu hawa masikini, wazee kule mimi masikini sana, uwezo wa kununua hata ile *gloves* hawana. Hapa naona serikali imejitolea kabisa katika hilo, naipa hongera sana. Lakini yasiwe haya yanaishia katika kitabu yafike kwenye utekelezaji. Maana mtu anapofika pahala kujifungua maradhi yale si kama homa kwamba utanunua dawa, ikishafika mahala mtoto anataka kutoka ni lazima atoke tu, huna njia ya kumzuia.

Sasa nataka kuiambia serikali kwamba iwe makini katika hili. Msiwaambie akina mama hawa ikawa wanakwenda kule wanakumbana na hayo hayo kwamba dawa anunue, *gloves*, sijui kitu gani anunue tutarudi kule kule. Mmesha wahakikishia kwamba kuanzia tarehe 1, Julai kila kitu kinapatikana, anakwenda zake anajifungua salama, usalimini, *Alhamdulillah*. Tunashukuru sana na tuhakikishe kwamba hichi kinafanyika. Isije ikawa mtu anafika kule akaambiwa ‘aah Waziri tu huyo alisoma huko, sisi huku hatujaletewa kitu. Ujipange leo Mhe. Waziri wa Fedha hizi fedha unazotuambia na vifaa viwe vipo pale mahospitalini. Isifike pale tarehe hiyo wanakwenda akina mama kujifungua anaanza kuletewa yale yale ambayo yeye ameshayasahau.

Najua serikali yetu ni sikivu na hili italisikia na itafikisha kwa wakati. Naomba sana sana. Hili suala si mchezo, jamani mambo mengine unaweza kustahamili dawa inaweza kwenda kununuliwa ukastahamili lakini kwenye

kujifungua hakuna huko lazima mtoto akishakufika mda wake atatoka. Hukumkaribisha chumbani atazaa nje na ndio maana utakuta akina mama wengine wanajifungulia nje. Unakuta daktari ana mzuia haingii hana pesa, huna hichi, hana uvumilivu anajifungulia nje. Jamani naiomba sana serikali katika hili, ihakikishe kwamba hivi vifaa vya mama mjamzito viwe vinafika kwa wakati na kusiwe kwamba aaah bajeti ya mwaka huu imeshakwisha maana tumepangiwa wajifungue watu 7 mmekuja 14. Mhe. Waziri sisi tunazaa sana utujue hivyo.

Mhe. Naibu Spika, niguse kwenye ukurasa wa 45, miradi mikuu uliyoiyonesha kuna suala ambalo ulilolizungumzia la uhaba wa Afisi za Serikali au uchakavu wa ofisi zilizopo. Mhe. Waziri hapa inaonekana unataka tukupe njia ya moja kwa moja sasa utuuzie nyumba zetu zile kongwe. Suala hili mimi Mhe. Naibu Spika, kwanza sikubaliani nalo. Naweza kukubaliana nalo kama tutalibadilisha utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa kuna uuzwaji holela wa majengo ya serikali. Katika hili Mhe. Waziri mimi naomba hili uliweke kando kabisa kuuza *asset* za serikali hizi. Ningeomba kwenye majengo ya serikali ya namna hii ni vyema unapotaka kufikia hatua hizo basi kabla ya kutiliana saini hiyo mikataba huko, uilete katika Baraza japo kwa Kamati ya Baraza kama ni ya PAC au ya Ujenzi au ya Biashara, wapitie na wao angalau waone ile mikataba kwanza ambayo unataka kufanya, kama ni kuuza kama ni kubadilisha kama kufanya nini. Kukuachieni tu moja kwa moja watendaji inaonekana katika zoezi hili hawakufaulu vizuri, limekuwa baya kidogo.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana katika zoezi hili Mhe. Waziri aliweke kando hapa tusiliridhie, maana anaomba kibali cha kufanya hivyo. Mimi ningeomba kwenye zoezi hili kabisa kabisa lisifanywe na watendaji peke yao kule. Serikali ikishakuwa inafanya hilo bora ilete katika Kamati husika nayo ipate angalau baraka wa wajumbe wa kamati ile ili liweze kufanikiwa.
Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii. Kwanza sina budi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya tukaweza kuamka salama na tukaweza kufika katika ukumbi huu tukiwa tumo katika hali ya afya njema.

Pia napenda nichukue fursa hii kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote waliokaa kwa muda mwingi kwa kuitengeza bajeti hii ya serikali na hatimaye wakaileta katika Baraza hili ili tuipokee, tujadili na hatimaye tuipitishe. Tuko hatua ya kuijadili na Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaipitisha.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nianze katika hii hali ya ukuaji wa uchumi. Kwa kweli bajeti imechangiwa sana na wataalamu. Na sisi tuliokuwa sio wataalamu tuna haki ya kupitia pitia ili tukaonekane ule udhaifu wetu ili Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha aweza kutuweka sawa. Katika ukuaji wa uchumi mimi sitaki niende ukuaji wa uchumi wa nje au wawapi. Mhe. Waziri anasema uchumi umekuwa, ni kweli kama uchumi umekuwa. Lakini uchumi umekuwa katika serikali yetu, imejionesha dhahiri kwamba mapato yanayokusanywa wizara nyingi zimevuka lengo lakini na serikali pia imeweza kugawa keki yao waliogawana katika kipindi cha mwaka jana pia na wao wamevuka lengo. Baadhi ya wizara nyingi katika kota ya pili ya tatu wengine keki ile wameshaimaliza. Ni kuonesha kuwa katika serikali uchumi unaonesha kuwa umekuwa.

Je, uchumi huu unaokuwa katika serikali unamnufaisha vipi Mzanzibari au mtu mmoja mmoja katika kukidhi mahitaji yake, naona hili linanitia utata na mimi kidogo. Nitamuomba Mhe. Waziri akija pengine kuna wataalamu wanaojua zaidi uchumi unavyokuwa watufahamishe na sisi.

Mhe. Naibu Spika, uchumi tunapoutaka ukuwe kwa mwananchi mmoja mmoja ni ule uchumi wa uzalishaji hasa ndio tunaokidhi kwa kuutaka umfikie mwananchi mmoja mmoja ili na yeye afaidike kiasi fulani. Mhe. Waziri Zanzibar tumezunguukwa na mahoteli mengi ya kitalii ambayo kuwa ni miongoni mwa kukuza huo uchumi. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, mahitaji ya mahoteli hayo ni mengi sana. Je, soko letu la ndani hapa Zanzibar tunaliweza kulikidhi haja kupitia huu uzalishaji. Kwa sababu tukipita masokoni kila kitu sasa hivi kinatoka Bara, ukenda tungule inatoka Bara, keroti zinatoka Bara, kitunguu kinatoka Bara, sasa sisi Zanzibar hatuna uwezo hata wa vitu hivi vidogo vidogo kuzalisha.

Mhe. Waziri kama kuna maeneo ambayo kuwa yanazalisha mambo kama haya tutakuwa tunakidhi hili soko letu la ndani hapa Zanzibar basi itakuwa na sisi hata hawa wananchi wetu tutasema wanakuwa katika kiuchumi. Lakini kama hakuna hayo basi Mhe. Waziri tunakuomba pamoja na serikali kuwashajihisha wananchi wetu ili kupitia njia hii ya uzalishaji basi na wao waweze kukidhi mahitaji yao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka niende katika hivi vipaumbele. Mwaka 2011/2012 kuna vipaumbele karibuni vitano ambavyo kuwa serikali walisema watavipa vipaumbele. Tunapozungumza kipaumbele ni kuwa kipaumbele kile kifikiwe lile lengo lililokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta ya kilimo baada ya Mhe. Rais kutangaza Mapinduzi ya Kilimo wananchi wetu walishajihika sana na wakaelekeza nguvu zao katika kilimo. Sekta hiyo ya kilimo kuna changamoto ambazo kuwa zimejitokeza. Chagamoto ya kwanza ambayo imejitokeza wananchi walilimiwa kinyume na wakati wanaotarajia katika kilimo kile cha mpunga. Changamoto ya pili ni changamoto ya pembejeo za mbolea. Nadhani serikali ilipotoa kipaumbele hiki haikujipanga katika hili. Tunapozungumza kuwa hii changamoto ya kilimo tunaigusia sana kwa sababu tayari watu waliitikia ule wito. Baada ya kuitikia ule wito serikali ilishindwa kutekeleza majukumu yake. Hatusemi kwamba kwa sababu mwaka huu haikutoa kipaumbele ni kuwa haitashushulikiwa, itashughulikiwa lakini hizi changamoto zinazojitokeza lazima tuzizungumze ili serikali ijue. Itakapojua ndio mwaka huu watakapojipanga. Vipi watawalimia wananchi wake, ni vipi wataleta mbolea ili iweze kutosheleza, hatimaye ukawekwa ugomvi katika mabonde.

Mhe. Naibu Spika, huko nyuma watu walikuwa wakilima lakini walikuwa wakilima wakitumia nguvu zao sana katika kilimo. Lakini badala ya serikali kutangaza kupunguza pembejeo na mambo mengine wanachi waliitikia huu wito. Wananchi walilima sana kwa wingi na kwa matumaini ya kuwa watapata kipato. Hatimaye serikali wao kumbe walikuwa wanaangalia tu yepi yatatokea. Tunaiomba serikali kama wanataka kweli Mapinduzi ya Kilimo basi wajipange, vipi watawalimia wananchi wao ndio watakavyojua. Vipi pembejeo za mbolea watazitoa, wao watakaojua, lakini wasiseme kitu kipaumbele hatimaye ikaleta ugomvi kwa wananchi.

Hata hivyo ukenda kwa watu wa Wizara wao bado wanasema kuwa matatizo ya kuwa mbolea zimekuwa kidogo, mbole zikimwagwa nyingi ndani ya ardhi tutakunywa wapi maji. Kwani hapo mwanzo waliposema hawakufikiria hilo. Kuwa wanapowahamasiha watu na watu watahamasika. Kama mliona mbolea ni tatizo katika ardhi kwa sababu tunatumia maji yale basi wangelitafuta mbolea mbadala ili wananchi wakaweza kukidhi ile haja ya kilimo. Tunaiomba serikali kupitia hili wajipange.

Mhe. Naibu Spika, niende katika vianzio vya kodi. Je, niulize katika vianzio hivi vya kodi vinavyowekwa sijui bandarini, sijui wapi, serikali imeshajipanga na udhibiti wa mfumko wa bei. Kwa sababu tatizo moja ambalo kuwa linaleta mfumko wa bei ni hivi kupandishwa vitu kiholela. Serikali tayari wao wameshaona maeneo ya kutafuta hivi vianzio vya mapato, lakini hii Sh. 1,000/ unayoitaka wewe basi na mwananchi yule vile vile itafika pahali inakuja kwake na kama kodi imeshapanda katika leseni, petrol, dizel, na hii na dereva na yeye ataitafuta hii shilingi yake moja anayoitia humu. Sasa akiitafuta na yeye yule abiria atakaepanda mule ataitoa yeye, hakuna mwengine atakaeitoa.

Mhe. Waziri hebu tuambie katika huu upandishaji wa hizi kodi mshajipanga vipi. Kwa sababu gari hiyo hiyo itakayotozwa shilingi 50 kwenye dizel, gari hiyo hiyo ndiyo inayokwenda kuchukua kipolo cha mchele Chakechake wakati alikuwa akichukua kwa shilingi 200 basi sasa na yeye ataitafuta ile shilingi 100 ataongeza. Akiongeza na yule mwenye kipolo cha mchele na yeye atatafuta ile pesa yake. Itakuwa hii pesa inazunguuka hatimaye ukenda dukani ukiambiwa imeongezwa shilingi 50 unajiuliza inatokea wapi? Kumbe ni ule mzunguuko wa ile pesa inayozunguuka halafu tunasema vyakula vimepanda bei, kumbe ni hii mizunguuko. Ukiuuliza unaambiwa sijui kuna majanga kumbe ni haya haya mambo tuliyokuwa tunayo katika maeneo yetu. Serikali na wao waliangalie kwa umakini sana. Wasipandishe mambo halafu hilo hilo linamzunguukia yule yule mwananchi.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kuondosha hili tozo la akina mama wanaokwenda kujifungua, nashukuru. Lakini mimi nina wasi wasi mkubwa kuwa tozo hili linaloondoshwa, hili hili litajirudia katika mzunguuko huu huu. Itafika hatima yule yule ndiye atakayelilipa hili. Mhe. Rais keshatwambia tutakwenda pale tujifungue Mwenyezi Mungu akitujaalia. Yule mwanamke sasa anataka kurudi nyumbani huku dereva ushampandishia kwenye petrol. Sasa hii hii shilingi itazunguuka hatimaye inamjia yule yule mwanamke ataichangia, akitaka, asitake.

Mwanamke huyo huyo ataingia ndani ya boti anataka kuja Unguja, huyu ndiye atakayeitoa pale. Sasa itakuwa kumbe huku tunapunguziwa lakini huku tunaongezewa. Hivyo ndivyo pesa inavyozunguuka, unaondoshewa hapa unakuja kupigiwa huku. Mhe. Waziri *Wallah* mipango ni mizuri sana, tunakupongeza kwa juhudi zako unazozifanya kwa kutafuta pesa. Lakini pia tunakuomba na wananchi wao waliokuwa chini uwafikirie, uwaangalie na wao. Mkishapandisha haya mambo madogo madogo na udhibiti wa mfumko wa bei uonekane serikali iwe na udhibiti huu, isiwaachie tu watu, muwaonee huruma.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, nasema kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Wilaya ya Micheweni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Kabla sijaendelea kuwaita waheshimiwa kuchangia naomba kutoa taarifa kwamba leo tumepata wageni wapo juu hapo ni Maofisa wa Kijeshi 67 kutoka Uganda, wakifuatana na wenyeji wao Maofisa vile vile kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania Zanzibar. Hivyo naomba niwatambulishe na nyinyi muwatambue.
Ugeni kutoka Uganda unaongozwa na Makamanda wafuatao:-

(1) Generali Apollo Kasita Gowa

(2) Kanal Oluku

(3) Kanal Kamanyire

Wenyeji wao wanaongozwa na:-

(4) Kanal Tongora

(5) Kanal Alphonce

Karibuni sana katika Baraza letu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, sauti yangu leo haiko safi lakini nitajitahidi kwa uwezo wangu nizungumze machache sana.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kukutana hapa katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee, kuhusu mpango wa maendeleo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2012/2013.

Lakini kabla ya kuanza shughuli hiyo nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohammed Shein kuweza kusimamia vizuri shughuli za serikali. Lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza rafiki yangu sahibu wangu Dr. Omar Yussuf Mzee kwa hotuba yake hii nzuri iliyopangika na haina mashaka. Nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, kwa sababu bila ya kuwa na mipango hii hotuba hii isingeweza kupangika vizuri, bila ya kuwasahau Wakurugenzi, Kamishna wa Tume ya Bajeti pamoja na wote waliosaidia kwa namna moja na nyengine katika kufanikisha suala hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na kwa nini nikasema ninaiunga mkono. Mhe. Naibu Spika, hotuba ya bajeti hii imeelezea mambo mengi na ya msingi. Kwanza imetuelezea namna ya utekelezaji wa bajeti iliyopita kwa hivyo tumeona namna ya utekelezaji wa bejeti iliyopita kupitia katika wizara mbali mbali. Lakini pia bajeti imetuelezea namna ya mapato yalivyokusanywa katika kipindi kilichopita. Kwa hivyo tumepata picha lakini pia wametueleza namna walivyotumia mapato yale.

Jengine Mhe. Naibu Spika, wametuelezea jinsi watakapokusanya katika bajeti hii na mipango yao ya maendeleo katika kipindi hiki tulichokuwa nacho. Kwa hivyo kwa kweli Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imetuonesha picha halisi ya bajeti iliyopita na mipango ya maendeleo na makadirio ya matumizi katika kipindi hiki. Lakini pia imetueleza vipaumbele katika bajeti iliyopita lakini na vipaumbele vya mwaka huu. Kwa hivyo kwa wastani bajeti hii imekamilika na imetoa picha au sura halisi ya utendaji katika serikali na utekelezaji wa serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri pia amepata nafasi ya kutuelezea hali ya uchumi katika nchi, ambalo ni jambo muhimu ambapo ametueleza kwamba pato halisi la taifa limekuwa kwa asilimia 6.5 na kufikia Tanzania shilingi bilioni 1.198 kwa mwaka 2011 kutoka Tanzania shilingi milioni 946.8 kwa mwaka 2010 ambapo ametwambia kasi ya ukuaji huu haijapatapo kutokea kwa kipindi chote cha miaka mitano. Kwa hivyo hizi ni taarifa njema na zinastahiki kupongezwa na wachumi wetu wameweza kufanya juhudi kubwa katika kukuza uchumi. Pamoja na kwamba waheshimiwa wajumbe wamekuwa na wasiwasi juu ya ukuaji huu ambapo ni dhahiri ukuaji huu haunekani moja kwa moja kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, tuliwahi kupata maelezo juu ya ukuaji huu wa uchumi ambapo wachumi walipata nafasi ya kutueleza kwamba uchumi wa aina au ukuaji wa aina hii impact yake haiwezi kuonekana moja kwa moja ni uchumi ule unaokua kwa zaidi ya asilimia kumi ndio unaoweza kuonekana moja kwa moja kwa wananchi. Kwa

hivyo tunaelewa uchumi umekuwa lakini kwa kuwa kufikia kiwango kile kinaweza kuleta impact kwa watu basi ni dhahiri tunafahamu kwamba uchumi unakuwa na juhudi zaidi zinahitajika ili tufikie katika hivyo kiwango ambacho kinatakiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametueleza sababu za kukua kwa uchumi na ametuelezea mambo matatu hapa ambayo yamesababisha kukua kwa uchumi huu. Sababu moja ya tatu ambayo ameielezea anasema ni kuimarika kwa sekta ya viwanda iliyokuwa kwa asilimia 5.8 kwa mwaka 2011 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 1.9 mwaka 2010 na akasema kutokana na mwenendo mzuri katika maeneo ya nishati, uchimbaji wa mawe na mchanga pamoja na ujenzi. Hili Mhe. Naibu Spika, ni eneo moja ambalo amelizungumza.

Mimi kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nikubaliane na eneo hili lakini nina wasiwasi juu ya ukuaji katika sekta ya viwanda. Na hii ndio sababu ya kwamba ukuaji wetu wa uchumi unakuwa hauonesha impact kwa sababu unakuwa kutokana na sekta za huduma. Sekta ya viwanda halisi haijaonesha sura ya ukuaji wake. Jana baadhi ya waheshimiwa wajumbe waliingiwa na wasiwasi wasiwasi juu ya sekta hii ya uchumi kukua kutokana na uchimbaji wa mawe na mchanga, jambo ambalo linahatarisha usalama wa mazingira yetu. Mimi ninakubaliana nao, lakini ukuaji wa uchumi katika hasa maeneo ya viwanda bado katika eneo hilo hatujaweza kulifanyia kazi.

Tumuulize Mhe. Waziri hivi tokea serikali hii ya awamu hi ya saba ambayo sasa hivi takriban tunaingia miaka miwili tumeweza kuongeza eneo la viwanda au uzalishaji katika viwanda au kuanzisha viwanda vyengine vipya mbali ya hivi vya maji ya kunywa na mengine kwa kiwango gani. Na serikali ina mpango gani katika kipindi hiki kilichobakia, maana pengine tunaweza kuwa kwa kipindi hiki hatujaweza kuanzisha, lakini mpango wa serikali katika kuanzisha viwanda ukoje. Na kwa sababu hili ni eneo muhimu sana kwa nchi na ni eneo ambalo linahitaji kupewa kipa umbele ili kuona kwamba uchumi wetu unakua kutokana na sekta hii ya viwanda kuliko ilivyo sasa. Kwa hivyo tungependa tu Mhe. Waziri utueleze namna mlivyojiandaa katika hili na utekelezaji wake.

Jengine Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pia ametueleza kuhusu suala la pato la taifa, pato la mtu binafsi na akatueleza kwamba pato la mtu binafsi sasa limekuwa katika kipindi hiki na kufikia shilingi 960,000 ambazo ni sawa na dola za kimarekani 617. Hii ni taarifa njema pamoja na kwamba kiwango bado kinaonekana ni kidogo lakini vinaongezeka kwa sababu katika mwaka 2010 pato la mtu binafsi lilikuwa shilingi 782,000 kwa hivyo hapa panaonekana kwamba pana uongezeko. Kwa hivyo tabaan inaonekana kwamba pato la mwananchi limekuwa. Kwa hivyo tunakupongeza Mhe. Waziri kwa juhudi za kukuza na tunataka bado tuendelee na hatimae tutafikia kiwango kikubwa kama nchi za wenzetu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni suala la utekelezaji wa bajeti ya serikali ya kipindi kilichopita. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa ametuelezea juu ya utekelezaji wa bajeti iliyopita kama nilivyotangulia kusema kwamba katika kipindi cha mwaka 2011/2012 serikali ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 613.08. Lakini taarifa zinaonesha kwamba kiwango hiki cha fedha kimekusanywa kwa kiwango kikubwa kupitia katika taasisi zetu mbali mbali na wahisani wetu wameweza kuchangia na serikali imeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa. Lakini pia tuzipongeze taasisi zetu za ukusanyaji wa mapato TRA, ZRB kwa kuweza kufikia malengo na wengine kukiuka malengo ya ukusanyaji wameweza kukusanya vizuri. Pamoja na kwamba wenzetu wa TRA walishindwa kufikia malengo kutokana na kukosekana kwa kiwango kile cha fedha tulizozitegemea kuzipata kutoka kwa wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya shilingi bilioni 18, ambapo kwa mazingira tu ambayo hatukuweza kuyaelewa, fedha zile tumezikosa na ni fedha ambazo tayari tulikuwa tumeshaziweka kwenye mipango yetu ya maendeleo.

Sasa Mhe. Waziri na mwaka huu tumejaribu tena kuweka bilioni 21 fedha za wafanyakazi wa SMZ walioko katika serikali ya Jamhuri ya Muungano, fedha ambazo ni halali ni haki yetu kuzipata. Mwaka jana hatukuzipata na mwaka huu umetuwekea tena kwenye mpango wa maendeleo. Lakini Mhe. Spika, kwa taarifa tulizonazo kwamba katika kikao kilichofanyika Dar es Salaam, mwezi wa Juni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata nafasi ya kuulizia juu ya fedha hizo katika kikao na Mhe. Waziri Mkuu aliagiza kwamba fedha zilizokuwa zilibakia karibu bilioni 9 zilipwe kwa SMZ mbali ya zile ambazo zimekosekana. Sasa utwambie pesa hizo ama zimepatikana kutokana na agizo hilo la Waziri Mkuu au hazikuweza kupatikana na kama zimepatikana mbona hazikuonekana humu kwenye maelezo yako. Na kama hazikupatikana ni sababu zipi zilizopelekea kwamba fedha hizo zisipatikane.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametuelezea utekelezaji wa hatua za kuimarisha mapato na ameeleza hapa katika kifungu cha 36, 37, 38 ambapo katika kifungu cha 38 anazungumzia hatua za kiutawala ambazo zililenga kuongeza ujuzi wa usimamizi wa kodi wa TRA na ZRB ambapo ni kusajiliwa katika mtandao wa kodi wa

wafanyakazi wapatao 290 Pemba na Unguja na kufanya ukaguzi wa pamoja baina ya TRA na ZRB na baadhi ya walipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na hatua hizi za utekelezaji wa hatua za kuimarisha mapato, lakini kuna eneo ambalo mimi mara nyingi nimekuwa nilisisitiza lakini inaonekana bado ni sawa sawa na kumpigia gita mbuzi. Serikali imekuwa haioneshi juhudi la kulifanyia kazi eneo hili. Bado serikali inakusanya mapato yake kupitia taasisi hii kwa utaratibu wa makadirio, jambo ambalo kwa kweli halikubaliki katika dunia ya leo. Huwezi kukusanya kodi kwa makadirio na ukategemea kwamba mapato yako yatakuwa, huwezi kukusanya kodi kwa makadirio na ukategemea kwamba utakusanya mapato halisi yanayotakiwa. Na kwa sababu tunawafahamu wafanyabiashara wetu, lakini eneo hili linaonekana bado halijaweza kufanyiwa kazi au serikali haijataka kulifanyia kazi au serikali haijaonesha nia ya kutaka kulifanyia kazi.

Sasa kwa kweli hili ni tatizo, sasa hivi dunia nzima imeondokana na utaratibu huu hata wenzetu Tanzania Bara wameshaanza kubadilika na mapato yao yamekuwa kwa hivyo mimi niiombe sana serikali kupitia Wizara ya Fedha jambo hili ni muhimu, waachane na hizi blaa blaa za ukusanyaji wa kodi ambazo utaratibu huu wa kukadiria mapato ndio njia wanaopata nafasi ya kunyokoa nyokoa mapato yetu au ya kudokoa dokoa mapato yetu. Lazima tubadilike twende na wakati na mimi ninaamini kwamba hata kama hatuna uwezo mkubwa wa kiasi hicho lakini tukitafuta wafadhili wa kutusaidia katika eneo hili wataweza kutusaidia. Kwa sababu nia yetu ni kutaka kujinasua katika kukuza uchumi, nia yetu ni kukuza mapato ya nchi badala ya hivi sasa haya tuliyokuwa nayo. Kwa hivyo eneo hili kwa kweli linahitaji kuangaliwa kwa makini. Pamoja na kwamba tunakusanya mapato tunahisi tunakusanya mapato mengi lakini hatukusanyi mapato halisi ambayo pengine tungekusanya mapato halisi basi sasa hivi tungeachana na huu utaratibu wa kuanza kuwakamua kamua wananchi wetu kupitia vikodi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kweli ni muda mdogo lakini tuna mambo mengi ya kuzungumzia, nitazungumzia kuhusu vipaumbele, kipaumbele ambacho mwaka huu kimewekwa kipaumbele kinachozungumzia huduma ya afya. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, suala la afya ni muhimu kwa watu wetu na mimi nimpongeze sana Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa hatua aliyoichukua ya kuwaondoshea kinamama hawa wajawazito pale wanapotakiwa kufanya operation nimpongeze sana. Na jambo hili kwa kweli tumekuwa tukilizungumzia sana tokea katika awamu zilizopita. Kwa kuwa leo Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein ameweza kuchukua hatua hii tunastahili kumpongeza sana kwa hatua hii.

Lakni pia nimpongeze Mhe. Rais juu ya suala la kuimarisha ustawi wa wazee wetu hususan Sebleni ambapo katika kipindi kijacho Mhe. Rais amekusudia kuwasaidia milo mitatu wazee wale ambao tumewaweka katika nyumba free of charge. Mimi ninampongeza sana katika hatua hiyo na niombe kwamba suala hilo liendelee na ni suala muhimu. Na kwa sababu wazee wale ni wazee wetu na tumewahifadhi pale, inakuwa si vyema wazee wale tukawaacha wanatanga tanga kutafuta milo. Kwa hivyo kama watakuwa wanapata uhakika wa chakula basi itakuwa ni jambo jema na ile hifadhi ya wazee basi itakuwa ni sahihi.

Mwisho kwa kuokoa muda Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala la amani na utulivu katika nchi. Suala la amani na utulivu katika nchi ni suala muhimu sana na ni jambo ambalo tumelitafuta kwa muda mrefu, tunakumbuka tulikotoka, tulikotoka tulikuwa na mivutano mikubwa ya kisiasa. Nchi yetu ilikuwa katika hali ngumu sana lakini kutokana na juhudi za Rais Mstaafu Rais Karume na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Shariff Hamad wakaweza kukutana na kufanya mazungumzo na hatimae tukakubaliana sote kwa pamoja tuunde serikali ya umoja wa kitaifa ambayo sasa tunayo. Serikali ambayo imewezesha nchi yetu kuwa katika hali ya utulivu na amani.

Sote tumeshuhudia mashirikiano makubwa yaliyopo katika kuiongoza nchi hii, tumeshuhudia maendeleo yaliyopo katika nchi hii, tumeshuhudia mambo mengi ambayo yameweza kutusaidia katika kuimarisha nchi yetu. Leo tumeshughudia katika Baraza lako hili Mhe. Naibu Spika, kwamba back bancher wanaisimamia vizuri serikali. Tumeshuhudia mapato ya nchi yamekuwa, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hayo ni maendeleo makubwa. Lakini katika siku za hivi karibuni tarehe 26, 27 na 28 kumejitokeza kuvurugika kwa amani katika nchi yetu, nchi ilikuwa katika hali mbaya, shughuli za biashara zilikuwa haziendi, maduka mengi yalikuwa yamefungwa, masoko yalikuwa yamefungwa mabarabara hayapitiki, watoto wetu hawawezi kwenda shule halkadhalika na mambo chungunzima yameweza kufanyika. Amani tuliyokuwa nayo ile katika muda mfupi huu wa miaka miwili ikatoweka moja kwa moja.

Hebu tujiulize Mhe. Naibu Spika, ni kipi kilichopelekea kuwepo katika hali ile, wazanzibari ndio sisi tulioisimamia amani kwa muda mrefu na tukaweza kufanikiwa. Wapo wanaozungumzia suala la kuwepo kwa

muungano na kukataa kwa muungano. Hivi tujiulize katika style hii kweli muungano unaweza ukavunjika? Katika style hii tunayokwenda nayo, tabaan huwezi ukauvunja muungano katika style kama hii.

Mhe. Naibu Spika, katika wakati ambao wananchi wa Zanzibar wanatakiwa kuwa na umoja ni wakati kama huu, katika wakati ambao tunahitaji mshikamano wa pamoja ni wakati huu. Tunaamini kwamba ni kweli kuna matatizo katika muungano tunayo matatizo, tunayo malalamiko mengi sana katika muungano na kwa kweli tumekuwa tukiyazungumza hapa, tuna matatizo ambayo hayawezi kutatuka kutokana na katiba yetu ya muungano na katiba ya Zanzibar.

Sasa wakati umefika tumshukuru Mwenyezi Mungu ametuwezesha Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amempa kauli ya kukubali kufanya marekebisho katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume Mhe. Naibu Spika, imeshaundwa tumeshuhudia na leo hii iko Zanzibar imekuja kuzinduliwa. Lengo la Tume hiyo ni kuja kuchukua maoni kwa wananchi wa Zanzibar jinsi serikali yao wanayoitaka ya muungano iweje. Jinsi ya mambo mengine yaliyokuwemo ndani ya katiba ya muungano yaweje na leo Mwenyekiti wa Tume hiyo Jaji Warioba amesema hadharani kwamba atachukua maoni yote ya wananchi wa Zanzibar. Hata yale maoni yanayokataa kuwepo kwa muungan atayachukua.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hatuna haja ya kufanya fujo, hatuna haja ya kufanya vurugu, wakati huu unahitajika kuwa ni wakati wa umoja na mshikamano wazanzibari tunatakiwa tuwe na kauli moja juu ya jambo hili. Tutakapokuwa na kauli moja juu ya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano basi mafanikio kwa Zanzibar yatapatikana. Kwa hivyo nitumie nafasi hii kuwasihi wananchi wa Zanzibar kwa kweli Mhe. Naibu Spika, tuwe watulivu tutulie tuitumie fursa hii iliyopo kueleza tuliyokuwa nayo na maoni yote yatachukuliwa, hakuna haja ya kufanya fujo, hakuna haja ya kufanya mambo yatakayoweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu amani ni kitu muhimu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kwa sababu hotuba hii Mhe. Naibu Spika, ni yetu niwasihi sana waheshimiwa wajumbe bajeti hii ni bajeti yetu, bajeti ya serikali ni bajeti yetu ya nchi kwa hivyo tuiunge mkono. Serikali tu hapa imeleta mipango ambayo itaweza kutekeleza tuiunge mkono. Lakini hatimaye bajeti hii itatambuliwa kupitia wizara moja moja. Kwa hivyo hapo itakapokuja hiyo Wizara sasa, sasa itakuwa ni kati ya Wizara na Baraza la Wawakilishi na namna ya utekelezaji na mipango yake.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, hivi sasa tumebakiwa na *backbencher* watatu itabidi watumie muda mfupi sana. Wa kwanza Mhe. Rufai Said Rufai, wa pili Mhe. Amina Iddi Mabrouk na wa tatu Mhe. Mohammed Mbwana Hamad halafu tuanze mawaziri.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi sina budi kumshukuru Allah kwa mchana huu kuweza kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Omar Yussuf Mzee.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niende katika ibara ya 58 ukurasa wa 29 inayozungumzia Kuimarisha Ubora wa Elimu. Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii Mhe. Waziri alitwambia kwamba serikali inakamilisha madarasa 80 kwa Unguja na Pemba kati ya 200, na jumla ya madawati 500 yamesambazwa katika skuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa uoni wangu nimeona kwamba madarasa 80 na madawati haya 500 kwa kweli hatujafika katika ubora wa elimu, hiki ni kiwango kidogo na hakikidhi haja. Bado serikali suala zima la elimu ilipe kipaumbele kwa sababu elimu ndio nuru. Lakini ukifanya hesabu katika madarasa haya 80 yaliyopatiwa madawati 500 utakuta kwamba kila darasa moja litapata madawati sita au mengine saba, darasa letu lina uwezo wa kuchukua madawati 40 mpaka 60. Lakini kwa taarifa nilizozipata leo katika Kipindi cha Mawio kuna skuli moja hapa Unguja darasa moja linakaliwa na watu 90, kwa hivyo ukifanya mahesabu ni kwamba asilimia 90 ya wanafunzi wetu bado wanakaa chini. Kwa hivyo tukisema huu ni ubora wa elimu naona bado hatujafika katika ubora wa elimu tuko katika bora elimu tu, kwa sababu kwa hali yoyote ile mtu aweze kusoma.

Kwa hivyo, bado Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, ni vyema wizara kwa kupitia wafadhili mbali mbali suala hili la vikalio na suala zima la kurekebisha haya madarasa yakaweza kukamilika na yale yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kuweza kukamilika kwa muda mfupi.

Mhe. Naibu Spika, pia katika kuimarisha Sekta ya Kilimo ni kweli kwamba Mhe. Rais wetu suala hili amelipa hatua na usimamizi mkubwa toka kuanza kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar. Mwaka jana Baraza hili kupitia Mhe. Waziri, kilimo kilipewa kipaumbele na wakulima wakajiandaa kuimarisha hiki kilimo lakini ndani ya miezi tisa hii hatujapata jawabu rasmi kuhusu sekta hii ya kilimo. Lakini vile vile mwaka huu bajeti hii ya mwaka 2012/13 kilimo kiko katika kushika mkia na wananchi wetu wengi ni wananchi wanaotegemea kilimo. Kutokana na mabadiliko ya hali ya nchi kuna uwezekano Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wengi wakakosa huduma katika zile nguvu zao walizozitoa katika kilimo.

Wengi wamekosa pembejeo, wamekosa dawa za kuulia magugu, wamekosa hata yale matrekta kulimiwa kwa wakati. Kwa hivyo, bado hatua hii ni vyema Mhe. Waziri akaipa nafasi yake kutokana na wakulima wetu wa Zanzibar ndio wengi kulikoni wafanyakazi. Hivyo ningeishauri wizara suala zima la kilimo kulipa kipaumbele, kinyume na hivyo wananchi wetu watakata tamaa na watashindwa kujiandaa katika miaka mingine inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika ibara ya 76 ukurasa wa 38 Uimarishaji wa Ustawi wa Wazee. Mhe. Naibu Spika, suala hili ni tatizo, Zanzibar tunao wazee wengi ambao hali zao ni duni na wazee hawa wote ni wazee wetu na wanahitaji nguvu zetu, lakini ukiangalia hawa wazee tunaowahifadhi pale Sebleni ni wachache mno na wako wengine katika mitaa ambapo wale walioko Sebleni wana uwezo kuliko hawa walioko nje. Kwa hivyo, serikali sijui imechukua hatua gani kwa wazee hawa ambao bado hawana washughulikiaji, wako mitaani wanaombaomba.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kuna wazee wale ambao wanalipwa *welfare* wazee hawa kwa kweli serikali wamewasahau. Mzee huyu analipwa shilingi 5,000 hebu Mhe. Naibu Spika, mchukue huyu mzee yuko Mnarani Pemba kule anakuja kuchukua *welfare* Wilayani Micheweni, nauli ya kutoka Wilayani mpaka Konde ni shilingi 1,000, kutoka Konde mpaka Micheweni ni shilingi 1,500, kwa hivyo shilingi 5,000 atakazozipokea anazimaliza kwa nauli tu bila hata kunywa maji mara moja pale Micheweni.

Kwa hivyo, utakuta kima hiki wanachopewa wazee wetu kuhusu *welfare* kwa kweli hakiendi na wakati huu tulioanao na hawa wana haki katika nchi hii. Wazee hawa wana haki na serikali ifanye wajibu na huruma kuwaangalia wazee wetu hawa na wao ni jumla ya wazee, au kama uwezo hakuna basi na hapa pia ni kuwapa majukumu mazito kwa sababu yeye ana tamaa pesa zake shilingi 5,000 atapata chochote lakini pesa zile zinamalizika kwa nauli. Kwa hivyo, ni vyema serikali wawaangalie wazee hawa zaidi na zaidi.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha 98 ukurasa wa 40 hadi 60 hapa Mhe. Waziri alizungumzia mambo ya Ushuru na Kodi Mbali mbali. Mimi Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii baadhi ya vifungu vilivyomo nakubaliana navyo lakini baadhi ya vifungu sikubaliani navyo, hasa kwa kumuwekea Mzanzibari wa kawaida, msafiri wa Unguja na Pemba; msafiri wa Donge – Mjini kulazimisha kwamba mtu huyu aweze kutoa kodi ya kutoka anakotoka na anakokwenda, hapo bado Mzanzibari hatujamtendea haki, bado Mzanzibari tunam-bana. Wako watu hapa wa kutoa kodi katika nchi, tuna wageni wengi tu lakini tumewaachia huru tunamkaba yule mwananchi anayetoa pato la nchi.

Kwa hivyo, bado mimi nakubaliana na wale wote walisoema kwamba tuwaonee huruma Wazanzibari wanaotoka sehemu moja kwenda kwenye sehemu nyengine katika Zanzibar. Kwa sababu Zanzibar tunasema ni nchi moja, kwa hivyo kuwalazimisha hawa wawe wanatoa kodi ya shilingi elfu moja basi bado tutakuwa tunamuonea.

Mhe. Naibu Spika, katika hizi kodi basi kodi nyingi ni anazopambana nazo mwananchi wa Zanzibar. Ukizikusanya hizi kama ndugu zetu watu wa daladala kodi zao tu zinafika shilingi laki mbili. Sasa ukimuwekea kodi huyu utamfanya huyu Mzanzibari apandishiwe nauli ambayo kipato chake cha kila siku tumeshasema hapa kwamba ni shilingi 2,600 lakini chukua nauli ya kutoka Konde hadi Chake Chake ni shilingi 2,000 na huyu ana wajibu kila siku kusikilika katika nchi yake. Kwa hivyo, ule uzalishaji anaozalisha hapa na maisha yetu tuliyonayo unamfanya Mzanzibari ashindwe kumudu maisha yake. Hebu haya mengine wananchi wetu tuwaregezee tutafute njia nyengine za kukusanya mapato ili nchi yetu iweze kupata mapato zaidi.

Katika hili Mhe. Naibu Spika, kuna vyanzo vingi katika nchi hii vimedumaa, vinazalisha wala serikali haviviulizi. Mimi nakumbuka Mhe. Rais wa Awamu ya Pili, Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi miaka ya 80 mpaka 82 alianzisha zao la mpira Zanzibar, mashamba mengi kabisa yakapandwa mpira na huu mpira unazalisha hapa Zanzibar, lakini katika haya mambo ya kukusanya hatujaona katika hotuba hii ya mwaka 2012/13 wala 2011/12, kiasi gani mpira unazalisha hapa Zanzibar. Mpira huu, mashamba haya wamekodishwa nani ikiwa pato la nchi halipatikani. Kwa hivyo hivi ni vyanzo lakini inaonesha wazi kwamba kuna watu mapato haya wameyamiliki wao na serikali imenyamaza kimya.

Mhe. Waziri naomba sana suala utakapokuja nipate majibu ya dhati kuhusu masuala ya mashamba haya ya mpira, mapato haya yanakwenda wapi?

Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala zima la Muungano, wenzetu wengi hapa wamelizungumza. Mimi nasema kwamba wenzetu wa Tanganyika ndio wenye kuvunja Muungano sio Wazanzibari, kwa maana gani? Kuna kero nyingi, kero hizi za Muungano hazikuanzishwa na Wazanzibari kero hizi zimeanzishwa na wenzetu wa Tanganyika. Sasa ukifanya kero mimi nasema kero ni chukizo, chukizo hili linafika kama ni jambo la ndoa ukichukiza inafika mpaka ile ndoa kuvunjika. Sasa wao wanasema ni kero lakini mimi nasema hizi kero wao ndio wanaosababisha na huu Muungano wakaanza kuuvunja.

Mhe. Naibu Spika, ukikumbuka kwamba mwaka 1992 Bunge liliweka sheria ya kuanzisha Akaunti ya Pamoja ya Muungano. Mwaka 1995 ikaundwa Tume ya Pamoja lakini hadi kufikia muda huu Zanzibar wamekamilisha kuhusu Tume hii lakini Watanganyika wameshindwa kukamilisha mwaka wa kumi huu. Je, ni nani hapo aliyevunja Muungano? Ni nani waliovunja makubaliano? Kwa hivyo, ni hawa wenzetu sasa kama hatutokuwa na maamuzi mazito, magumu, tukaendelea tu sisi kuhami Muungano sijui hatma yake itakuwaje.

Mimi nampongeza sana Mhe. Rais wa Awamu ya Nne Mhe. Dr. Salmin Amour Juma, ingelikuwa hadi leo hatuzungumzi habari ya Vyuo Vikuu hapa, lakini akafanya ujasiri akaanzisha haya mambo na ndio tunafaidika Wazanzibari, na sisi awamu hizi tulizonazo kama tutakubali kuendeshwa tu hivyo hivyo hatima yake Zanzibar tutaimaliza kuiponza.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 70 kuna Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2012/13, maelezo yangu yako katika Mchango wa Serikali na Washirika wa Maendeleo. Ukiangalia mchango wa serikali, serikali imekusudia kutoa shilingi 47.9 bilioni na Washirika wa Maendeleo 293.2 bilioni.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nimepata mashaka makubwa na mashaka yangu yako kwa hawa tunaowaita Washirika wa Maendeleo ambao mimi ninawaita wafadhili. Mhe. Naibu Spika, inaelekea kwamba Wazanzibari hatutofika katika hatua ya maendeleo kwa kutegemea wafadhili, kima cha serikali ni kidogo kuliko cha wafadhili na wafadhili katika dunia wameshabadilisha sheria zao, habari ya kwamba nisaidie saidie hawataki tena, wameweka sheria nyengine mpya na sheria hizi tayari zimeshafika Afrika na hivi sasa zinachungulia Zanzibar. Kima hiki cha shilingi 293.2 bilioni sheria zao zinasema kwamba kama unataka nikusaidie ukubali kubadilisha sheria za nchi yako wanaume kwa wanaume wao wanne na wanawake kwa wanawake wao wanne.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda wapi! Huko si ndio tunakoelekezwa huko? Kwa hivyo kama nchi haitojipinda na ikatafuta vitega vyake uchumi na wakasimamia mapato ya nchi kidhati Mhe. Zanzibar tutaowana wanaume kwa wanaume. Ahsante sana.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia hapa kuwa wazima na wenye afya njema. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mwakilishi aliyeteuliwa hivi karibuni Mhe. Marina kwa uteuzi wake huo, lakini zaidi nampongeza kwa kuwa ni mwanamke mwenzangu.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii adhimu kabisa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake kwa namna alivyotuletea kitabu hiki, lakini pia ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 8 mpaka 11. Kitabu hiki cha Mhe. Waziri kinaonesha kwamba pato la taifa limeongezeka kwa asilimia kubwa, lakini ukiangalia kwa undani utaona kwamba mwananchi wa kawaida kwa kweli hafaidiki na ongezeko la pato hili mbali ya kuwa sekta ya elimu, afya ni bure lakini mwananchi huyu bado anahitaji awe na mahitaji muhimu kwa mfano awe na pesa mfukoni ili ziweze kumsaidia katika maisha yake ya kawaida.

Mhe. Naibu Spika, hiyo sekta yenyewe ya afya ukiangalia mwananchi yule hawezi kufika katika hospitali zetu kama hana mfuko wa pesa ili ziweze kumsaidia kwa mahitaji ya usafiri.

Lakini pia ukiangalia katika Sekta ya Elimu kwa undani sawa elimu ni bure, watoto wetu wanasoma bure, lakini ukimuangalia mzazi wa yule mwanafunzi ambaye anasoma bure pengine mtoto yule anapotoka nyumbani mzazi yule hajaweza hata kumpa chai angalau apate nguvu na kuweza kuwa makini darasani kumsikiliza mwalimu wake. Sio hilo tu Mhe. Naibu Spika, gharama siku hadi siku zinaongezeka. Sasa ina maana bado wananchi wetu ni masikini mno lakini pia kitabu kinatuonesha kwamba pato la taifa linaongezeka siku hadi siku. Sasa Mhe.

Naibu Spika, labda ningemuomba Mhe. Waziri abuni nyenzo mbali mbali za ajira za moja kwa moja ajira zisizo za moja kwa moja ili ziweze kumtatua mwananchi wetu na umasikini.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa huo huo wa nane Mhe. Waziri ametueleza kwamba Sekta ya Viwanda imeimarika katika mwaka 2010 – 2011 kwa asilimia 5.8. Lakini ukiangalia uhalisia hali ilivyo huko nje kwa kweli sekta hii muhimu inaonekana imekufa na haina maendeleo yoyote.

Zamani kwa kweli nchi petu hapa tulikuwa na viwanda vingi, kulikuwa kuna Kiwanda cha Sukari, Kiwanda cha Sigara, Kiwanda cha Ngozi na Viatu, lakini viwanda hivi vyote vimekufa. Mhe. Naibu Spika, sio hilo tu, hapa kwetu palikuwa na Kiwanda cha Maziwa na kama tunavyokumbuka mimi nilipokuwa mdogo ilikuwa ikifika siku ya sikukuu vibanda vya maziwa vyote vina foleni wananchi wako pale wanasubiri wapate maziwa, lakini hatimaye Mhe. Naibu Spika, viwanda vile vyote vimekufa. Sasa labda Mhe. Waziri atwambie kama kuna viwanda vya Mikate ya Boflo kweli vinaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atapokuja hapa atueleze huo uimarishaji wa viwanda umekua kivipi. Pengine labda sisi tuliopo hapa hatujaelewa vizuri, kwa hivyo naomba atapokuja hapa atupe ufafanuzi wa kina ili tuweze kuelewa hii sekta yetu ya viwanda imekua kivipi.

Nikija katika ukurasa wa 51 kwa kweli mimi binafsi nimeingiwa na wasiwasi mkubwa baada ya kuwasaidia wafanyabiashara wetu wadogo wadogo lakini inaonekana kwamba tunawaongezea kodi siku hadi siku. Mhe. Naibu Spika, sio hilo tu, lakini tunao wafanyabiashara wetu wakubwa wao tunaangalia namna ya kuwapunguzia kodi siku hadi siku. Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa mtizamo wangu mimi kwa kweli hapa hatujaweza kumsaidia mfanyabiashara wetu mdogo na ukiangalia mfanyabiashara huyo yeye ndiye anayeumia zaidi kuliko wafanyabiashara wakubwa.
Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huu niendelee na ukurasa huo huo na Mhe. Waziri ametwambia kwama kodi hizi zinaongezwa kwa sababu muda mrefu kodi hizi hazijaongezwa. Labda mimi nirejee kusema Mhe. Naibu Spika, kwamba bado serikali haijaangalia maeneo muhimu ya kubuni ili kuongeza kodi.

Mhe. Naibu Spika, kipindi kilichopita kama nina kumbukumbu vizuri mwaka 2008 Baraza lako tukufu hapa tulipitisha Sheria ya Kodi ya Majengo, ambayo hii kwa wenzetu wa Bara nadhani imeanza kazi zamani. Lakini toka tupitishe sheria hii ya majengo haijafanya kazi na toka tupitishe sheria hii kama ingefanya kazi vizuri kwa kweli serikali ingekuwa imeongeza kiasi cha mapato kikubwa mno. Sasa Mhe. Waziri atapokuja atwambie ni sababu gani ambazo zilipelekea sheria hii ya majengo isiweze kufanya kazi.

Kwa sababu sheria hii imemuelekeza zaidi mfanyabiashara mkubwa kwa sababu yeye anakuwa na majengo na majengo yale anatumia kwa kukodisha, haimgusi mwananchi wa kawaida kwa sababu haigusi mwananchi ambaye anakaa katika nyumba yake mwenyewe inamgusa mfanyabiashara mkubwa. Sasa Mhe. Waziri atueleze kwa nini haifanyi kazi sheria hii.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kusema kwamba wanategemea kupata msaada wa *Scan* chombo amabcho kwa kweli kitasaidia pale Bandarini kuona makontena ambayo yanatoka nje ya nchi na kuingia ndani ya nchi kuangaliwa kwa undani. Lakini Mhe. Waziri ninavyokumbuka mimi mwaka jana au mwaka juzi wenzetu wa *TRA* walifanya mazungumzo na Shirika la Bandari ili waweze kuweka chombo hiki, lakini Shirika la Bandari likawajibu kwamba hawana nafasi ya kuweka chombo kile. Sasa Mhe. Waziri atapokuja aje atwambie je, Shirika la Bandari sasa limepata nafasi? Kama limepata nafasi kwa nini isirejee mazungumzo na wenzetu wa *TRA* ili wakaona namna ya kuweka chombo kile.

Jengine Mhe. Waziri ametwambia kwamba anategemea kupata msaada kutoka katika Serikali ya China. Sasa msaada huo ni msaada wa aina gani, ni msaada wa kuwa serikali ilipe kidogo kidogo au msaada wa bure, aje kutueleza.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunaagizia vyombo kama hivi lakini ufanisi wake unakuwa mdogo. Kwa mfano, tulikuwa tuna *CT Scan* hapa ililetwa katika Wizara ya Afya lakini hatimaye Mhe. Naibu Spika, chombo kile kilikaa kwa muda mrefu na Mhe. Waziri akatwambia kwamba bado hawajafundisha wafanyakazi wao kuweza kutumia chombo kile. Sasa ili isije ikatokea kama ilivyotokea Wizara ya Afya, Mhe. Waziri atwambie je, amejitayarisha kiasi gani kusomesha wafanyakazi wake ili chombo hiki kitapofika kisikae bure kwa muda mrefu, amejipanga vipi lakini pia amejiandaa vipi na amefundisha wafanyakazi wangapi mpaka sasa hivi huku akiendelea kusubiri chombo hiki.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba si ungi mkono mpaka Mhe. Waziri ataponijibu hoja zangu hizi na nikamuelewa ndipo nitaunga mkono bajeti hii. Ahsante sana.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi kuunga mkono hoja hii. Kwa hivyo kama nilivyosema kuwa ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

Mimi kwanza ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutuwekea wazi juu ya deni letu la taifa. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametueeleza deni letu la taifa ni asilimia 10 ya pato letu la taifa. Sasa hii ilishitua watu wengi wakaona labda tunadaiwa sana kwamba asilimia 10 ya pato letu la taifa. Lakini Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari yafaa tujipongeze sana kwamba Zanzibar kumbe ni katika nchi ambazo hazidaiwi sana.

Mhe. Naibu Spika, nimeangalia ripoti ya IMF ya mwaka jana kuhusu nchi zote duniani na madeni yao, lakini ni madeni ya ndani. Watu wazima hawa ambao wanatusaidia kwa mfano kama United Kingdom, wao deni lao la ndani ni asilimia 82 ya GDP, nchi kubwa kama Uingereza hiyo.

Ukiangalia nchi kubwa tajiri kama United Arab Emirates, wao ni asilimia 16 ya GDP, yaani deni lao la ndani. Ukiangalia kuna nchi kama Switzerland ambayo ni nchi tajiri lakini bado deni lao la ndani ni asilimia 48 ya GDP. Mhe. Naibu Spika, huo ndio mfano.

Lakini nikagundua kuna nchi kubwa kama Saud Arabia ambayo sikufikiria kwamba serikali kama ile inaweza ikadaiwa, lakini na wao wana deni la ndani la asilimia 7.5 la GDP. Nilichogundua Mhe. Naibu Spika, ni Brunei na Libya tu ndizo ambazo hazidaiwi deni la ndani. Kwa hivyo Mhe.Naibu Spika, ninachotaka kusema kwamba kumbe sisi tunakopesheka, kumbe Zanzibar hatudaiwi. Kwa hivyo ile hofu tuliyokuwa nayo kwamba Zanzibar tunadaiwa sana, watoto wetu watakuja kuwa vipi kumbe hatudaiwi. Kuna nchi nyengine zinapindukia asimilia 100 ya GDP ya deni lao.

Atakaye hitaji nitampatia na ya kwanza ni Portugal ni asilimia 106 ya deni lao ndani. Halafu Singapore asilimia 100 ya deni lao la ndani, anayetaka bahati nzuri ninayo hii hapa nitampa. Kwa hivyo ninachosema kwamba kumbe Mhe. Waziri ni mtu makini sana katika kuangalia madeni.
Kwa hivyo ile hofu tuliyokuwa nayo tusiwe nayo asilimia 15 ni mchanganyiko wa deni la nje. Yaani Zanzibar hiyo asilimia 15 ni mchanganyiko, *almost* tunaweza tukasema hatudaiwi. Kwa kweli ni pongezi kubwa sana.

Halafu Mhe. Naibu Spika, jengine ninachotaka kuchangia mimi ambalo watu wamelifanya kubwa sana hata ukubwa wake hauonekani. Ni hii ada ya shilingi elfu moja ya bandarini.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi ninasafiri kwenda Dar Es Salaam ninatumia boti, lakini ninaapa na Mwenyezi Mungu nilikuwa sijui kama ninalipa kama shilingi elfu moja. Kwa hivyo hawa wananchi tunaowatetea kupiga kelele kwamba wataumia wao wanalipa hawajui na wala hawajalalamika.

Sasa ninadhani haya mambo mengine tutayaona kama ni makubwa hayawezi, mazito magumu lakini kumbe tunayafanya bila ya kujua kama tunayafanya. Sasa mimi ninafikiri hivyo Waheshimiwa tusilipe uzito mkuwa sana kwa sababu, tukilipa uzito mkubwa sana Mhe. Waziri katwambia ada ya bandari inatumika kwa kununulia madeski. Na sisi Wawakilishi wa Baraza hili Mhe. Naibu Spika, siku zote huwa ndio tunaopiga kelele kwamba watoto wanafanya vigongo kwa ukosefu wa madeski.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa una huruma basi wa kumuonea huruma kati ya mtoto na mtu mzima, wakumuonea huruma ni mtoto. Hata katika vita au maafa yoyote kwanza tunakimbilia kuwanusuru watoto. Sasa kufa sisi wazee wao wakapona watoto wetu kuna tatizo gani?

Mhe. Naibu Spika, wacha tuumie sisi wazee tujikamue shilingi elfu moja lakini watakaonufaika ni watoto. Watoto wa leo ndio taifa la kesho. Tukisema tunawaonea huduma watu wazima ina maana kitaifa la kesho kutwa litakuwa wapi, watoto watakuwa wamefanya vigongo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninasema mtu mwenye huruma ya kweli kweli basi ni mwenye huruma na mtoto. Huwezi kumuonea huruma mtu mzima usimuonee huruma mtoto. Kama huruma zako za kweli basi nawaomba waheshimwa wenzangu turudishe imani yetu kwa watoto wetu, tuunge mkono jambo hili, wala ninasema si jambo kubwa na zito, kwa sababu huyo mtu atakayetoa hata hajui kama anatoa, inakatwa moja kwa moja katika manunuzi ya tiketi wala hajui.

Waheshimiwa sote tunasafiri kwenye ndege, hivyo nani hapa anajua kama analipia ada ya uwanja wa ndege, tunalipa shilingi ngapi, zinalipwa kwenye tiketi wala hakuna anayejua. Kwa hivyo ninafikiri bure tusiwatie wananchi *pressure* wakafikiria kwamba watakadhulumiwa na hivi kwa jambo dogo hilo ambalo hata wenyewe hawalioni moja kwa moja. Hilo Mhe. Naibu Spika, limezungmzwa sana lakini kwa kweli limezungumzwa sivyo, wa kumuonea huruma ni mtoto kuliko mtu mzima.

Halafu jengine ni kutaka kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa jambo moja. Hii ni bajeti yake ya pili. Mhe. Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana, bajeti ya mwaka huu matumizi ya mipango ya maendeleo yanazidi matumizi ya kawaida.

Ukiangalia matumizi ya mwaka jana na matumizi ya bajeti yaliyomalizika ilikuwa matumizi ya kawaida basi ni madogo ukilinganisha na matumizi ya maendeleo. Na mara hii ni hivyo hivyo. Ni 52.6 kwa 47.4.

Waheshimiwa huko tunakotoka ilikuwa ni asilimia 30, 40 ndio bajeti ya maendeleo. Lakini bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa asilimia 60 na 70 ndio inakocheza. Ni kubwa mno, samahani bajeti ya kawaida. Kwa hivyo kumbe tunapiga hatua lakini hatujioni sisi wenyewe. Kwa hivyo ninampongeza sana Mhe. Waziri n wizara yake alau kwa kutufikisha hapa tulipofika *alhamdulillah* tumshukuru Mwenyezi Mungu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ninataka nilizungumze kwa ufupi sana kwa sababu watu wengi wamelizungumza ni hili la mchakato wa Katiba mpya. Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka niungane mkono na Mhe. Salmin Awadh kwamba na mimi bahati nzuri nimemsikia Jaji Warioba, nimesikia anasema hata wale wasiotaka muungano waje watoe maoni yao tutayachukua.

Kwa maana hiyo kwa kauli hii hivi sasa atakayefanya vurugu atakuwa na agenda yake ya siri. Lakini itakuwa sio tena ni suala la mchakato wa Katiba. Kwa hivyo mimi ninafikiri Mhe. Naibu Spika, ninatoa wito kwa Wazanzibari wote tuungane tuwe kitu kimoja, tusahau tofauti zetu ili tukatoe maoni yetu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Lakini hofu yangu Mhe. Naibu Spika, ipo hapa tukaja tukawa kama Ireland ya Kaskazini. Unajua wananchi wa Ireland ya Kaskazini muda mrefu walikuwa na mivutano, toka mwaka 1921 hasa ilipokuja kuota mizizi. Wengine Waprotestant wao ni unionist, wanapendelea union na wengine wanapendelea Jamhuri ya Ireland ambao wanaitwa nationalist.

Ikawa mivutano hii mikubwa sana Mhe. Naibu Spika, na ikenda wakapigana sana mpaka wakafika pahala wakaiweza, lakini kuiweza kwenyewe ni vipi? Jamhuri ya Ireland wachukue wa Jamhuri ya Ireland wanaotaka uraia wa United Kingdom wabakie kuwa raia wa United Kingdom.

Sasa hilo ni tatizo. Kwa sababu hivi sasa sheria ile ya Jamhuri ya Ireland inayomruhusu wale wananchi wa Irelanda ya Kaskazini ambao ni part ya United Kingdom, kuchukua uraia wa Jamhuri ya Ireland. Kuna wananchi wengine hao hao wa Ireland ya Kaskazini ni raia wa United Kingdom. Hilo ni tatizo katika nchi.

Tatizo liliopo hakuna ile identity moja. Huyu anataka hivi na huyu anataka hivi. Sasa hapa mimi ninafikiri tumuombe Mwenyezi Mungu atuepushe na itikadi za aina yoyote ambazo zitatugawa na sisi tukawa kama mfano huu wa Ireland. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutoa maoni yetu ambayo maoni hayo hayatoondoa umoja wetu Wazanzibari.

Lakini Mhe. Naibu Spika, itakuja jambo la kushangaza sana kwamba fursa hii inayokuja tukaitumia, matokeo yake ikawa Wazanzibari ikawa ni *loser*, ikawa hatukufaidika na mchakato huu. Na tutakuta *loser* na *unified factors*, kitu kitakachotuunganisha, tusahau itikadi za vyama na itikadi nyengine kama za kidini, tuwe na lengo moja. Ninahakika asilimia mia moja tutafanikiwa katika lile tunalolitaka.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tukikosea hapa sasa wenzetu wa upande wa pili watatupiga miswaki juu ya vichwa, maana yake itakuwa ni uzembe wetu wenyewe. Itakuwa ni makosa yetu wenyewe.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hilo naomba kwamba tujitahidi sana ili tusije tukafanya makosa. Kwa sababu nimetoa mfano huu wa Ireland ulivyoathiri sehemu hii ndogo yenye watu milioni mbili tu, lakini mitikiso yake ilikuwa ni mikubwa.

Ninakumbuka nyuma kulikuwa *Irish Republic Army*, ilikuwa London ilikuwa hapakaliki mpaka ikafika *town* city ikafungwa. Ilikuwa kwa kweli wana vuguvugu la hali ya juu. Sasa kwa kweli mimi sipendelei Zanzibar

twende huko, ninapendelea kwa kweli Zanzibar, sijui nani atatuongoza katika hili, maana atakayetuongoza akatuweka pamoja, tukatoa maoni kwa pamoja mimi simjui nani mpaka hivi sasa.

Lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu ajaalie atokezee mtu mwenye hekma na busara atuawidhi Wazanzibari tuwadhike, tukae pamoja kama tulivyokaa hii Serikali ya Kitaifa mpaka tukaipata basi na hili naomba atokezee mtu afanya hivyo hivyo, *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu amuwezeshe atuweke pamoja tuweze kufanikiwa ili sote twende kwa kauli moja na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafanikiwa.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha bila shaka pamoja na Waziri wa Miundombinu, najua hili litakuwa ni wazo kutoka kwake la kurejeshea fedha ile barabara ya kutoka Kangani kwenda Mkanyageni.

Hii barabara muda mrefu ilikuwa inapangiwa fedha lakini haziingizwi lakini mwaka jana kabisa hazikuingizwa. Lakini ninataka niwakumbushe wenzangu ambao tupo serikalini tunamsaidia Rais kazi.

Ninakumbuka Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano mbele ya Rais na wananchi basi, maana ingelikuwa peke yetu ni jambo jengine, alitoa ahadi kwamba barabara hii ya Kangani ikimalizika, tunataka kujenga Kangani mpaka Mkanyageni. Bahati nzuri wananchi wa Kangani na Mkanyageni walikuwepo na wakaisikia ile ahadi.

Na hata mimi juzi nilipojaribu kutia kifusi, nililaumiwa sana mheshimiwa usiitie kifusi hii Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano ameshaahidi kuja kuitia lami, mimi nikawaambia wacha niitie ni dharura tu hii, atakapokuja kuitia lami mheshimiwa barabara yake atakiondoa.

Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Barabara iwapatie fedha barabara hii ijengwe ili kujenga heshima ya Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano na heshima ya Rais ambayo vile vile wananchi baada ya kusema vile walitegemea ataisimamia itajengwa.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa fursa hii na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kujadili bajeti hii mpaka leo itafika kikome chake na inshaallah bajeti hii itapita bila ya vikwazo vyovyote *inshaallah*.

Lakini la pili ninapenda kumpongeza kwa dhati kabisa kipenzi changu Mhe. Omar Yussuf Mzee ambaye ni Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa hotuba yake ya bajeti nzuri ambayo imepangika na kwa kweli ninawapongeza sana pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kazi ngumu waliyoifanya hasa katika uchumi huu tulionao. Katika mazingira haya tuliyonayo, ninaamini kwamba lazima apatikane mtu mbunifu, mwenye uwezo ambaye atakayewea kutupangia mipango yetu ya bajeti katika mpango huu wa bajeti ya makisio sio cash bajeti. Kwa kweli Mhe. Omar Yussuf unastahili pongezi nyingi sana.

Pia naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wawakilishi wote ambao wamechangia kwa moyo mmoja, wamejikita katika kuchangia bajeti hii na kutoa maarifa yao yote ambayo yatasaidia kujenga uchumi bora wa nchi yetu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mwakilishi wetu mpya Bi. Mariana Joel Thomas kwa kuchaguliwa kwake na kuapishwa kuwa mwakilishi wa Baraza letu hili.

La tatu ninashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri na mimi nitaichangia kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa kabla ya kuchangia kwa dhati kabisa ninasema kwamba ninaunga mkono hotuba hii ya mpango wa maendeleo wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mpango huu wa makadirio kwa kweli umejikita katika yale mambo muhimu ambayo kwamba yanawakwaza wananchi, na imeangalia moja kwa moja kama ilivyo nyundo juu ya msumari. Kuona yale malalamiko ya wananchi wanachukuliwa hatua moja baada ya jengine.

Mhe. Naibu Spika, katika serikali hii ya awamu ya saba ya Umoja wa Kitaifa, tumepiga hatua kubwa katika masuala ya kiuchumi. Mpaka uchumi wa taifa umekua kama alivyosema Mhe. Waziri kwa asilimia 6.8 ambapo

pato la taifa ni shilingi bilioni moja point tisa nukta nane ukilinganisha na mwaka uliopita wa bilioni mia sita na arobaini na sita point nane.

Kwa hivyo hilo ni moja katika nukta nzuri ya maendeleo katika pato la taifa. Kwa muda wa miaka wa miaka mitano iliyopita hatukuweza kufikia lengo la asilimia 6.8. Sababu zipo za kukua kwa pato la kwani huduma za biashara ya mahoteli na utalii yamekua zaidi, ukiangalia idadi ya watalii waliongeza nchini, mapato ya utalii yamekua.

Vile vile sekta ya biashara imeimarika vizuri. Tukiangalia katika biashara ilivyoimarika utaona kwamba ukiangalia mwaka uliopita mwaka 2010 hata biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar ilikuwa kulikuwa na nakisi kubwa sana. Mwaka 2010 bidhaa kutoka Zanzibar zilizokwenda Tanzania Bara ilikuwa ni shilingi bilioni mbili point mbili tu na bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kuja Zanzibar zilikuwa ni shilingi bilioni 23 point 68.

Kwa hivyo katika mwaka 2010 kulikuwa na nakisi kubwa sana ya biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar ya shilingi bilioni 21.06. Lakini tuangalie kwaka mwaka 2011, kwa juhudi kubwa iliyochukuliwa na Serikali ya Kitaifa, urari wa biashara baina ya Tanzania Bara na Visiwani umeweza kukua karibu sana. Bidhaa zilizosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara ni shilingi bilioni sabini na moja point tatu tisa na bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar ni shilingi bilioni sabini na nne point saba tatu.

Kwa hivyo tofauti baina ya bidhaa ya kutoka Zanzibar na Tanzania Bara ni shilingi bilioni tatu point tatu. Kwa hivyo utaona biashara baina ya nchi za nje na Zanzibar imekua kwa uagiziaji na usafirishaji, na bidhaa au biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara umekua. Kwa hivyo haya ni maendeleo makubwa sana yamepatikana katika awamu yetu ya saba ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Jengine ni tumefaidika sana na biashara ya karafuu katika soko la dunia na hivyo kuweza kunyanyua uchumi wetu kwa Zanzibar na vile vile kuweza kusafirisha bidhaa za nje kwa uzuri zaidi. Kwa hivyo sekta ya biashara imekua mara tatu, kutoka asilimia saba hadi kufikia asilimia ishirini na moja point tano.

Kwa hivyo ni lazima tujipongeze na kuona kwamba biashara imekua na hii ni challenge kwetu au changamoto kwetu kuona kwamba biashara ikue zaidi katika mwaka huu 2012/13. Na ndio bajeti hii inaelekeza huko kwamba tuweze kukuza biashara zetu ili uchumi wetu uweze kukua.

Utalii umekua mara tatu zaidi kutoka asilimia tatu mpaka kufikia kumi nukta mbili. Kwa hivyo hivi inaelekeza kwamba utalii utakua zaidi kwa kipindi kinachofuatia. Kwa hivyo utakuta pato la mtu binafsi limeongezeka sana kufikia kutoka dola mia tano sitini mpaka mia sita kumi na saba.

Hivyo lengo la bajeti hii ni kuongeza vile vile pato la mtu binafsi liongezeke kwa mwaka unaokuja. Kwa hivyo ukiangalia mwelekeo wa bajeti hii ni kukuza uchumi wa Mzanzibari na ili uchumi wa ukue lazima biashara ikue.

Katika suala la viwanda wengi wachangiaji wamechangia suala la viwanda lakini ukurasa wa tisa wa bajeti hii, Mhe. Waziri wa Fedha ameeleza wazi hapa kwamba ili uchumi wetu ukue vizuri na ukue kwa kasi tunayotaka sisi basi ni lazima tujikite katika kuimarisha viwanda.

Waheshimiwa Wawakilishi ninataka niwahakikishie kwamba serikali haikulala juu ya suala la kuimarisha viwanda. Tunafanya kazi usiku na mchana kuona namna gani wawekezaji wataweza kuwekeza katika suala la viwanda. Sharti tufahamu kwamba serikali imeondoa mkono wake kabisa katika suala la kujenga viwanda. Serikali haijengi viwanda bali itaweka mazingira mazuri ili wawekezaji waweke kuja kujenga viwanda. Tusitarajie tena kwamba serikali itarudi tena katika kujenga viwanda vya sukari, ngozi na viatu, sigara, hapana. Viwanda vyote vitakavyojengwa vitajengwa na wananchi wenyewe waliomo ndani na wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Hivyo serikali kuona malengo yake namna tunawawezesha vijana wetu ambao wamemaliza masomo yao ya Vyuo Vikuu na wafanyabiashara wa Zanzibar wanaingia katika sekta hii ya viwanda. Tunaamini kwamba sekta hii ya viwanda itaweza kumeza au itaeka soko kubwa la ajira na wataweza wananchi wetu ambao hawana ajira wakapata ajira kwa njia rahisi.

Kwa hivyo mimi kama nikiwa ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, naomba nikuhakikishieni tuna kazi kubwa ya kufanya na tutahitaji misaada yenu mikubwa, wawakilishi wote na wananchi wote tukishirikiana kuona kwamba viwanda vinashamiri Zanzibar.

Changamoto ni Mhe. Naibu Spika, wakifika Zanzibar wanataka kuona bandari kubwa yenye uwezo wa kuweka meli kubwa ambazo zitakazoweza kuingiza mali ghafi nchini na kusafirisha mali zinazozalishwa viwandani.

Kwa hivyo changamoto kubwa ni bandari na pili ni umeme wa uhakika. Lakini hizi zote Serikali ya Zanzibar inafanya kila inavyowezekana kutatua matatizo haya. Kwa hivyo ninaamini kwamba kwa muda mfupi ujao viwanda vitashamiri nchini kwetu na hasa pale itakapoanza ile special economic zone itaweza kushajihisha wengi kuja kufanya viwanda hivyo.

Tukishirikana na wizara uwezeshaji, tutaanzisha business incubator. Hii ni taasisi maalum ambayo itawafanya Wazanzibari wenyewe waweze kuingia katika shughuli za viwanda na hasa wale graduate wanaotoka katika Vyuo Vikuu. Kwa hivyo mashirikiano baina ya wananchi na serikali na wafanyabiashara wote itaweza kusisimua msisimko mpya wa kuanzisha viwanda Zanzibar. Ninataka kuwahakikishieni kwamba serikali ipo pamoja na nyinyi katika suala hili.
Lakini sharti tufahamu kwamba suala zima la biashara linategemea sana kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu ili tuweze kupata biashara ziende vizuri zaidi. Wawekezaji wote aidha wa watalii au wa viwanda kuja Zanzibar itategemea amani na utulivu wa nchi yetu. Kwa hivyo amani na utulivu wa nchi yetu ndio suala la kujivunia na ndio suala ambalo litakalowezesha kujenga uchumi wa nchi yetu.

Uchumi wa nchi yetu utategemea sana kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Wanasiasa sote tumeshirikiana kwa pamoja kuona kwamba nchi yetu ina umoja wa hali ya juu, mshikamano wa hali ya juu, ina ushirikiano wa hali ya juu tukaweza kuzika tofauti tukaweka upande, tukajenga serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu.

Kwa hivyo amani ni moja katika tool muhimu sana ya kuweza kujenga biashara, viwanda na uchumi wenye kujihimili. Kwa hivyo mimi kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba sana chonde chonde Wazanzibari tusichezee amani tuliyokuwa nayo. Amani tuliyokuwa nayo, mshikamano tuliokuwa nao, umoja tuliokuwa nao ndio nyenzo muhimu ya kujenga uchumi imara utakaoweza kuiongoza nchi, ikiwa hatuna amani hivyo uchumi utaporomoka, utakwenda katika zero kabisa, tutakuwa hatuna la kufanya.

Kwa hivyo amani tudumishe amani, tushirikiane, tupendane, tuwe kitu kimoja kujenga nchi yetu. Hatukuja mtu yeyote kuja kujenga nchi yetu. Sisi wenyewe lazima tushirikiane kuijenga nchi yetu. Na nina amani ikishamiri na viwanda vitakuwa vingi Zanzibar na uchumi utakuwa mkubwa kabisa. Kwa hivyo ninawasihi Wazanzibari tushikamane na amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kutoa wasia wangu kwa Wazanzibari wote, kama hotuba yake alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi katika suala zima la uchangiaji ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katiba ndio sheria kuu ya nchi, ndio mkataba wa wananchi na viongozi wao, ndio muongozo mkubwa katika nchi yoyote ile. Kwa hivyo nchi ambayo haina Katiba ni matatizo matupu. Katiba ndio muongozo mkuu wa kuongoza nchi. Katiba tuitakayo lazima tuizae sisi wenyewe.

Kwa hivyo Tume ya Katiba inakuja. Leo imeshaingia Zanzibar na wameshaanza kutoa hotuba ya mwanzo ambayo ni nzuri kabisa na mimi nimeisoma. Kwa hivyo jamani tushirikiane kwa pamoja kusemezana, tofauti ziwe ni changamoto ya kuleta maendeleo na sio ugomvi, zisijenge chuki wala husda wala ugomvi katika kuvunja amani yetu.

Muhimu tuwe na uvumilivu, tuvumiliane, kila mtu ana fikra zake na kila mtu ana uoni wake lakini kila mmoja anastahiki heshima. Kwa hivyo tuheshimiane tuvumiliane na tukiweza kuvumiliana tukaweza kushirikiana, ninaamini kwamba wimbi hili litapita kwa urahisi kabisa na tutakuwa na Katiba tutaitakayo kwa maslahi ya Wazanzibari wote na Watanzania wote.

Umoja wa Wazanzibari ni kitu muhimu sana kuliko chochote chengine. Wazanzibari tushikamane tushirikiane tuungane tuwe kitu kimoja, tutaweza kufanikiwa kutoa maoni yetu katika Katiba, tutapata Katiba tunayoitaka. Muhimu viongozi sote tuwaelimishe wananchi waisome Katiba iliopo hivi sasa, waelewe ili waweze kujua wapi panahitaji au panastahiki masahihisho. Kwa hivyo sisi ndio tuna wajibu wa kuelimisha wananchi wetu na kuwapatia Katiba hii waisome na waweze kuichangia ipasavyo.

Wananchi wote tushirikiane twende kwenye Tume ya Katiba tutoe maoni yetu, tutoe joto letu. Ninatoa wito kwa Wazanzibari wote, wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanyabiashara ndogo ndogo na kubwa,

wanaume, wanawake, wazee, vijana, walemavu, taasisi za kiraia, tushirikiane kwa pamoja kutoa mawazo yetu katika tume hii, na ninaamini tutavuja salama katika mkondo huu. Baada ya kusema hayo ninasema ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kwa michango ya asubuhi hadi hivi sasa, ninachoomba kwamba Wajumbe wote tuje mapema tusikilize hoja tulizotoa zinajibiwa. Kuna utaratibu kuwa wengi wanapojibiwa hoja wanakuwa hawapo, halafu wakati wa kupitisha bajeti mabuti yanakuwa mengi. Kwa hivyo tunashauri mtu aje asikilize hoja yake, karidhika imekuwa basi kama hakuridhika ndipo anaweza kuomba kupata maelezo zaidi.

Baada ya maelezo hayo machache ninaakhirisha kikao hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea ninayo taarifa kwamba tumeanza kusikia michango ya Waheshimiwa Mawaziri na kwa kuwa hii ni kazi ya pamoja mimi nafikiri tufanye kila njia, mawaziri hasa wale ambao kwa njia moja au nyengine wameguswa wazi wazi na Waheshimiwa Wajumbe ndani ya bajeti hii, basi tupate maelezo mawili au matatu, ili Waheshimiwa Wajumbe waelewe nini kinachoendelea. Basi baada ya hayo nashukuru sasa ni zamu yake Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, anayefuatia tutamtaja baadae.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Alaasiri ya leo hii kupata nafasi ya kwanza kuichangia bajeti yetu hii ya serikali. Aidha, nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hiyo.
Mhe. Spika, na mimi nianze moja kwa moja kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na wasaidizi wake wote, kwa namna walivyotuletea bajeti hii mwaka huu hapa katika Baraza letu la Wawakilishi.

Lakini nimpongeze sana waziri mwenyewe Mhe. Spika, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nina hakika kuna mchango wake mkubwa kabisa katika bajeti hii na ndio maana bajeti hii imekuwa na dira na imekuwa na majawabu ya haraka zaidi na huhitajii sana kuisoma kwa sababu ukiisoma ukenda mbele unapata jawabu. Kwa hivyo, na yeye nampongeza sana Mhe. Rais.

Mhe. Spika, sioni ajabu Waheshimiwa Wajumbe wengi waliochangia hapa wamempongeza Mhe. Omar Yussuf. Mhe. Omar mimi namuelewa zamani sana huyu. Mwaka 1979 nilipata nafasi ya kumweka darasani na mimi nikasimama kwenye ubao nikamsomesha kidogo. Kwa hivyo, uwezo wake naujua. Nadhani ndio waziri mdogo kwenye Baraza la Mapinduzi, ndio mdogo wetu na kapewa kazi kubwa, lakini analelewa vizuri na sisi tuko tayari kumsaidia.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Rais kwa kumteuwa mwakilishi mpya na yeye ameongezea mtungo wa wanafunzi wetu waliokuwemo humu ndani Mhe. Bi Marina Joel Thomas. Namtakia kila la heri na fanaka katika kazi yake. Mimi namfahamu uwezo wake na nina hakika kwamba atafanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, kabla sijasahau, kwa sababu wakati unapoona raha na furaha basi ni vizuri kuyasema yale uliyokuwanayo moyoni kwanza. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi ukiwemo wewe mwenyewe Mhe. Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hii ni bajeti yetu sote, haina chama wala itikadi ni bajeti yetu na sote kwa nguvu zetu zote tuiunge mkono ili tuitekeleze vizuri. Nilimsikia Mhe. Mjumbe mmoja akisema hapa asubuhi kwamba hii tutaipitisha kwa nguvu zetu zote, tunangoja hizo wizara zenyewe sasa tuje tupambane nazo. Sasa naomba Mhe. Spika, nazo vile vile wazitendee haki kuzihoji zihojiwe lakini pale ambapo inafika wakati wa kuzipitisha basi zipitishwe bila ya matatizo.

Mhe. Spika, nimeshuhudia mambo makubwa sana mwaka huu katika Baraza hili hasa kipindi hiki, michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe, uwezo wao wa kujieleza kwa kweli ni mkubwa mno na hii ni sifa kubwa kwa Baraza letu na hata huko nje linazungumzwa vizuri. Mhe. Spika, sifa hizi zipitie kwako wewe

kwamba Waheshimiwa Wajumbe wameshakomaa katika kuchangia bajeti zetu na shughuli zetu mbali mbali ndani ya Baraza. Nawapongeza sana kwa sababu kila aliyesimama kamshinda mwenzake kwa kuchagia na kila mmoja ana ufundi wake na *study* zake za kuchangia.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja kuieleza bajeti hii kwamba ni bajeti yenye matumaini, bajeti ambayo imewagusa wananchi moja kwa moja na ni bajeti ambayo inajitosheleza, bajeti iliyokuwa wazi lakini pia imetoa majawabu, pale ambapo imeongeza kodi imesema kodi hizi zitatumika kwa shughuli fulani. Kila mahali ambapo imesema imeongeza kodi, imesema imeongeza na baadae itafanyika nini. Hili ni jambo kubwa ambalo hatujawahi kushuhudia katika bajeti zetu nyingi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakutakia kila heri na *Inshaallah* katika suala zima hili.

Mhe Spika, katika bajeti hii waheshimiwa wengi walizungumza sana suala la ajira na kwa vile suala la ajira kama ulivyotuelekeza limenigusa mimi upande wa wizara yangu, ni vyema nalo nikalizungumza kidogo. Mhe. Spika, hakuna hata mheshimiwa hata mmoja ambaye jambo hili hakulizungumza, hasa la vijana na tafsiri hasa ya ajira yenyewe. Tunapozungumza suala la *unemployment*, yaani ukosefu wa kazi. Ni hali ambayo tunasema ya kukosa kazi kwa watu wa rika lenye uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji na utoaji huduma. Hili ndio suala la watu hawa ambao hawajaajiriwa, lakini ni rika hili ambalo lipo na kwa hapa Zanzibar, rika hili tumeliweka katika umri wa miaka 18 hadi 38 kutokana na sera ya vijana. Lakini kwa kimataifa rika hili linajulikana katika miaka ya 15 hadi 24, na kwa hapa Zanzibar rika hili lina asilimia 17.1 ambalo bado halijapata ajira. Sio kundi dogo na lazima tunahitajia kulishughulikia ipasavyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga vizuri na lazima sote kwa pamoja jambo hili linatugusa kwa njia moja ama nyengine, kwa sababu ajira haiji serikalini tu au haiji kwenye sekta binafsi tu ajira iko kila mahala na inamgusa kila mmoja wetu. Kwa hivyo, ni lazima sote kwa pamoja tushirikiane ili tuhakikishe kwamba shughuli hizi zinaendelea.

Kwa upande wa serikali Mhe. Spika, serikali katika bajeti hii ambayo Mhe. Waziri ameisoma imetenga bilioni moja na milioni mia moja kwa mwaka huu wa fedha na nina hakika Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mwaka huu ataipa kipaumbele Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika kupitia mpango huu, ili zoezi zima la utoaji wa huduma za ajira kwa vijana wetu. Tulifanya haraka iwezekanavyo, natarajia katika miezi mitatu ya mwanzo tu basi mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Spika, katika mpango huu inagusa sekta karibu nyingi sana. Sekta ya uvuvi na kilimo na hasa katika bahari kuu na fedha hizi tumekusudia kununua boti mbili ambazo zitakwenda kufanyakazi ya uvuvi katika bahari kuu. Nina imani kubwa vijana wetu watakuwa tayari kufanya zoezi hilo. Pia shughuli za kilimo, shughuli za utalii, wajasiria mali mbali mbali na vikundi vya ushirika mbali mbali ambavyo vitajipanga, basi Mhe. Spika, vitafaidika na zoezi hilo. Tunakusudia zoezi hili kwa kutumia fedha hizi za bilioni 1.1 tuajiri au waingizwe vijana ndani ya ajira hii kiasi cha vijana 2,300 na mimi imani yangu ni kwamba azma hiyo tutafanikiwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Spika, suala la kukosekana kwa ajira ni tatizo la dunia nzima. Asubuhi nimelieleza hapa wakati nilipokuwa nikijibu swali la Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa urefu sana. Nililieleza kwa urefu na sijawahi kueleza swali kwa urefu kama hili la leo asubuhi. Nililieleza kwa sababu ya uzito na umuhimu wake. Shirika la Kazi Duniani, tayari kwa kushirikiana na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeandaa programu endelevu ambazo watakuwa wanatusaidia. Tayari tulishawaandaa vijana 33 katika Chuo cha Kizimbani kule. Vijana hawa ni wengi wao wana digirii ya kwanza na wengine wachache wana diploma, tutawasambaza katika wilaya zote. Vijana hawa kazi yao kubwa ni kwenda kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwaelimisha vijana katika vijiji, mitaa na wilaya mbali mbali ili kwanza wafahamu vipi wanaweza wakakusanywa na wakaweza kutengeneza ajira.

Mhe. Spika, vijana wamepata sifa kubwa na *Inshaallah* hivi karibuni watasambazwa na zoezi hili litakuwa linaendelea ili tuhakikishe kwamba tunawapata vijana wengi watakaopata ajira za kuweza kuwasaidia katika maisha yao ya baadae, kwa sababu ajira sio ile tu ambayo inatolewa katika serikali. Humu pia zimetajwa kuwa wanakusudia kuanzisha ajira 2,000, lakini ajira hizo ni kwa sekta ya binafsi na sekta ya umma. Sote kwa pamoja tunahakikisha kwamba serikali itafanya kila liwezekanalo, hatuwezi kutoa takwimu kuwa sekta ya umma itatoa ngapi na sekta ya binafsi itatoa ngapi. Lakini nina hakika kwamba sekta binafsi inaweza kuwa na mchango mkubwa zaidi katika suala hili.

Mhe. Spika, pale Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tumeanzisha kitengo maalum cha kuorodhesha, kurikodi, kuweka kumbukumbu. Wote wale ambao wanahitajia kujiorodhesha kwenye soko la ajira basi waje pale kituo kile kitakuwa kinafanya kazi hiyo na tayari kimeshaanza kazi na kinaendelea vizuri.

Kwa hivyo, natoa wito kwa wananchi wote na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote waliokuwepo hapa Mhe. Spika, kwa kupitia kwako wawashawishi, wawaelekeze vijana wao katika majimbo yao, wapite pale wizarani, kwa sababu wakati zinapopatikana fursa za kazi, basi itakuwa rahisi kuwachukua vijana wale tukaweza kuwapatia ajira kiurahisi zaidi. Kuliko sasa hivi ambapo kila mmoja anategemea kama atasikia tangazo kwenye redio au ataona kwenye gazeti.

Mhe. Spika, hata pale nje ya wizara tumeweka bao moja kubwa kabisa linaloelezea nafasi za kazi katika maeneo mbali mbali, zikiwemo kwenye mahoteli na sekta mbali mbali. Kwa hivyo, kwa kupitia Baraza hili Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwamba sote kwa pamoja tushirikiane katika suala hili, vijana hawa tunawahitajia kuwapa nguvu zetu zote ili waweze kupata soko la ajira.

Mhe. Spika, nilizungumza hapo mwanzo na bado naendelea kulizungumza suala hili kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa kipaumbele katika suala zima la ajira kwa vijana. Haikuwa rahisi safari hii kuweka kiwango kikubwa cha bajeti, lakini hiyo ni hatua moja, pamoja na kwamba bado hatujafika mahali pakusema kwamba mfuko wa AK na JK tumepata mafanikio makubwa, lakini angalau tumeweza kutoa mikopo ambayo imefika 726 na mingine inaendelea.

Lakini hivi karibuni Mhe. Rais alizindua mfuko wa uwezeshaji na *Alhamdulillah* tumekusanya tulichokusanya na kamati hii ina wajumbe mahiri kabisa, humu Barazani tuna Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ni mjumbe wa kamati hiyo na wengineo. Lakini nasema Mhe. Spika, kwamba hii ni kamati iliyokuwa na uwezo wa kuweza kuwashawishi na kuwaomba wenzetu ambao wana uwezo kuchangia mfuko wa uwezeshaji. Tumeshakusanya kiwango fulani cha fedha natarajia kwenye bajeti yangu nitakaposoma nitataja kiwango hicho, lakini tunakusudia kabla ya kusoma bajeti tutafanya kikao chengine cha sekta au taasisi nyengine katika kuchangia. Tunakusudia kukusanya kiasi cha bilioni moja na laki mbili hivi, ili tuongezee nguvu na hivi vikundi vyote vya ushirika ambavyo waheshimiwa wamelalamika kwamba bado havijawezeshwa, kwa kupitia mfuko huu basi *Inshaallah* tukijaaliwa tutaviwezesha bila wasi wasi wowote wala ubaguzi wowote.

Pia tuna mpango mzuri kwa kupitia wizara ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary katiba na sheria kwa kupitia kitengo chake cha wakfu na mali ya amana, katika fedha maalum ambacho tunatarajia hivi karibuni kitazinduliwa. Tumeshazungumza na wahusika utaratibu ambao utatumika katika fedha zile kuwapatia wananchi, ili tuweze kuwasaidia na baadae waweze kutoa zaka kwa njia ile au faida ile ambayo wataipata.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kuzishukuru sana taasisi binafsi ambazo zimeanzisha utaratibu wa kuwaajiri au kutafuta kazi nje ya nchi. Lakini hili nilichangie sambamba na wakati ambapo nitakuja kuchangia hoja ya Muungano. Kwa sababu ni vizuri tukaelewana mapema katika suala hili. Ajira hizi ambazo zinatolewa sasa hivi na leo asubuhi nilitoa ufafanuzi wake. Tayari kuna kampuni mbili tumeshazipa maelekezo, moja tayari imeshapata kibali na nyengine imo kwenye hatua za kukamilisha na nyengine tunazungumza nazo sasa hivi, jumla yake ni tano. Hizi zitakuwa na madaraka kamili ya kutafuta ajira nje ya nchi na ikiwezekana hata ndani ya nchi kuwasaidia wananchi wetu na vijana wetu kuweza kupata kazi.

Tunafanya hivi makusudi Mhe. Spika, kwa lengo la kupunguzia vijana wetu adha ambazo wanazipata sasa hivi katika suala zima la ajira. Hatua nyengine ambayo tutaichukua ni kusajili rasmi au kuitambua sekta isiyo rasmi kwamba sasa ifanyekazi rasmi. Narudia tena. Sekta ambayo sio rasmi lakini ifanye kazi rasmi yaani itambuliwe na tutaanza na huduma za usafiri. Wale madereva wa daladala au taxi, maskini ya Mungu mpaka wanazeeka hawana mkataba wala hawana khatma. Sasa wale wote tutawaorodhesha, tutaunda umoja wao mkubwa kabisa kama ni ushirika wao na tutataka wawe na mikataba yao ambayo pia italinda maslahi yao ya baadae. Ikiwa ni pamoja na *social security* vile vile. Mwelekeo umeonesha kwamba wako tayari sasa hivi, hatua hizo ziko mahali pazuri kabisa na siku sio nyingi na tayari kwenye bajeti yetu na hili litajitokeza kwa sababu ni jambo ambalo tumeshaamua kulifanya, kuifanya sekta ambayo sio rasmi na kuifanya iwe ni sekta rasmi.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, zingatia na muda.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, namalizia katika mada moja iliyobakia. Mhe. Spika, suala la vyama vya ushirika tutaendelea kutoa taaluma, tutaendelea kutoa huduma mbali mbali, tutaendelea kutoa mafunzo ya kila aina ili kuhakikisha kwamba vyama vya ushirika vinapata mafunzo ya uhakika na hivi karibuni tunategemea kupata mtaalamu kutoka Rwanda, ambaye asili yake ni kutoka India atakuja kutoa mafunzo kwenye sekta hizi za vyama vya ushirika, hasa kwenye viwanda vidogo vidogo na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, jambo ambalo napenda kulizungumza ambalo kwangu mimi litakuwa ni la mwisho ni suala zima la Muungano. Suala la Muungano nataka nilizungumze hapa hasa mchakato huu wa katiba. Naomba nitoe wito, kutokana na historia yetu jamani, suala hili hakuna sababu ya kumzuwia mtu yeyote yule ambaye anataka kutoa maoni yake anaruhusiwa kutoa wala hakuna matatizo. Leo tumeona kwenye magazeti mwenyekiti amezungumza suala hili la kutoa fursa na huu ndio wakati wenyewe Mhe. Spika. Kwa hivyo, mtu yeyote mwenye maoni yake, wazo lake kuhusiana na muundo wetu wa Muungano wakati ndio huu umefika sasa hivi, tusiwe na woga wala wasi wasi kila mmoja ana haki ya kusema.

Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo katika kitabu cha Mhe. Waziri kwa ruhusa yako, alisema hivi, 'katika kuwa na fikra tofauti juu ya muundo wa Muungano wetu, wapo wanaotaka muundo wa Muungano uendelee na wako wanaotaka marekebisho katika muundo wa sasa. Kwa hivyo, wote hawa wanaruhusiwa kutoa maoni yao na wasiwe na mashaka. Sisi upande wetu na wao upande wao wananchi wote sote tuwe kitu kimoja kwa sababu hili ni jambo letu sote na tunahitajia kulifanyia kazi kwa pamoja. Lakini naomba sana hasa vijana. Jambo ambalo nilisema mwanzo kwamba nitalisema baadae, kulikuwa na suala la ajira za nje, hivyo naomba vijana watulie, kwa sababu nchi za nje wakija wakiona vijana wetu hawajakuwa na utulivu huku basi kupata kazi nje kutakuwa mashaka kidogo.

Kwa hivyo, naomba *Inshaallah* sote tutulie tume imeshaingia tutaisikiliza na tutoe maoni yetu na *Inshaallah* sote tuchangie kadiri itakavyowezekana. Chakula ndio kinapikwa sasa hivi, tusije tukafika mwisho huko tena ukajakusema nimesahau kuweka chumvi na hiliki.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja na tunaomba *Inshaallah* sote tuunge mkono hoja kwa sababu ni jambo letu sote, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Tunashukuru. Mhe. Haroun Ali Suleiman, umetumia muda mkubwa kidogo, lakini wajumbe tunaofuata tutajitahidi kutumia dakika 15 ili tumpe Mhe. Waziri muda wa kutosha. Tumkaribishe basi Mhe. Said Ali Mbarouk, Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na baadae tumkaribishe Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi pengine muda wangu nitakuachia mwingi, kwa sababu nina mambo machache ambayo nilitaka niyazungumze. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake na namna alivyowasilisha. Nitangulize tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono sana hoja yake.

Mhe. Spika, nianze kwa kuzungumzia suala la utalii ambalo lilizungumzwa na wachangiaji wawili au watatu. Mhe. Spika, kwanza niwakumbushe Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tumeamua kuwa utalii ndio sekta kiongozi katika nchi yetu na kwamba hili ni letu sote na mafanikio yake ni kwa wananchi wote na taasisi zote, wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mwezi Oktoba mwaka jana Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein, alizindua dhana ya utalii kwa wote. Hii ni dhana muhimu na utekelezaji wake unatuhusu sote, maana yake ni kwamba tunaendesha utalii ambao sasa unufaishe wadau wote katika sekta ya utalii. Iwanufaishe wananchi kwa ujumla na kwa mapana yake, inufaishe serikali na pia wawekezaji wa sekta ya utalii.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sekta ya utalii kwa mapana zaidi ilikuwa iko katika, wachumi wanasema *macroeleven*. Sasa tunataka kuhakikisha kwamba pia inasaidia katika ile *macroeleven* ya hali ya uchumi wa nchi yetu. Nitoe mfano wa msimu wa karafuu Pemba Mhe. Spika. Ikifika msimu wa karafuu nyingi Pemba kila mtu huwa ni sehemu ya chumo lile, aliye na mikarafuu huwa anafaidika, aliyekuwa hana ni mchumaji tu wa karafuu na yeye huwa anafaidika, aliyekuwa hawezi kuchuma ni muanikaji tu basi na yeye huwa anafaidika.

Mhe. Spika, pia mafundi wanafaidika katika kujenga kambi za karafuu na hata kinamama wale ambao wanaotengeneza usumba basi kambi zake ni muhimu sana katika uchumaji wa karafuu. Kuna wale wanaofanya biashara ndogo ndogo za mandazi ni muhimu wanafaidika, kuna wale wanaofanya mikate ya ajemi au ya bekari, kwa ujumla wale wakulima wa ndizi, muhogo na wa nazi wote kwa kweli msimu ule huwa ni msimu wa chumo lao. Kwa hivyo, dhana ya serikali sasa ni kuupeleka utalii wa Zanzibar uwe katika hali hiyo, kwamba msimu wa utalii iwe unasubiriwa na unashajihishwa na kila mwananchi wa Zanzibar, tuone kwamba manufaa yake yanakua na *multiply effect* kubwa katika jamii yetu. Sasa huko ndiko ambako tunakwenda na hili sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Kamisheni ya Utalii, jukumu letu kubwa hivi sasa ni kuelimisha jamii katika hili.

Tumeanza na semina mbili moja Pemba na moja Unguja juzi na tunaendeleza semina nyingi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa kwa upana dhana ya utalii kwa wote. Nina hakika Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukijaaliwa na wao tunatafuta uwezo wa kuwafanyia semina ili waweze kufahamu hasa nini utalii kwa wote na waweze kusaidia katika kuuelimisha na kuuendeleza. Nina hakika kwamba wajumbe wako watakuwa ni sehemu muhimu katika suala hili.

Mhe. Spika, jengine lililozungumzwa ni suala la namna gani Wazanzibari hawajafaidika sana na sekta ya utalii. Inawezekana kauli hii ikawa ni kweli ndio maana tukaja na dhana hii. Lakini pamoja na hayo hivi sasa kuna wananchi wa Zanzibar ambao msimu wa utalii ukimaliza kwao ni tatizo kubwa, kuna wale wenye gari aina ya mabasi na daladala mbali mbali ambazo zinachukua watalii, msimu ukisha kwao huwa ni athari kubwa na huwa ni wakati wa ukata mkubwa katika matumizi yao. Pia ni kweli kwamba bidhaa ambazo zinatumiwa kwenye mahoteli hivi sasa kwa kiwango kikubwa zinatoka nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hilo nakiri na ndio maana katika kitabu hiki Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, katika ukurasa wa 40 kifungu cha 79(2) amesema kwamba atajitahidi kuimarisha upatikanaji wa zana za kilimo, mbegu bora na mbolea kwa wakulima sambamba na uimarishaji wa zao la karafuu. Kwa hivyo, serikali imeliona hili na ndio maana katika bajeti hii hilo limechukuliwa tahadhari na tujitahidi kuona kwamba Wazanzibari wamekuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa mbali mbali ambazo zinaweza kuuzwa katika masoko ya utalii. Kwa hivyo, kama serikali ni letu sote, lakini pia wananchi na wao wanapaswa kujiweka tayari na hilo na kuona kwamba kuna soko la bidhaa ambazo wakizalisha wanaweza wakauza kwa bei nzuri.

Kwa hivyo, wito wangu ni kuwaomba wananchi waone kwamba soko la utalii liliopo basi wajitahadi kuzalisha bidhaa za ndani, badala ya bidhaa zile kuagizwa kutoka nje basi ziwe zinatoka hapa hapa ndani, na kuuzwa kwenye mahoteli ya kitalii kwa ajili ya kupata tija kubwa zaidi.

Kwa hivyo, ni muhimu kwamba bidhaa zinazozalishwa ziwe zile zenye kiwango, kwa sababu wenzetu mara zote wanajitahidi kuona kwamba bidhaa zinazouzwa au kuliwa mule ziwe zimefikia kiwango. Kwa mfano, wakati mwengine wananchi wanalalamika kwamba wanayo mayai, lakini hawana sehemu ya kuyauza.

Mhe. Spika, ni kweli kwa sababu uzalishaji wenyewe wa mayai kuna matatizo mengi ambayo kiafya huwa ni mtihani kidogo. Kwa maana hiyo, ni muhimu bidhaa ambazo tunazozalisha ziwe zenye *hygienity* na pia ziko *organic*.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumzie kuhusu suala la umuhimu wa sensa. Kwa kweli nawaomba wenzangu kwa suala hili kwamba tuwahamasishe watu wetu wajiweke tayari kwa ajili ya kuhesabiwa siku ya sensa itakapofika, kwa sababu mipango yote ya maendeleo katika nchi yetu inategemea na idadi ya watu waliomo ndani yake.

Kwa hivyo, si busara hata kidogo kuwazuia wananchi wetu au sisi wenyewe, ni vyema sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuchukue dhima ya makusudi kuona kwamba tumewashajihisha wananchi tunaowawakilishi hapa washiriki vyema katika sensa.

Mhe. Spika, suala hili lina matatizo yake mengi. Kwa mfano, Tume ya Uchaguzi kila mara hufanya mapitio ya mipaka ya majimbo na wadi, kiwango kikubwa wanachokitumia ni idadi ya wakaazi katika jimbo. Pemba tulikuwa na majimbo 21 kabla ya Sensa ya mwaka 2002, lakini Sensa ya mwaka 2002 ilipofanywa ikaonekana kwamba idadi ya wakaazi Pemba imepungua, basi Tume ya Uchaguzi ilifikia uamuzi wa kuyapunguza na kufikia hadi 18.

Kwa hivyo, tukifanya mas-khara tena mwaka huu tukisema wananchi wetu tusiwashajihishe na kwenda katika sensa, basi Tume ya Uchaguzi inaweza kuchukua data ya Sensa ya mwaka 2002 na mwaka 2015 iwe mtihani mkubwa.

Kwa maana hiyo, kisiasa ningewashauri sana wananchi waone kwamba, ili kudhibiti majimbo pamoja na wadi zao basi ni muhimu sana kushiriki katika sensa, kwani wale wanaohesabiwa ni wanafamilia, yaani kuanzia baba mpaka mtoto aliyezaliwa siku ile.

Kwa hiyo, ni muhimu sana na wala hakuhitajiwi kitambulisho cha kura wala *ID*, isipokuwa ni wananchi wanaoishi katika nyumba ile. Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa Waheshimiwa Wananchi washiriki katika sensa kwani ni jambo muhimu ambalo litatupa nafasi ya kuzingatia idadi ya wananchi wetu, ili mipango ya kiuchumi na kimaendeleo itakapofanywa tuwe na usahihi wa *data* ambayo tutakayoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho nimuunge mkono sana Mhe. Waziri wakati alipozungumzia kuhusu suala la maoni juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano tunayoihitaji. Kwa kweli hili ni jambo muhimu ambalo wenzangu wameshalizungumza sana, ni kweli kanuni zetu zinakataza kurejea, lakini kwa umuhimu wa suala hili naomba Mhe. Spika uniruhusu nizungumze kidogo sana.

Suala hili ni muhimu sana kwani ni muda mrefu tumekuwa tukiulalamikia muungano ulivyo, unavyotuathiri Wazanzibari, una kero nyingi na wala nyengine hazitatuki. Sasa wakati wa kupata dawa yake ni kushiriki katika uandaaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nimefurahi sana kwamba Mwenyekiti wa Tume hii Mhe. Jaji Warioba katika gazeti la jana alinakiliwa na vyombo vya habari akisema kwamba, Mhe. Spika naomba kunukuu "hata wanaotaka kuvunja muungano walete maoni yao watasikilizwa". Kwa kweli hayo ni maneno ya Mhe. Mwenyekiti wa Tume aliyosema.

Kwa hivyo, ni jambo zuri kwamba wananchi wasiipoteze hii fursa na twende kwa wingi tukaseme tuliyonayo na wale wanaotaka serikali moja waseme, tatu, nne au tano. Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwamba katika hili sera za vyama tuziangalie kwa miwani mikubwa.

Mimi binafsi sikusudii hata kidogo kuiunga mkono ile Sera ya Serikali Tatu. Sasa Mnadhimu Mhe. Rashid Seif Suleiman akinitia adhabu kwa hili basi niko tayari, lakini ninayo maoni yangu, uhuru wangu na wakati ukifika Mhe. Spika nitaeleza bila ya woga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wazanzibari tujitokezeni, tuzungumze mwenye kutaka serikali nne sawa, tano sawa, tatu sawa, mbili ya aina yoyote iwe za mkataba au jambo gani ama mfumo gani tuzungumzeni na hata moja. Lakini jambo la msingi kwa kila Mzanzibari hii ni fursa adhim ambayo adimu tukiipoteza, kwa kweli itakuwa tumepoteza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru na kama nilivyoanzia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naomba niunge mkono hotuba ya Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kupata wasaa huu mdogo wa kuchangia Hotuba hii muhimu ya Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, pongezi nyingi zimeshatoka na mimi sitaki nipoteze muda isipokuwa naunga mkono wenzangu wote waliompongeza vizuri sana Mhe. Waziri.

Mimi kwanza Mhe. Spika, nimejaribu kwenda Maktaba nikaangalia takwimu za kiasi ya miaka mitano iliyopita ya Bajeti ya Serikali na kufanya *reference* ya bajeti yetu ya mwaka huu. Kwa kweli nimeona Mhe. Spika ule mchupo ambao tumeupiga kinambari, kimatumizi pamoja na kimapato na wala sitaki kupoteza muda wako Mhe. Spika.

Lakini nataka kusema kwamba kati ya mwaka 1997/98 mpaka mwaka 2002/03 kwa miaka minne tulikuwa na *deficit* bajeti na miwili tu tena hiyo miwili yenyewe hiyo *margin* tulikuwa tuna-*operate* inatisha. Lakini *Alhamdulillah* tumeondoka huko kwa juhudi zetu, kwa mshikamano wetu pamoja na ari yetu ya kutaka kujitegemea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naipongeza sana Wizara ya Fedha na Mipango kwa kututoa huko tulikokuweko na kutuweka sawa na leo tunayo bajeti kabisa, tena wakati huo tulikuwa tunazungumza Mhe. Spika naomba nikariri mwaka wa mwisho tu mwaka 2002/03. Mhe. Spika, mapato ya kawaida yalikuwa ni shilingi milioni 46,516.6/= na matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi milioni 58,433.9/= na hapo utaona *deficit* ya shilioni milioni 11,917/=.

Sasa leo *Alhamdulillah* mwaka huu Mhe. Waziri hapa ametupa bajeti ambapo kwenye *recurrent* kwanza sikuiweka kwenye mapato na matumizi, lakini kwenye matumizi yote ni shilingi bilioni, yaani tumetoka milioni na sasa tuko bilioni 307.5/= na *capital* ni shilingi bilioni 341.2 na jumla yote ni shilingi bilioni 648.9/=. Kwa hivyo, hiyo inatuonesha jinsi tulikokuweko huko na tulipo leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitoe pongezi zangu za dhati kabisa narudia tena kwa wizara kwa kutuongoza, kutuelekeza na mashirikiano ya pamoja, hakika huu ni mchupo mkubwa sana. Hivyo, ni vyema juhudi zetu inabidi tuziimarishe na kuimarisha kwenyewe wenzangu tayari wameshaeleza kwamba zote zitakuja kwa amani, umoja,

masikilizano na haja ya kubadilika kufanyakazi na hilo ni suala la msingi kabisa, yaani lazima tubadilike kufanyakazi. *(Makofi)*

Kwa mfano, hapa wakati wa asubuhi nilijibu swali la Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ule mchupo wa mapato yao wanayokusanya na sio Halmashauri ya Chake Chake tu ni Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji na wao pia wameonesha kuchupa katika makusanyo yao. Mhe. Spika, hii yote inaonesha uwajibikaji wao na kufahamu kwamba ku-*survive* ni kufanyakazi na kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Kwa kweli hili nilisema nizungumze kwa ufupi sana na mimi kuonesha kwamba naunga mkono juhudi hizi za Wizara ya Fedha katika kuzalisha zaidi na kupata fedha zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu yale mambo ambayo wizara yetu imeguswa. *GSO* Mhe. Spika imesemwa kwamba haifanyikazi ipasavyo watu wanaajiriwa bila ya sifa zinazotakiwa.

Mimi nasema Mhe. Spika watu wanaajiriwa kwa sifa zinazotakiwa na hiyo ilikuwa ni *history* huku nyuma, kwa sababu sasa tumekuwa wakali na tunafuatilia, yaani sasa imekuwa ni *joint project* kati ya Wizara ya Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na wizara husika yenyewe na wala sio kama zamani wizara inamaliza mambo tu, sasa imekuwa ni mafya matatu kwa hiyo mtu kupita sasa ni kazi kweli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumewabaini watu kupitia *GSO* wengine wana *Masters* lakini cheti cha *Form IV* amedanganya na sijui amepata vipi *Masters* na watu hao wapo Mhe. Spika. Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba *GSO* wanafanyakazi tena ya kupigiwa mfano kabisa, najaribu kukariri bajeti *speech* yetu ya mwaka jana kwamba tulisema tutafanya upekuzi wa watu 529 na mwaka huu tulionao tutafanya upekuzi wa watu 500 na hili ni zoezi endelevu upande wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kuwahakikishia wenzangu kwamba tushirikiane tunaposema upekuzi hatukusudii kumtia mtu hatiani aa! Isipokuwa huu ni utaratibu wa kawaida kama vile kiusalama, siri za serikali lakini hasa kwenye ajira lazima tumjue mtu ile *authentic* yake, yaani ule uhalali wake isiwe mtu anacho cheti lakini hawezi ku-*perform*. Mhe. Spika, nataka kuwahakikishia wenzangu kwamba *GSO* wanafanyakazi na tuwape mashirikiano katika Wizara zetu. *(Makofi)*

Suala jengine kuhusu wizara yangu ni vitambulisho, hili takribani Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumza. Mhe. Spika, suala la vitambulisho nakiri kwamba kwa baadhi ya sehemu kuna matatizo, lakini sera tuliipitisha na tulifanyiwa semina na Sera ya Vitambulisho tuliipitisha, mwanzo ilikuja sheria na baadaye ikaja sheria nyengine, sasa ya mwisho sheria iliyokuja ni *Registration of Zanzibaris Resident Act No.* 7 ya mwaka 2005 na hii tuliipitisha Barazani hapa.

Mhe. Spika, ninachoomba Waheshimiwa Wajumbe kama tunaona kuna mapungufu, basi tulete maoni na wala hatukatai, kwa sababu tunajua matatizo yapo kwenye utekelezaji. Kwa kweli tunayo mipango mingi ambayo ni mizuri kwa nia safi kabisa, ikiwa kuna matatizo sisi kama binadamu hatukatai na tunaomba tukae, ili tuje tuitafakari na mutuletee maoni na tutayafanyiakazi na tuone vipi tutaiendeleza na wala hatutaboresha Maalim Mhe. Haroun Ali Suleiman ametukataza, lakini tutarekebisha vipi ili mambo yakae sawa. Suala hili nimeona bora nilitolee maamuzi hayo tu, kwamba kweli matatizo yapo. *(Makofi)*

Lakini tulichogundua ambacho ni kikubwa na utafiti huu umefanywa na wenyewe wa Idara ya Usajili wa Kadi za Utambulisho. Mhe. Spika, wanasema kwamba tatizo kubwa linatokezea watu wanapohama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, yaani kule wanakotoka huwa hawachukui barua kutoka kwa Sheha, sasa kule anakokwenda anataka apate utambulisho na Sheha anasema sikujui na matatizo mengi yanakuja hapo.

Mhe. Spika, haya ndiyo tuliyopewa *input* kutokana na utafiti wao watu wa Idara ya Usajili wa Kadi za Utambulisho. Lakini ninachosema ni kwamba haya yanazungumzika, tukae, tutafakari na tuone matatizo yako wapi na tutarekebisha, kwa sababu hatutaki na ni sheria kila mtu apate kitambulisho.

Mhe. Spika naomba kunukuu kwenye Sera ya Vitambulisho “ni dhahiri kwamba Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni nyenzo muhimu katika kukabiliana na changamoto za kiusalama, kiuchumi, kisiasa na kijamii zinazoikabili Zanzibar”. Kwa hivyo, kama Katiba ilivyosema, sheria ilivyosema kila mmoja wetu lazima awe na kitambulisho na wala hazuiliwi mtu yeyote muhimu taratibu zifuatwe.

Suala jengine ambalo wizara yangu imeguswa ni kuhusu Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Mhe. Spika, naomba ninukuu Katiba kidogo kwenye kifungu cha 61(1) na (2).

Katiba ya Zanzibar kifungu 61(1) na (2) vinaeleza hivi:-

(1) "Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa katika kila Mkoa wa Zanzibar ataeteuliwa na Rais.

(2) Kutakuwa na Mkuu wa Wilaya katika kila Wilaya ya Zanzibar ataeteuliwa na Rais".

Mhe. Spika, naomba kuwauliza wenzangu hivi sasa upo Mkoa au Wilaya ambayo haina kiongozi na hili ni suala la msingi, kila mkoa yupo Mkuu wa Mkoa na kila wilaya yupo Mkuu wa Wilaya labda Mkoa wa Kusini bahati mbaya mwenzetu Mustafa Mohammed Ibrahim amepata maradhi na Mwenyezi Mungu amsaidie apone upesi, lakini yupo Kaimu Mkuu wa Mkoa, hili ndilo suala la msingi. *(Makofi)*

Kwa kweli hakuna mahala ambapo hapana Mkuu wa Mkoa sasa tunapomshindikiza Mhe. Rais ateue Wakuu wa Mikoa ah! Hawa waliopo je si wapo. Sasa kumuajiri Mkuu wa Mkoa na kumfuta kazi Mkuu wa Mkoa hiyo ni kazi ya Rais Kikatiba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niseme huko nyuma sote tunakumbuka kwamba Wakuu wa Mikoa walikuwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, lakini kutokana na marekebisho ya Katiba haya ya mwaka 1984 Toleo la 2010 tulisema wao wasiwe Waheshimiwa na badala yake wawe watendaji, sasa wameachwa na wao ni watendaji.

Lakini sababu moja wapo kubwa inayomfanya Mhe. Rais asubiri kwanza na atafakari kuna mambo mengi huku mikoani. Kwa mfano, kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Mhe. Mkuu wa Mkoa kwa nafasi yake ni mjumbe wa kamati, kuna wenyeviti wa CCM wa Chama Tawala, lakini sasa tunayo Serikali ya Umoja wa Kitaifa, sasa *composition* ya Kamati ya Ulinzi na Usalama iweje na hili ni moja tu ambalo nimelisema.

Kwa hivyo, kuna mambo ambayo lazima Rais atafakari ayafanyie kazi na kuteua ni mara moja tu, kama vile leo nitamtangaza fulani bin fulani Mkuu wa Mkoa mwengine na huyu ninamuondoa, lakini je tumeshayaweka sawa haya.

Mhe. Spika, kubwa jengine ni hivi juzi tu serikali tayari imeshaipitisha Sera ya Tawala za Mikoa hili nalo litatuathiri sana je, Wakuu wa Mikoa walivyo na Mikoa yetu ilivyo iendelee kuwa ilivyo, wilaya zetu bado ziendelee kama zilivyo.

Sasa kwenye *administration* hiyo ya Sera za Tawala za Mikoa, moja kubwa ya mipaka yetu ya mikoa na wilaya itapimwa upya kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hilo ni sharti moja kubwa sana na hiyo kazi inafanywa. Kwa maana hiyo, haya mambo mengi na yote Mhe. Rais ndiyo yanamsaidia kufikia hiyo *conclusion* na sio kwamba tumshindikize ateue na hivi sasa wapo na wanafanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilikuwa na hayo matatu na la mwisho kabisa kuhusu suala la usafi na utunzaji wa mazingira, Waheshimiwa Wajumbe wengi walizungumza kama vile sokoni pale pananuka, pachafu. Kwa kweli tunajitahidi na niliwahi kusema siku moja tu pale ya Mungu kama hapakufyagiliwa pale Darajani basi ni hatari na wala hapapitiki. *(Makofi)*

Lakini tunakubali kwamba nyenzo pamoja na uwezo wetu ni mdogo na hivi sasa tunajipanga upya Baraza la Manispaa, Halmashauri. Vile vile tunashukuru kwamba kuna miradi ambayo tayari imeshajitokeza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuna mradi mmoja bado haujafanyiwa kazi, namhakikishia kwamba utafanyiwa kazi, lakini kama mradi basi lazima kidogo hatua za uchambuzi ni vyema kushughulikiwa. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi litashughulikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema ndugu zangu wale ambao wanasema muungano basi, mimi nasema laa. Kwa kweli Jimbo langu Mhe. Spika, yaani wananchi wangu wengi sana maisha yao wanategemea uvuvi *at lay men's approach* wanategemea uvuvi. Mhe. Spika, uvuvi wao ni Ununio, Msasani, Kunduchi na hizo ndio bandari zao za kazi. *(Makofi)*

Sasa leo tukiuvunja muungano itakuwa tuna-*operate* kama Zanzibar na Mauritius, Zanzibar na Seychelles, Zanzibar na Comoro tena tutafute *Passport* na mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nasema kwa muungano bado tuendelee na muungano wetu na matatizo nakiri yapo mimi kama waziri nimeshashiriki vikao vingi kabisa vya kuzunzumzia makero ya muungano, tutashirikiana na wenzetu na sote humu *backbenchers* pamoja na mawaziri pamoja na wengine tupigane kwa ajili ya kuondoa kero za muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono *budget speech* na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi adhimu sana kwa ajili ya kuchangia Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Lakini kabla sijasahau naomba nitamke rasmi kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, jambo la pili naomba tuangalie ukurasa wa 7 na 8 wa kitabu cha bajeti unaozungumzia kuhusu mwelekeo wa bajeti yetu. Mwelekeo wa bajeti yetu una ishara muhimu sana zinazotoa dalili kwamba uchumi wetu unakua na nitazielezea.

Ishara ya kwanza ni mpangilio wa bajeti yenyewe kati ya fedha za matumzi ya kawaida na zile za maendeleo. Kwa nchi inayoendelea kama yetu ya Zanzibar, bajeti yake huwa namna kama hivi ilivyopangwa na Mhe. *Professor* Omar Yussuf Mzee, yaani ameipanga kwa mwaka wa pili au wa tatu mfululizo kwamba fedha za maendeleo zinakuwa nyingi zaidi kuliko fedha za matumizi ya kawaida.

Kwa mfano, mwaka juzi ilikuwa hivyo, mwaka jana pia pamoja na mwaka huu kwa bahati nzuri amepanga hivyo, nadhani mpaka tumeridhika kwamba tumepiga hatua nzuri ya maendeleo. Mhe. Spika, vyenginevyo mimi nampongeza na ninamuomba sana asibadilishe utaratibu huu, ili atupe nafasi ya kuendeleza *program* zetu za maendeleo pamoja na miradi ya maendeleo kwa sababu hiyo ndiyo inayotoa kigezo kizuri kwamba tunakua kiuchumi au hatukui kiuchumi. Kwa hivyo, utaratibu alioupanga ni dalili kwamba uchumi wetu unakua.

Pili nilikuwa nikizungumza na mtaalamu mmoja siku moja kwa ajili ya kunipa tasfiri ya *GDP* kwamba ni kigezo cha kukua au kushuka kwa uchumi, pia anipe utaratibu wa kisasa unaochukulia *Human Development Index*, yaani alininganishie vitu hivi viwili, ili nipate na mimi kuelimika ni kipi bora au kizuri cha kutumia. Mhe. Spika, aliniambia ukitaka kujua kwamba uchumi unakua au umeshuku, basi kigezo cha *Human Development Index* ni kigezo kizuri sana cha kuonesha kwamba uchumi unakua au umeshuka. *(Makofi)*

Vile vile aliniambia kwamba kigezo hiki unakiangalia au unakipima jinsi barabara zetu zilivyojengwa, madaraja yetu yalivyoendelea kujengwa, hospitali zetu zilivyohudumiwa na kutoa huduma na kujengwa na kutiliwa zana zinazofaa, skuli zetu, maji safi na salama yanavyopatikana, umeme na kadhalika.

Mhe. Spika, aliniambia vitu hivi ukivipima vipo au havipo, vinaendelea au haviendelei, basi utapata kujua tena kwa ushahidi kwamba uchumi wetu unaendelea au unashuka na namsadiki na nimemsadiki, kwa sababu huyu naye alikuwa ni *Professor* katika masuala ya uchumi.

Tukiangalia unaposema unataka kuona kitu gani cha dalili kwamba uchumi wetu unakua. Tufanye ulinganisho kati ya miaka 10 iliyopita na sasa tuangalie barabara zetu zinajengwa hazijengwi, zinafika mjini hazifiki, zinafika vijijini hazifiki, zinaenea au hazienei. Utakuta kwamba hali ni tofauti, hali ya miaka kumi iliyopita na hali ya sasa ni tofauti. Hali ya sasa ni nzuri labda mara sita hata kuliko hali ya zamani.

Leo ondoka Makunduchi saa 6 mchana kwa muda wa masaa matatu kwa *very conservative estimates* kwa muda wa masaa 3 utafika Nungwi kutoka kusini kwenda kaskazini, bila ya kupata pancha njiani bila ya kupata kugoma gari yako na kadhalika. Kwa sababu barabara ni nzuri. Yakitokea hayo ni bahati mbaya ya gari kukataa, mafuta kwisha. Lakini kama kila kitu kimekaa sawa unakwenda *non stop* kutoka Makunduchi mpaka Nungwi bila ya matatizo.
Sasa hayo ni maendeleo yanayoonekana wazi wazi ni maendeleo yaliyotumia fedha sio chengine, ziwe za mkopo, ziwe za SMZ, ziwe za kugaiwa lakini ni fedha zimetumika katika nchi na hiyo ndiyo *development index*.

Jambo la pili Mheshimiwa la kipimo cha maendeleo maana miongoni mwetu Waziri amesema tunaendelea, fedha zetu ni nyingi zimekuwa, kipimo chetu cha maendeleo kimekuwa, lakini mbona hatuvioni? Mbona hatufaidiki? Nitaelezea namna ya kufaidika, tunakofaidika ukiacha hii tofauti iliyokuwepo sasa ya kutembea msitu na nyika kutoka Kusini/ Kaskazini, Mashariki/Magharibi kwa gari ya matatizo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, amenifurahisha sana leo alipochangia, alizungumza katika vitu vinavyosaidia uchumi kukua au kutokua ni utalii, biashara na mambo haya ya miundombinu na huduma za jamii. Akatoa mfano ule anaoujua yeye zaidi wa biashara. Akatwambia ukitaka kujua wananchi wamefaidika vipi katika biashara angalia tofauti ya biashara ilivyo sasa na jinsi ilivyokuwa na ulinganishe na miaka 2, 3 au 5 iliyopita.

Kwa mfano katika mwaka jana na mwaka huu ule urari wa biashara kati ya Zanzibar na Bara umepungua sana. Miaka 2, 3 iliyopita, tulikuwa tunazungumza tofauti kubwa sana kati ya Zanzibar na Bara kiasi ambacho biashara iliyotoka Zanziba kwenda Tanzania ilikuwa ni shilingi bilioni 2.2. Lakini iliyotoka Bara kuja Zanzibar ni shilingi bilioni 23.3 ni tofauti kubwa sana.

Kati ya mambo yaliyotukwamisha ni yale ambayo tunayazungumza sana. Muungano una matatizo na unafaa tuyakalie kitako tuyatatue. Tunajitahidi kuyakalia kitako lakini bado. Kwa mfano hivi karibuni tulikuwa tunapiga kelele ya *double taxation* kati ya Zanzibar na Bara tulilizungumza sana. Limetatuka kwa kiasi kikubwa, sasa tumerudi kwenye biashara ilikuwa 23 bilioni sasa tuko katika bilioni 2.2. Katika biashara inayotoka Zanzibar kwenda Bara ni shilingi bilioni 71.3 inayotoka Bara kuja Zanzibar ni shilingi bilioni 74.7. Bado ipo *difference* ndogo ya shilingi labda bilioni 2 au 3. Hiyo kwa Rehema ya Mwenyezi Mungu na juhudi zetu sisi wenyewe tutaiondosha. Tunapotoka ni mbali sana, tumejitahidi mpaka tumefika hapa tulipofika. Urari wa biashara sasa hivi umepungua sana.

Mhe. Spika, leo vijana wetu Wazanzibari wetu wamechangamka wanakwenda nje ya nchi, wananunua magari, saruji na vifaa vyengine wanakuja kuviuza Zanzibar na Tanzania Bara ndiko kwenye soko na gari zetu zinakwenda huko *without double taxations* tunapata faida na wananchi wetu wanafaidika.

Kama tunazungumza suala la ajira, mara nyingi tunasikia viongozi wetu na hususan Rais wetu anazungumzia ajira. Ajira maana yake sio lazima serikali ikuajiri, tafuta mbinu za kujiajiri wewe mwenyewe. Tafuta namna uwe na uwezo wa kufanya mbinu mpaka ukajiajiri ilimradi ukapata mapato ya halali. Leo vijana wadogo sana akina mama kwa majina nawajuwa wanakwenda Dubai kila kukicha wanakuja na gari wanaziuza.

Tuziangalie barabarani gereji ngapi zipo zimeongezeka za kuuza magari, kila unapopita kuna gereji za kuuza magari. Hiyo ndiyo biashara ilivyokuwa. Biashara ikikuwa kwa mujibu wa nchi kama yetu ya kisiwa ndio maendeleo yanapatikana. Tukitaka kuyaangalia maendeleo kwa vitendo ni haya, vijana wetu wanapata pesa, wanapata mapato ya kujiendeleza na kadhalika.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amesema kwamba biashara inakuwa. Na ni kweli sana, inakuwa kweli kweli, tuangalie vipimo vya miaka mitatu iliyopita za uzalishaji wa zao la karafuu, uchumaji wa karafuu na uuzaji wa karafuu nchi za nje. Tuangalie karafuu zilizochumwa Zanzibar Pemba na Unguja bahati nzuri hazikuvuja kwa sababu bei ya kuuza ilikuwa ni nzuri, na bei ya kuchuma nayo ikawa nzuri. Anayechuma ni nani? Ni mwananchi. Anayeuza ni nani? Ni mwananchi. Faida inakwenda wapi? Inakwena kwa mwananchi.

Mhe. Spika, mwaka wa 2011 kwa mfano karafuu zilizouzwa baada ya kuchumwa, serikali ikawapa pesa wananchi walioziuza, serikali ikazinunua ni shilingi bilioni 50. Unaponiuliza uchumi umekuwa mbona wananchi hawapati pesa, pesa hatuzioni. Si ndio hizi. Ni dhahiri Mheshimiwa pia maeneo ya Mkoani, maeneo ya Wete, pita maeneo ya Donge, Bumbwini na kadhalika kunakozalisha karafuu.

Mhe. Spika, hii miradi yetu ya kujenga barabara inazidi kuleta *multi effects* kwa wananchi kutumia fedha zao vizuri na kujenga nyumba nzuri. Kama unataka tuangalie namna uchumi ulivyokuwa na tuuangalie.

Mhe. Spika, nisengemtendea vyema Profesa wangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, kama sikuishukuru na kuipongeza bajeti yake. Kwa namna bajeti hii ilivyotizama mahitaji ya Wizara yangu mpya ya elimu. Katika changamoto mbili nilizonazo na nimeanza kuzifanyia kazi na naahidi nitazifanyia kazi. Ukiacha matatizo ya watoto wengi kufeli na kufutiwa mitihani yao. Maana hiyo ni changamoto kubwa na nimeanza kuifanyia kazi, nimeanza kuzungumza na walimu wakuu na kadhalika. Kwa sababu wenye makosa haya si wanafunzi peke yao, sio walimu peke yao, sio wizara peke yake, ni mchanganyiko. Tunafanya kazi kwa nguvu zetu na hatimaye tutaweza kutafuta dawa ya kuondosha aibu hii.

Mhe. Waziri huyu ameniongezea katika bajeti yangu shilingi bilioni 8 kutoka bilioni 4 za mwaka jana kuja biloni 8 za mwaka huu. Huo ni mchupo wa asilimia 100, hapa sina sababu ya kutomuahidi yeye na Baraza hili kwamba hakutatokea mwanafunzi yeyote amaestahiki kwenda Chuo Kikuu na hususan Chuo Kikuu cha Tanzania akakosa mkopo. Tunaanza kupokea maombi, tunayafanyia kazi na fedha hizi zitatutosha kwa mwaka

huu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wetu. Tukija tukiambiwa mikopo haipo haikupatikana sasa tena hapo nihukumuni. Msinihukumu leo, maana fedha bado hazijatoka, zitatoka lakini. Zikitoka majina tuna- *compare* tunafanya vitambulisho vyote, tunawapembua wakopaji, tutatoa mikopo kwa kila mwanafunzi anayetaka kusoma Chuo Kikuu, iwe diploma iwe shahada tutampa mkopo.

Pia amezungumzia kuhusu kodi. Hili limezungumzwa sana na wachangiaji kwamba tumetoza kodi nyingi, tunawabana wananchi. Lakini Mheshimiwa alipokuwa akisoma bajeti alisema tutatoza kodi ya Bandari kiasi kadha, pasenteji kadha lakini fedha hizi zinakwenda katika kununua madeski. Kama kuna mchango mkubwa serikali yangu imeutoa kwa wizara hii ni mchango huu wa kuwapatia wanafunzi mikopo na kuwapatia vikalio wanafunzi wote. Ishaallah tutajitahidi tuwezavyo kuhakikisha kwamba haya mambo mawili yanapatikana sambamba.

Mheshimiwa miaka 3, 2, 1, uliopita tumejenga skuli mpya 13 za kisasa kabisa, tena tumezijenga vijijini Pemba na Unguja. Hivi karibuni skuli hizi zimeshamalizika, tunazikamilishia madeski na vitu vyengine, zenye nyumba tumeshamaliza nyumba, fanicha na kila kitu, punde si punde tutazifungua. Tumewapanga watu mashuhuri mbali mbali watakaokuwa wageni rasmi kwa kuzifungua skuli hizi akiwemo Spika wetu mpendwa wa Baraza la Wawakilishi.

Kama tutakupa ya Kibuteni au ya Donge, kamati ndiyo itakayoamua lakini umo katika watakaofungua skuli hizo. Hii *Alhamdulillah* ni neema, na skuli nyengine nane tunazijenga za kileo za kisasa, ilimradi miaka mitatu minne ijayo tuepukane na tatizo la darasa moja kuwa na wanafunzi 100, 80, 90, ili katika hizo mbinu za kuhakikisha watoto wetu wanapasi moja ni hii ya kuwapatia vikalio, skuli za kisasa na walimu wa sayansi. Napata malalamiko ya hapa na pale kwamba skuli yangu kadhaa ipo Kibuteni, Jambiani, uko wapi haina walimu wa sayansi.

Mhe. Spika, juzi tumeajiri walimu 111 wa sayansi. Tukimaliza kuajiri wa sayansi tukimaliza wa diploma, tukimaliza wa digirii na wale walimu wa *Arts* nao tutawaangalia. Lakini maamuzi ya Wizara hii, maamuzi ya sera yetu, maamuzi ya serikali yetu, kuweka mkazo katika masomo ya sayansi tupate walimu wazuri wa sayansi tuwapeleke katika skuli zetu. Hivyo Mheshimiwa ndivyo tulivyojipanga, kutekeleza agizo hilo la serikali.

Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na nasema nimezungumza na wananchi wangu wa Donge katika suala hili la bajeti hii, wameniagiza nitamke na wananisikia niunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya serikali, hotuba ambayo iliwasilishwa juzi na Swahibu yangu mkubwa Alhaj Omar, Yussuf Mzee. Nimpongeze kwa hotuba yake na bajeti yake. Pamoja na pongezi hizi naomba vile vile niwapongeze wafanyakazi wake katika Wizara hii kwa namna walivyomsaidia hadi leo kupata pongezi zote kwa kila anayesimama hapa.

Mhe. Spika, vile vile niwashukuru sana wajumbe wote wa Baraza lako tukufu ambao wamechangia bajeti hii ya serikali na wakagusa katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Mimi na Naibu wangu Waziri tumekuwa makini sana kusikiliza michango yao. Leo kwa sababu ya wakati tutafafanua baadhi ya mambo ambayo yameelezwa hapa. Ni imani yangu kwa sababu iko bajeti ya wizara hii basi mengi zaidi tutafafanua siku hiyo. Kwa hili naomba radhi sana inawezekana wote tusiwaguse lakini tutachukua yale maeneo ambayo ni vizuri leo kuguswa.

Mhe. Spika, zabuni za ujenzi wa barabara na miundombinu kwamba hawapewi wakandarasi wa kienyeji. Zabuni zote za ujenzi wa barabara na kwa sababu nyingi ni za kimataifa huwa ni za *International Tender* zinaendeshwa kwa mujibu wa masharti ya msaada tulioupata, uwe ni mkopo au ni msaada. Lakini kabisa kabisa hakatazwi *contractor* wa kienyeji kuungana na *contractor* wa kigeni. Natoa wito rasmi na kwa bahati nzuri sasa hivi tumeanza utaratibu kwamba moja katika masharti ambayo tumewaambia wenzetu watukubalie ni kusema kwamba, kila anaeomba kazi basi ashirikiane na *contractor* wa kienyeji. Kwa hivyo fursa hiyo ipo sasa.

Wakandarasi wote wa kienyeji ni vizuri wawasiliane na wakandarasi wanaoomba kazi hizi, ili na wao wawe ni miongoni mwa washiriki katika ujenzi wa barabara hizi. Faida ipo kubwa kuna *technological transfer* watapata ujuzi. Lakini si lazima na wewe uwe na hadi na *cla*ss kama ya *contractor* wa kigeni, hata kama ni *contractor* wa *class one, two, three, four, five,* kuna kazi ndogo ndogo utapewa ufanye, kuanzia sasa ni vyema kabisa.

Mhe. Spika, tumeanza na mradi huu wa *Airport Ground handling*, ambao nao nitausemea baadaye. Tumetoa *tender* kama serikali ilivyoagiza na tumeweka sharti kwamba yoyote ambaye ataomba tenda hii awe ameshirikiana na Kampuni ya kienyeji, kwa hivyo fursa ipo.

Mhe. Spika, ucheleweshwaji wa barabara au miradi ya barabara hasa inayojengwa na MECCO. Nakiri kwamba kweli baadhi ya miradi yetu imechelewa sana, lakini haikuchelewe tu kwa sababu ya kuchelewa. Zipo sababu za msingi na zisizokuwa za msingi. Lakini mimi nataka kuzungumzia sababu za msingi.

Kwanza kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi mwenyewe. Kuna wakandarasi katika kufanya kazi hizi ili wawahi muda basi wameweza kutumia fedha zao kabisa. Ucheleweshaji unakuja kwamba mkandarasi anafanya kazi, *certificate* ya malipo inatayarishwa, inaidhinishwa, lakini mlipaji anachukua muda mrefu. Hiyo nasema ni sababu ya malipo. Zipo na sababu nyengine vile vile za maumbile kama mvua. Hivi juzi *contractor* anayejenga barabara chini ya msaada wa MCC alikaa mwezi mzima hayupo kwenye s*ite*, mabuldoza yamekwama kwenye tope. Huu ungetarajia kuwa aendelee mwezi mzima na kufanya kazi, kazi ya barabara ni tope, vumbi na vitu kama hivyo.

Kwa hivyo mimi nasema zipo sababu za msingi na zile ambazo si za msingi tunakabiliana nazo, tunafanya vikao mara kwa mara. Imani yangu kwamba kwa sababu tunafanya vikao vingi na vyengine hata vya kutishia kusimamisha mradi. Tunafika mahali kwamba basi wacha tuendelee kwa sababu tunaona hasara ya kusimamisha mradi ni kubwa zaidi kuliko kuvumilia mpaka barabara yetu ikamalizika.

Malipo haya si kwa Kampuni au kwa Benki zinazotukopesha tu, lakini hata kwa serikali. Kwa sababu serikali hii inaendeshwa kwa kodi mpaka Waziri wa Fedha anayeshughulikia mambo ya Fedha akusanye, kipatikane na kikipatikana hawapewi miundo mbinu peke yao, tunajikuna tujipatapo. Nashauri kabisa na nakubali kwamba barabara zinachelewa lakini tuna sababu za msingi.

Mhe. Spika, sababu za kusita kwa ujenzi wa jengo la abiria la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kwa jina maarufu *Terminal Two*, ujenzi umesita takriban sasa ni miezi mitatu. Sababu za kusita kwa ujenzi ule zipo na ni za msingi na Serikali Kuu wanajua kabisa sababu hizi zikoje. Ujenzi wa jengo lile ni *system* moja ambayo inaitwa (*design and build)* unasanifu na unajenga.

Mhe. Spika, wakati ujenzi huu unaendelea serikali ikaona kwamba kuna mabadiliko makubwa tufanye ili jengo letu likimalizika liwe la aina yake. Lazima kuwe na mapitio, hichi kitoke hapa kikae hapa, hichi tunataka kiongezwe. Sasa mapitio hayo yanakwenda ku-*design*, *negotiation*, *costing* mpaka mnakubaliana. Tumewambia kabisa kwamba msifanye hili mpaka hili tukubaliane. Kwa hivyo si sababu tu kwamba imesimamishwa. Maana maneno yapo mengi lakini ukweli ni huu.

Jengine sio hilo nikiri kwamba kulikuwa na kasoro katika mikataba. Hizi zinazotumika ni fedha za wananchi, ni mkopo lakini ni wananchi wenyewe wa Zanzibar watakaolipia mkopo ule. Lakini uwe na sababu za msingi ukija ukiwa *audited* uwe na ushahidi kwamba liko hivi, liko hivi, liko hivi. Hapo ndipo serikali inapopata *credits*. Kwa hivyo kasoro zile zimechukua muda kidogo mpaka tumekubaliana.

Nataka nitoe taarifa rasmi kwamba tumekubaliana vizuri, mikataba imewekwa vizuri, serikali ipo *very safe* na hata mkandarasi yupo *very safe*. Kwa sababu hiyo basi wakati wowote ujenzi utaendelea kama ulivyokuwa unaendelea.

Mhe. Spika, suala la *ZAT* katika Airport yetu. Wajumbe wamechangia vizuri lakini kinachonisikitisha ni kwamba hawana habari za kutosha. Sasa kama huna habari za kutosha unaweza ukasema vitu kumbe ni tofauti na vilivyo. *ZAT* alikuwa na mkataba wa miaka 30 kutoa huduma za kuteremsha na kupakia na kucheki tiketi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, kutoka mwaka 1995 mpaka mwaka 2025 ni yeye tu. Kukawa na malalamiko mengi na nyie mnajua, watu wanaotoa kodi yao ya Kiwanja cha Ndege wanataka huduma nzuri. Ni nani anafurahi kumuona mtalii amebeba begi kutoka kwenye ndege kama si *hand luggage*, nani anafurahi kuona ndege imeharibika lakini haiwezi kuondoka mpaka iletwe ndege nyengine kwa sababu hakuna vifaa kwa ufupi kulikuwa na mapungufu makubwa serikali ikaona hapana moja katika mapato ya serikali inatoka viwanja vya ndege.

Kuna siku pale wanakuja abiria mpaka mia nane wanalipa ada ya kiwanja, wanalipa viza sasa mapungufu haya yanaweza kabisa kabisa yakachangia ndege zikakataa kuja kwa sababu ya huduma dhaifu serikali ikasema kwamba kwa sababu hii ni airport ya kimataifa basi tufanye marekebisho, kwa hivyo waheshimiwa wajumbe katika marekebisho haya ambayo serikali wanataka kufanya, kwanza wamesema ZAT ni muekezaji mzalendo

kwa hivyo yeye hataondoshwa, lakini lazima tupate Kampuni nyengine ije ifanye kazi basi itakuwa kuna ushindani. Sasa kama atakuwa *ZAT* ana nguvu zaidi na ufanisi zaidi basi kampuni nyengine haitapata kazi.

Lakini Mheshimiwa mmoja alikuwa anachangia ametaja kampuni moja ya Swiss Port. Mhe. Spika, makampuni ambayo yameomba kupewa kazi ya ground handling kama kampuni ya pili na ambayo kuna masharti kwamba lazima kuwe na *local company* inayoshirikiana nayo. Moja ni *Swiss Port* wapo watano, unaposema huyu hatumtaki mimi ninafikiri si sahihi kwa sababu tenda ni za kimataifa zitafanyiwa na tathmini na timu ambayo inakubalika na wakandarasi na kwa sababu mkandarasi yule yumo, ikitokea kwamba amekosa anaweza kukosa hayuko peke yake sisi wajumbe wa Baraza hili inawezekana kabisa kabisa tukaonyeshwa kidole nimekosa hata pengine hana sifa, nimekosa kwa sababu Baraza la Wawakilishi limesema hivi, hamkatazwi kusema lakini ni vizuri waheshimiwa, katika kusema tuwe na hadhari ya kusema.

Kwa nini tufanye maamuzi ambayo baadae tunaonyeshwa vidole na sisi tumeaminiwa, tumeambiwa tuje hapa tuwatumikie watu, lakini tusisahau kwamba vile vile serikali yenyewe kama muhimili mwengine wa kwanza wa pili au wa tatu basi nayo ina majukumu yake, hili mimi ninashauri wenzangu kwamba kama ambavyo hatuwezi kujadili jambo ambalo liko kwenye mahkama hii ninayoizungumza haliko katika mahkama lakini halina tofauti kubwa na mwisho tunalolitaka kwamba Baraza la Wawakilishi likisema jambo ninaweza nikasema ni kama mfano Baraza likishasema jambo ndio basi, kumbe sisi hapa hatufanyi maamuzi hasa katika masuala ambayo yapo katika mkondo mwengine. Kwa hivyo Mhe. Spika, ningeshauri sana wajumbe wenzangu tunaochaniga hapa tunachangia vizuri, hoja nzuri lakini saa nyengine kuna over do na inatupa matatizo.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji meli mpya hili limesemewa na wajumbe karibu wote. Mhe. Spika, ni bahati mbaya kwamba kila serikali wanachofanya hawaji hapa wakakieleza. Na ingekuwa kuna utaratibu huo hili suala lisingeulizwa. Mhe. Juhudi za serikali zimeanza muda mrefu hata kabla ya meli ya Spice Islander kuzama. Lakini baada ya mkasa ule serikali ikaongeza juhudi zake, tumekutana na makampuni kama serikali zaidi ya sita tumewaita kwa gharama zao wamekuja tumekaa nao kitako lakini bado masharti yamekuwa magumu kiasi ambacho tunasema aaa ngojeni kwanza. Lakini imefika mahali sasa si makampuni tu lakini hata serikali rafiki, viongozi wetu wa SMT na SMZ kila mahali wanapokwenda walikuwa wanalizungumza hili ama kwa mkopo nafuu ama kwa msaada, bado hatujafanikiwa. Lakini katika hali hii ni imani yangu kwamba si muda mrefu serikali itapata solution ya kudumu ya tatizo hili.

Kwa hivyo wajumbe ambao wamechangia hili ni imani yangu kwamba si ajabu wakati ninaposoma hotuba yangu kukaa na kauli ya kufurahisha zaidi kukaa na kauli ya kufurahisha zaidi kuliko hili. Suala kwa nini halikuingizwa kwenye bajeti Mhe. Spika, weye ni mzoefu sana wa Baraza hili yapo mambo chungunzima hayakuingingizwa kwenye bajeti na yanafanyika. Ni maamuzi ya serikali, kwa hivyo mimi naamini kwamba hata kama hesabu hayamo mule kwamba meli hii labda tuweke dola milioni moja au mbili au tatu lakini ninawaarifu wajumbe tu kwamba meli ambayo tunaihitaji na kwa sababu tumeshatafuta makampuni yote maarufu ya utengenezaji meli, China, Japan, Korea, Uturuki, South Africa na kwengineko hakuna hata meli moja katika hizo meli ambazo tuna *specification* itakaopungua dola milioni kumi na nne.

Kwa sababu dola milioni kumi na nne ni shilingi bilioni karibu ishirini na mbili ni bajeti ya wizara yangu mara tatu. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba serikali hili wameliona siku nyingi nina hakika inshaalla tuombe Mungu, wakati ninasoma bajeti yangu hapo huenda tukawa na kauli nzuri zaidi kuhusu hili.

Mhe. Spika, kuhusu mamlaka mbili moja ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege na Mamlaka ya Usafiri baharini kwamba mapato yao hayaonekani. Mhe. Spika, mamlaka hizi mbili zinakusanya fedha na fedha hii inakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mamlaka ya Usafiri Baharini imekusanya asilimia mia mbili zaidi ya makisio yaliyokisiwa kwa mwaka huu na hizo zote ziko katika mfuko wa Serikali. Kwa hivyo mamlaka hii inachangia.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nayo vile vile imechangia kwa kiasi kikubwa, na kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji sehemu kubwa ya fedha hizi zinatumika kwa viwanja vya ndege na sehemu ndogo inakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo mapato yanayokusanywa na Mamlaka hizi mbili Mheshimiwa yanaingia katika Mfuko wa Serikali na yanatumika kwa mujibu yalivyopangwa.

Mhe. Spika, la mwisho ni kuhusu *scanner* kwenye bandari ya Zanzibar. Bahati nzuri katika ziara hizi za viongozi wa serikali nchini China tulipata nafasi wenzangu ni mashahidi. Mwezi wa Februari ujumbe ulioko China ulipata nafasi ya kutembelea, kuona kiwanda kinachotengeneza *scanner* cha China na sikuona tu tumeoneshwa namna ya *scanner* ilivyo na namna inavyofanya kazi. Kabla ya kuona tulikuwa na mawazo makubwa kwamba lazima upate jengo kama hili, mahali pakubwa, nafasi kubwa kumbe maskini ni kitu

kinawekwa kwenye *mobile van* na contena inawekwa mbele yake inanyanyuliwa tu na lift, ten, fifteen minutes kazi imemalizika kila kitu kinaonekana.

Sasa sisi hatukuwa na dhana hiyo na kwa sababu dhana hiyo haipo ukweli si hivyo tulivyokuwa tunafikiria, Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha Uchumi, Mipango ya Maendeleo akaona alaa kumbu inawezekana. Kwa hivyo msaada ambao utapatikana kwa ajili ya bandari ya Zanzibar, sasa unaweza kabisa kabisa ukakubalika kwa sababu hakuna mahali pakubwa panapohitajika kwa ajili ya shughuli hizi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ni kwamba juzi Serikali ya Muungano ilitia saini mkopo wa dola milioni ishirini kutoka *BADEA* na *SAUD FUND* kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka Wete hadi Chake yenye urefu wa kilomita 22. Inshaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ikifika Oktoba tutakuwa tayari tunajua mjenzi ni nani. Lakini si hilo tu ni kwamba serikali imeridhia mkandarasi bibi Shapria kupewa kazi ya kujenga barabara inayotoka Jendele, Cheju mpaka Unguja Ukuu kae bona kilomita 11 na wakati wowote Mhe. Spika, mkandarasi huyu ataitwa kwa ajili ya kusaini mkataba aendelee na kazi.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Ole kwa heshima na taadhima tunaunga mkono bajeti hii na nawaomba wajumbe wenzangu waiunge mkono kwa sababu ni bajeti ya serikali, ndio bajeti kubwa, bila ya bajeti hii hakuna shughuli katika serikali.
Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitajitahidi nieleze kwa kifupi sana mambo ambayo waheshimiwa wajumbe wameeleza yanayogusa wizara yetu, kwa kuwa naelewa wiki ijayo tutapata nafasi nzuri ya kueleza kwa kina katika bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea na mkutano wetu huu wa bajeti. Aidha nichukuwe fursa hii kumpongeza sana sana Waziri wa Nchi, Fedha na Uchumi kwa namna ambavyo amewasilisha bajeti yake vizuri na bajeti ambayo kama ilivyoelezwa na walionitangulia kwamba imekamilika vizuri na imesikiliza kilio cha wananchi wetu, ninakushukuru sana Mhe. Waziri Ahsante sana.

Mhe. Spika, nianze kwa kuunga mkono bajeti hii naunga mkono mia kwa mia. Mhe. Spika, kubwa yaliyogusa wizara yangu yalikuwa ni mambo 4. Moja ilikuwa kero za muungano, pili ilikuwa ni suala kwa mbali la sensa, tatu ni suala la tume teule iliyoundwa ya Baraza la Wawakilishi ambayo itazungumziwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, la nne linagusa kidogo Tume hii inayosikiliza maoni kuhusu masuala ya Katiba yetu mpya.

Mhe. Spika, nianze hili la mwanzo kuhusu matatizo ya ndani ya muungano wetu. Ni kweli matatizo yapo na matatizo yetu yamechangiwa zaidi na kutokana na kucheleweshwa na majibu ya matatizo yenyewe, kupata ufumbuzi wa kero zilizojitokeza ndani ya muungano ndizo hasa Mhe. Spika, zimelalamikiwa san asana na wananchi wetu na kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Kwa hivyo licha ya mbinu mbali mbali zilizochukuliwa za kutafuta ufumbuzi wa kumaliza kero hizi, bado kumekuwa na malalamiko mengi. Kwa hivyo serikali katika kuona umuhimu wa tatizo lenyewe yanavyoathiri wananchi wetu ndio wakakubaliana na maoni ya wananchi, vyama vya siasa na wadau mbali mbali kuhusu kuanzishwa kwa mchakato wa katiba mpya ili wananchi wapate fursa kwa kina zaidi kuyaeleza matatizo yao na kutoa ushauri na mapendekezo sahihi yakayowezesha kumaliza matatizo ambayo yanatukabili.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninaamini sana kwamba utaratibu huu ambao serikali umeufikiria na kwa kauli moja ukapitishwa pale Bungeni ninaamini sana kwamba itakuwa ni moja katika njia sahihi sana ya kumaliza matatizo yetu ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, matatizo ni mengi lakini leo na hasa katika kikao hiki kubwa ambalo limezungumzwa lilikuwa ni suala la mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, juzi nilipokuwa ninajibu swali nilisema kinaga ubaga kwamba tatizo hili liko ukingoni kumalizika ufumbuzi wake umo karibu kupatikana. Hivyo ninaamini si muda mrefu tatizo hili nalo litakuwa historia. Na ninaamini linafanyika hivyo kwa sababu za msingi kabisa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa Zanzibar na kusikiliza kilio na matarajio ya wananchi wa Zanzibar kuhusu kutaka kwamba mafuta na gesi asilia yatolewe katika orodha ya mambo ya muungano.

Na kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar uamuzi huo ulikwisha fanyika na kwa kuwandikia wenzetu wa Jamhuri ya Muungano na kwa kueleza yale ambayo Baraza lako tukufu hili yameyapendekeza kutoa azimio rasmi la Baraza hili. Kwa hivyo napenda niwahakikishie waheshimiwa wajumbe kwamba tatizo hili karibu litapata ufumbuzi wa uhakika na ufumbuzi wenyewe ni kulitoa katika orodha ya mambo ya muungano.

Mhe. Spika, jengine lililozungumzwa lilihusu mchakato wa katiba, ilijitokeza dhana Mhe. Spika, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inabana watu wasitoe maoni yao. Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina nia hiyo wala haitokuwa na nia hiyo, nia ya serikali ni kutaka watu watoe maoni kinagaubaga, wayatoe kwa kina, wayaeleze, wayaseme lakini kilichosisitizwa ni kufata taratibu na sheria ziliopo.

Kwa sababu Mhe. Spika, nchi inaongozwa kwa taratibu na sheria, nchi inaongozwa kwa mipango iliyowekwa ili kuepuka vurugu. Kwa sababu Mhe. Spika, wakati huu ni kipindi cha mpito, ni wakati muhimu sana wa kuhakikisha kila mmoja wetu anafuata utaratibu tuliojiwekea wa sheria ili kuepuka mivutano.

Mhe. Spika, tutakuwa tuna hoja mbali mbali, Mhe. Mansour jana alieleza hapa kwamba kila mmoja anakuwa na maoni yake na ni vizuri maoni ya kila mmoja wetu yakasikilizwa na serikali haikatai hilo. Na wale wanaosema waachiwe wapumue tunawaachia wapumue lakini kwa kufata taratibu za sheri, utaratibu wa sheria lazima ufatwe Mhe. Spika, kwa sababu kama kila mtu atajifanya anavyotaka yeye, huyu anasema mimi nataka muungano, huyu anasema mimi sitaki muungano, huyu anafanya maandamano sitaki muungano na yule mwengine naye anayetaka muungano akafanya maandamano, je wanapokutana ipo salama hapo Mhe. Spika.

Kwa hivyo tunachokisema utaratibu wa sheria uheshimiwe sana kwenye kipindi hiki ni kipindi cha mpito, wananchi watoe maoni yao na tupo tayari kuyasikiliza. Na kwa bahati nzuri jana tumemsikia Mwenyekiti wa Tume hii ya kusikiliza maoni na leo vile vile walifanya uzinduzi kwa upande wa Zanzibar alisema watu watu wote watasikilizwa maoni yao. Wanaotaka muungano waseme, wasiotaka waseme, wenye matatizo Fulani wayaseme, kila mwenye lake aseme tena aliseme kwa shibe yake. Lakini tuheshimu taratibu na sheria.

Mhe. Spika, kuzungumzia kusema masuala ya kuondosha kero za muungano si kwenda kuvunja baa za watu ukanywa bia za watu, si kwenda kutia moto makanisa na nyumba nyengine za ibada. Tunapozungumzia mambo haya lazima tuheshimu mali za watu wengine ili mambo yetu tuyafanye kistaarabu, kivizuri yatufikishe mahala pa salama. Kwa hivyo sisi tunachokisema hapa watu wasifanye fujo, watu wasifanye vurugu watii amri halali ya serikali ili mambo yaende vizuri na nchi yetu ikae kwa salama na amani.

Mama yangu mama Asha aliyazungumza mambo haya kwa vizuri sana, raslimali kubwa ya wazanzibari Mhe. Spika, ni amani na utulivu. Ulipoondoka amani na utulivu kwa siku moja tu kila mmoja alipiga kelele Mhe. Spika. Shughuli za biashara hazifanyiki, kazi zetu za kawaida hazifanyiki, maduka yanafungwa, nyumba zimechomwa moto, gari zimechomwa moto, barabarani kumechomwa moto mapira, mawe yamewekwa ovyo, hakufanyiki shughuli yoyote. Mwenye kwenda shamba haendi shughuli yoyote ya kujipatia rizki haifanyiki.

Kwa hivyo tunachokisema tuheshimiane, tuvumialiane kila mmoja akajieleza ili tuwe na katiba nzuri yenye manufaa na nchi yetu, hilo ndio serikali inalolisema. Lakini halimkatazi mtu yoyote kutoa maoni yake.

Mhe. Spika, jengine linahusu sensa, kuna watu wamesema kutatakiwa vitambulisho, kutatakiwa ruhusa ya sheha, Mheshimiwa sensa hakuna ruhusa ya sheha, wala hakuna suala la vitambulisho. Sensa wanahesabiwa watu wote pamoja na wageni watakaokuwepo siku hiyo katika nchi yetu. Kwa hivyo suala la sensa ni jambo muhimu, lina maslahi kwa nchi yetu ili tuweze kujua watu wetu, tujuwe matatizo yao, tujuwe mahitaji yao tujuwe tuwafanyie nini kwa ajili ya maendeleo yao.

Kwa hivyo cha msingi ni kwamba watu wajitokeze na siku ile ya sensa utahesabiwa pale ulipo. Tumo humu ndani twenye nyumba nyingi nyingi hivi pala utakapowepo ndipo utapohesabiwa. Kwenye shughuli yako pengine kuna wavuvi hapo hapo ulipo utahesabiwa. Suala la msingi uhesabiwa mara moja. Kwa hivyo ninawaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili tukufu waelewe kwamba suala la sensa halitakuwa tatizo, wala halitakuwa bughudha na watakuwepo watendaji makini, madhubuti, wanaojua kazi yao na wataifanya kazi hiyo kwa umakini na uaminifu mkubwa sana.

Mhe. Spika, katika suala la Mhe. Hija alielezea kwamba yuko mtendaji wa TPDC ambaye yeye alikuwa na mambo yake kwenye mitandao. Mheshimiwa serikali hii haiendeshwi na mitandao. Serikali hii inaendeshwa na kauli thabit zinazotolewa katika Baraza lako hili tukufu. Nataka nimhakikishie Mhe. Hija, serikali zetu mbili zinazungumza jambo hili na litaendelea kulizungumza kwa kuhakikisha kwamba linapata ufumbuzi. Kama yupo mtendaji anaevunja moyo au anaharibu kwa makusudi mazungumzo yetu haya basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Kwa sababu nia na madhumuni ni kuhakikisha maslahi ya watu wetu yanalindwa na kila jambo ambalo serikali imeamua kulifanya lifanywe kwa utaratibu mzuri ili matatizo yaliyopo yaondokane. Hatuna nia ya kuongeza matatizo Mhe. Spika, nia yetu ni kuyaondoa matatizo na ikiwezekana kuyaondoa yote

haraka iwezekanavyo ili tuwe na muungano mzuri tuishi vizuri, tushirikiane vizuri, nay ale ambay yanaonekana hayafai yatolewe ili tukae kwa salama na amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naendelea tena kuunga mkono mia kwa mia hotuba hii. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Spika, kwanza baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kuendelea na shughuli hii muhimu katika Baraza hili tukufu, naomba na mimi nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hoja hii ya bajeti ya serikali.

Lakini la pili naomba na mimi pia niungane na wenzangu kumpa pongezi Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo lakini ninashukuru wenzangu wamenisaidia sababu za kumpa pongezi hizo kwa hivyo sipendi nizirejee, kwa sababu ya kuokoa muda. Lakini na mimi nitangulie kusema wazi kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mimi naomba nichangie katika maeneo manne na hili nachangia ili kumsaidia kupunguza muda ule ambao Mhe. Waziri atakuja kutoa maelezo kuhusiana na michango mbali mbali ambayo wametoa waheshimiwa wajumbe hapa.

La kwanza ni kuhusiana na kamati teule. Waheshimiwa wajumbe wengi wamehoji kwamba hakujatoka taarifa ya utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa katika kamati teule. Sababu zao za kuhoji hilo ni za msingi kwa sababu wakati mwengine kimya kinaweza kikatia shaka, labda hakuna kinachoendelea. Lakini mimi ninachoomba kuwatoa wasiwasi tu ni kwamba kimya hiki ni kwamba kina mshindo mkubwa lakini utakapofika wakati wake.

Naomba niwakumbushe kwamba kamati teule iliundwa tarehe 9/8/2011 na ikawasilisha ripoti yake tarehe 20/4/2012 yaani baada ya miezi minane. Tokea tarehe 20 April mpaka leo tarehe 20 Juni ni miezi miwili. Na naomba niwakumbushe kwamba katika kamati teule ilikuwa na hadidu rejea 9 na ilipoleta mapendekezo lileta mapendekezo 56 ambayo unaweza ukayagawa katika sehemu 7. Na mengi katika mapendekezo haya ni ya kuchukua hatua za kurekebisha zikiwemo, taratibu za kiserikali kurekebisha sheria, lakini na pia kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale ambao wamehusika au Kamati Teule iliona kwamba wamehusika kwa namna moja au nyengine na makosa mbali mbali.

Lakini pia naomba niwakumbushe wenzangu kwamba katika hii Ripoti ya Kamati Teule ilisema kuwa kuna baadhi ya mambo yafanyike ndani ya miezi mitatu, ilisema wazi hasa kwamba jambo hili lifanyike ndani ya miezi mitatu leo tuna miezi miwili. Lakini la msingi lililosema Azimio la Baraza ni kwamba, serikali ilete taarifa ya utekelezaji na bahati nzuri Mhe. Spika, Kanuni zetu tumezirekebisha tumeweka kifungu cha 44 fasili ya nne imeweka wazi kwamba taarifa hiyo itakapoletwa Waheshimiwa Wajumbe watakuwa na fursa ya kuichangia.

Sasa katika hili mimi labda niseme mambo matatu, la kwanza nianze na ile kauli ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule, Mhe. Omar Ali Shehe, alipokuwa anamalizia kuwasilisha ripoti hii alitoa maneno ambayo yalionesha kuwa ni mtu muungwana mno, alisema kwamba hii ripoti imetayarishwa na binadamu na mwenyewe katika uungwana wake alisema na binadamu wenyewe ni akina Omar Ali Shehe, inawezekana ikawa na mapungufu. Nadhani sina haja ya ku-*quote hansard* kwa sababu hayo maneno aliyoyatoa ni ya kiungwana mno naamini kila mtu atakuwa anayakumbuka humu ndani.

Indhari hiyo sasa aliyotupa ilikuwa ni ya msingi, kama serikali unapoifanyia kazi hayo lazima uyazingatie. Kwa sababu hii ripoti imependekeza kuchukua hatua za kinidhamu na hayo yana taratibu zake vile vile na katika kufuata hizo taratibu uzuri wake kwamba Kamati Teule yenyewe miongoni mwa mambo ambayo ililaumu sana ni kutokufuatwa utaratibu, sasa unapokuja kuchukua hatua bila ya kufuata utaratibu Mhe. Spika, itakuwa ni ile hadithi ya Kobe kumcheka Kasa. Kwa sababu Kobe alimcheka Kasa kuwa gamba lake limepasuka pasuka sasa ukitizama na yeye mwenyewe sijui yuko vipi. Hilo ni lazima tulizingatie kwa sababu baadae tunarudi hapa hapa aliyekosewa kimbilio lake ni kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Makame Mshimba juzi alipata *promotion* akawa mwanasheria mkubwa, alikuwa mwanasheria mdogo sasa mwanasheria mkubwa maana aliweza kutetea kesi tatu katika kikao kimoja jambo ambalo kwa wanasheria wa kawaida linawashinda. Lakini yeye ni mmoja ambaye ana kesi zake hapa za kwamba watu wamechukuliwa hatua taratibu hazikufuatwa na hapa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na nani sijui wote taabani kwa hoja hizo za Mhe. Makame Mshimba. Sasa hilo ni lazima Waheshimiwa tulizingatie.

Lakini kuna mambo ya kufuata utaratibu na pia lakini tutakapotekeleza haya jambo la tatu ni kwamba tunatakiwa tuje tulete taarifa, taarifa hii sidhani kama Waheshimiwa walikusudia tukishakufanya moja tukimbilie hapa tuseme hili tushalifanya, tukifanya la pili jamani na hili tayari tumelifanya. Ninachoweza kuwahakikishia ni kwamba serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kushughulikia ripoti hii kwa dhati kabisa, kwa makini na itakapokuja taarifa basi hizo hatua zote ambazo zimependekezwa zitaonekana hatua ambazo zimechukuliwa.

Mimi naomba Waheshimiwa kwenye hili watufahamu kama nilivyosema wamechukua miezi minane kuiandaa, wakajifungia sijui mara ngapi kutayarisha ripoti kuiandika, sasa naomba watuamini na tunaposema serikali Waheshimiwa ukiachia na humu tuliomo ndani na viongozi wetu wengine ambao hawamo humu wawili Mhe. Rais mwenyewe na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ni sehemu ya serikali na haya yanapofanyiwa maamuzi na wao wanakuwemo. Sasa sidhani kwa viongozi wetu tulioano kama kuna mtu ataona muhali kuchukua hatua kwa sababu ama mtu ni jamaa yake, ama ndugu yake, mimi naamini na wao ni waumini wa Kanuni ile ya Mhe. Hija Hassan pengine kuliko yeye mwenyewe Mhe. Hija.

Kwa hivyo, hili naomba watuamini, naomba watupe muda linafanyiwa kazi haina haja ya kusema kwamba hatupitishi bajeti hii kwa sababu ya Ripoti ya Kamati Teule inafanyiwa kazi kama ilivyoelekezwa.

Jambo jengine ni dogo ambalo nashukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifafanua kuhusiana na uteuzi wa Wakuu wa Mikoa.

Mhe. Spika, katika hili nadhani majibu yake yako wazi, yako rahisi katika Katiba kifungu cha 54 pia kifungu cha 61. Mkuu wa Mkoa baada ya kuteuliwa Katiba inavyoelekeza ataondoka katika wadhifa wake kama Rais ataamua kumuondoa katika wadhifa wake, vyenginevyo kwa kubadilika Rais yeye habadiliki anaendelea na cheo chake mpaka atakapoteuliwa, kama atabadilishwa, kama atawekwa Mkoa mwengine hilo ni suala jengine na naomba lisiwape khofu.

Najua kibinadamu walifikiria kwamba labda kama kaja Rais mpya bila shaka na sisi pengine tunachekechwa huko ili tupanguliwe au tuondolewe. Sasa hayo ni mamlaka ya Mhe. Rais lakini kisheria wao wanaendelea na kazi zao, nyadhifa zao na yale mengine kuhusiana na utaratibu wao mpya wa kazi hayo serikali inayashughulikia chini ya Mfumo Mpya wa Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, labda niseme jambo jengine ambalo Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu hapa alijaribu kulitolea ufafanuzi kuhusiana na mkataba wa *ZAT*. Pamoja na kuungana na yake aliyoyaeleza lakini mimi nasema labda niweke sawa tu labda kumbukumbu ili zitusaidie kwenda sambamba. Kwanza yale aliyosema yote kwamba kwa mujibu wa sheria ni sheria ambayo imeelekeza kuwa, tena sisi tulipoleta mswada tulisema mikataba yote iliopo pale *Airport* baada ya mwaka mmoja yote itakuwa imefutika tuanze upya, tu-*negotiate* upya na wale ambao wanafanya kazi, lakini Baraza likashauri na serikali ikakubali kushauriwa kwamba aa, baada ya miezi sita tu na hicho ndicho kilichotokea lakini serikali ikakaa na *ZAT* ikawasilikiliza matatizo yao na sasa iko katika hatua za kukamilisha utaratibu wa kuwawezesha kuendelea na kazi kwa masharti mapya kwa mujibu wa sheria mpya ambayo ipo. Kwa hivyo, hakuna suala la kuondolewa.

Lakini sheria yenyewe ambayo tuliipitisha sisi hapa Barazani ilisema kwamba ule *monopoly exclusivities* kadiri itakavyowezekana iondoke katika kutoa huduma na hilo ndio serikali ambalo imefanya, kwamba kuimarisha huduma basi kutafuta kampuni ambayo inaweza ikatoa ushinda katika kutoa hizi huduma. Hilo nilisema labda niweke kumbukumbu sawa ni kwamba lilipotolewa mara ya mwanzo bahati mbaya kulikuwa na makosa na serikali ikatoa maelekezo na nalitolea ufafanuzi kwa sababu mimi nilitakiwa kusimamia hilo kuwashauri wenzangu.

Kwa hivyo, hata ile zabuni iliyotolewa mwanzo kama waliofuatilia basi iliondolewa, serikali iliifuta ikasema hii ya kukaribisha makampuni mapya. Serikali ilitoa maelekezo kwamba iondolewe ifutwe mpaka tumalizane na suala la *ZAT* tuliweke katika utaratibu mzuri wa kisheria.

Hatua hizo zilichukuliwa, kwa hivyo mpaka sasa hivi kwa kadiri ya kumbukumbu zangu ni kwamba hakuna kampuni mpya ambayo imeomba, itakapotoka zabuni kampuni inayotaka kuomba kama *Swiss Port*, kama ni nani, lakini itasubiri wakati huo ambao ile zabuni itatolewa rasmi, ilitolewa mara ya mwanzo ikafutwa ndio msimamo mpaka sasa ambao upo. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa hili tulisubiri wakati wake utakapofika na bila shaka serikali sababu ya kuchukua hatua hiyo ni kuhakikisha ile sheria tuliyoiptisha katika Baraza hili tukufu inafuatwa na inasimamiwa vizuri ipasavyo.

Mwisho Mhe. Spika, mimi naomba nizungumzie kidogo tu suala la hoja ya Katiba Mpya. Na hili mimi naomba nizungumzie kwa sababu Waheshimiwa wengi wamelizungumza tena vizuri, kwa ufasaha, kwa busara ya hali ya juu; anayetaka kufahamu kama hakuwafahamu Waheshimiwa walivyozungumza basi huyu atakuwa na tatizo la kufahamu, lakini nadhani limeelezwa vizuri kabisa.

Nasema haya ninayoyasema machache ni kwa sababu tu ya kusaidia kuwatanabahisha wenzetu wananchi. Kwa sababu wakati mwengine mtu anaweza Mwenyezi Mungu akampa uwezo au nafasi na pengine akaitumia vibaya na nafasi moja wenzetu pengine wanaitumia vibaya ni hii ya kuwa Kiongozi wa Dini, wa taasisi ya dini. Kwa sababu ukishakusema dini watu wanakutegemea na wanakuheshimu, sasa unapoitumia vibaya kwa kweli unakuwa watu hukuwatendea haki.

Mimi hiki kikundi wenyewe wanaosema cha UAMSHO waliniomba kuja kukutana na mimi ofisini kwangu na nikawaambia sawa siku fulani njoni na nikakaanao kwa muda wa saa tatu nzima. Walieleza hoja zao moja ya hoja waliyoeleza kwamba sisi bwana Muungano na hili ndilo ambalo wamekwenda kuwapotosha watu kwa bahati mbaya sana, kwamba sisi baada ya kujadili Katiba Mpya tujadili kwanza huu Muungano wenyewe si halali. Wakasema kwa mujibuwa wa '*Fiqhi-l-Usul'* jambo likishakuwa kharamu haliwezi kuhalalika, nikawasilikiza vizuri na mimi nikawauliza, lakini tutakapokuja kuamua huo uhalali wa Muungano tutatumia *Fiqhi-l-Usul* au *Fiqhi-l-dunia* hii sheria yetu ya nchi ndio itakayotumika?

Sasa kama ni hoja hiyo, hiyo hoja haina msingi na kwa nini haina msingi? Haina msingi kwa sababu kama unahoji suala la uhalali wa Muungano suala la uhalali itabidi ufuate sheria tulizonazo za nchi. Lakini tujaalie ukubaliwe huo Muungano au tuseme upige hiyo kura ya maoni useme huu Muungano basi watu wote hatuutaki kwa Zanzibar.

Kwanza suala la msingi la kujiuliza sasa nani watakaopitisha ilo azimio si Baraza hili, ndio hapa ambapo Waheshimiwa wamesema aa, hii tumekubaliana sisi hii ni *Representative Democracy*, Bara hili ndilo lililopewa mamlaka hayo ya kupitisha hilo azimio lenyewe. Kwa sababu sasa hivi badala ya kuwa-*engage* hawa Wajumbe wa Baraza wenyewe badala ya kuwa unakaa huko na kuanza kuwatukana unataka nani aje apitishe hilo azimio. Wao wanahubiri amani Wajumbe wa Baraza wewe unahubiri fujo sasa mwisho wa siku nani apitishe hilo azimio.

Lakini kwa utaratibu huo hata azimio Baraza hili likipitisha kwa mujibu wa ibara ya 1998 ya Katiba ya Muungano inabidi suala liende Bungeni na wakubali Wabunge wa Bara *two third majority* wakubali Wabunge wa Zanzibar *two third majority*. Sasa hawa Wabunge wa Zanzibar hujawa-*engage* unafanyia fujo wao wanahubiri amani kwanza watapitishaje? Wakikataa wale wenzetu *two third majority* huo Muungano unaosema uishe utakwishaje. Sasa unawapeleka watu katika njia ambayo mwisho wake *almost* haiwezekani.

Lakini leo imekuja njia hii ambayo hilo unalolitaka, maana yake kumetengenezwa barabara ya lami unaweza ukapita kama alivyosema Mwenyekiti wa Tume wewe peleka. Uzuri wa Sheria hii ya Marekebisho ya Katiba imeeleza kwamba watu watachukuliwa maoni, halafu zitakuwa *forum* kujadili je, maoni yao yamechukuliwa? Halafu litaundwa Bunge la Katiba ambapo wawakilishi wote hao watakuwemo kwenye Bunge hilo na maamuzi itakuwa Zanzibar pia ina maamuzi na baada ya hapo watakachoamua hao Wabunge wa Bunge la Katiba litarudi kwa wananchi. Sasa hii njia unayotaka kuwapitisha watu wewe ni pori tupu, hii njia ambayo imewekwa wazi *you can see all the stairs* kwa nini uwapitishe watu katika *dead end* wakati njia sahihi, nyeupe ipo imewekwa.

Mimi ndio maana nasema watu wetu, wenzetu wananchi ni vizuri wapime hiyo njia wanayotaka kupelekwa na hawa watu, hawa wanataka kuwatia porini wakati njia nyeupe ipo tena imetandikwa vizuri kwenye sheria na hii sheria kwa bahati nzuri imeandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza. Labda kazi mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watusaidie au tusaidiane katika kuwaelimisha wananchi kwamba njia nyeupe ipo, hii tunayohubiri ndio njia nyeupe lakini ukitaka njia hiyo njia nyengine labda kama umejitayarisha vita. Kwa sababu wakikataa wenzetu utakwenda kupigana vita? ndio maana yake.

Sasa mimi ninachosema ni kwamba nawaomba sana watu waelewe kwamba vurugu na fujo haitosaidia na mwisho itakuwa kichekesho kweli kweli Mhe. Spika. Kwa sababu wewe kama unawatetea watu wa Zanzibar halafu watu wa Zanzibar ndio unaowafanyia fujo, maduka yanafungwa, nyumba zao zinaingia mabomu, sasa wewe wakili gani wa kwamba yule unayemtetea ndiye unayemuathiri, yule mgomvi wako kakaa bukheri hana wasiwasi. Hizi nadhani kweli, mimi nadhani watu watafakari maana yake tatizo la hili jambo wala halihitaji darasa ukiangalia unaona hapa pana tatizo, halafu wakili anayekwambia mimi nitakutetea mpaka upate nchi yake yeye mwenyewe kushitakiwa kwa maandamano katafuta wakili, lakini huyu anasema anaweza kutengeneza hoja ya kisheria mpaka akakubatia wewe nchi yako. Jamani si jambo la ajabu?

Sasa mimi naomba watu wakae watanabahi, watafakari hili jambo wataona kwamba hapa wenzetu hawana nia ya kututetea, hawana nia ya maslahi ya nchi yetu isipokuwa labda wana ajenda yao ya siri.

Mhe. Spika, mimi nilisema niseme hayo machache kwa sababu nadhani yatasaidia labda kufumbua macho kwa anayetaka kuyafumbua. Lakini baada ya kusema hayo na mimi niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Wahehsimiwa Wajumbe hapana shaka makofi hayo ya kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa maelezo, kwa hotuba aliyotoa akiwa anasaidia hoja mbali mbali ambazo zimetolewa hapa, lakini pia hata hoja ambazo zinatoka kwa wananchi. Muda uliyobaki ni dakika 25, hii ni shughuli kubwa muhimu ambayo ni vizuri tukaitafakari vizuri sana.

Sasa ni juu yetu Waheshimiwa Wajumbe tukiona kazi hii tuimalize sasa hivi nimwambie Mheshimiwa hapa atoe hoja, la kwamba muwafaka wetu na kwa vile jinsi tunavyoona inafaa ili shughuli hizi ziende vizuri tutafakari haya yaliyozungumzwa sasa hivi basi pengine shughuli hii tuifanya kesho. Niliona tufanye hivi kwa sababu haiwezekani Waheshimiwa Wajumbe waseme maneno mengi, wahoji mengi bila ya serikali kutoa majibu kuhusu hayo.
Kwa hivyo, mawaziri wote wale ambao waliomba na kuna jambo waliseme kumsaidia Mhe. Waziri. Nashukuru kunisikiliza kwa makini na nadhani inafaa sana kutafakari hayo pamoja na Mhe. Waziri kwenda kujitayarisha vizuri zaidi. Kwa sababu bajeti hii tukiipitisha vizuri mswada ule utaokuja baada ya kazi hii nao unakuwa ni mwepesi. Kwa mtazamo huu na kwa furaha hii basi naomba tusitishe shughuli zetu kuanzia sasa na kuahirisha kikao hiki hadi kesho.

(Saa 1:20 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 21/6/2012 saa 3:00 asubuhi)